

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 29 Agosti, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Yustino Ndugai) Alisoma Dua*

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na kipindi cha Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninayo orodha hapa ya Waheshimiwa waliokwisha jiandikisha tayari.

Lakini kama ilivyo ada swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe – Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana, kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Swali la Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika siku za hivi karibuni, pameonekana kutokea mvutano wa Kidiplomasia kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Rwanda. Hali hii imepelekea kutengwa kwa Tanzania kwenye shughuli mbalimbali ambazo pengine zingelionekana zingelistahili kuwa za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nini kauli ya Serikali kuhusu jambo hili? Na nini mkakati wa Serikali kujaribu kumaliza tatizo hili? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijaribu kutoa maelezo kidogo kuhusu swali la Mheshimiwa Freeman Mbowe – Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni.

Ni kweli kwamba kwa muda hivi sasa tumekuwa na dalili za kutokuelewana kati ya nchi hizi mbili, na pengine niseme hasa upande wa Rwanda ambao ndiyo wameonekana kulibeba kwa nguvu sana.

Hasa Mheshimiwa Freeman A. Mbowe anachokisema ni kwamba hii inaashiria dalili za vile vile kutaka kuitenga Tanzania kutoka katika kundi hili la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Lakini kubwa ni lile kwamba kuna mikakati gani sasa kwa upande wa Serikali kujaribu pengine kupata suluhu ya jambo hili ili tusiendele kuwa na mivutano kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika hotuba ya mwisho wa mwezi uliopita, alijaribu kueleza

jambo hili kuonyesha nini kilichofanyika na kikasabisha hiyo hali, ambayo kwa kweli kama mmemsikiliza vizuri, alisema Tanzania haina uhasama na Rwanda hata kidogo. Wala haiwezi kusema ina *offence* dhidi ya nchi hiyo hata kidogo.

Sasa pamoja na maelezo ya Rais, na kauli ambazo zimerudiwa na baadhi ya viongozi kujaribu kuonyesha hiyo hali, ni kweli bado kunaonekana dalili za wenzetu pengine hawajalichukulia kwa namna ambavyo sisi tunalitazama.

Kwa kuwa tangu mambo haya yaanze hatujapata tatizo la pengine mikutano ya Jumuiya ama kususiwa, kwa sababu hatujapata kikao cha kuweza kuwakutanisha, ni jambo ambalo tutaendelea kuliangalia ili kuona kama tutafikia hatua hiyo au hapana. Lakini mimi ninavyojua, Rais amemwomba Rais wa Uganda, Rais Yoweri Museveni, ajaribu kuona ni namna gani hili jambo linaweza likasuluhishwa na maneno haya yakapungua watu tuendeleo kuchapa kazi kama ambavyo tumekuwa tukifanya.

Kwa hiyo, ninaamini busara zitatumika kuhakikisha kwamba jambo hili linakwisha vizuri. Sasa kama litaendelea na kama tutafikia hatua hiyo, basi tutasubiri tuone wakati huo, yatakayokuwa yametokea, sasa hatua ambazo zinaashiria wazi kabisa kwamba pengine ndiyo haya unayoyasema Mheshimiwa sasa yametekelezwa, basi nadhani busara kubwa zaidi zitahitajika. Ninachoweza kusema kwa kifupi ni hilo tu.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoonekana katika mgogoro huu, ni kwamba wenzetu

wa Rwanda wameweza kuwavuta Waganda na Wakenya katika mikakati yao ambayo katika mazingira ya kawaida ingelikuwa ni mikakati ya Afrika Mashariki, ikiwemo matumizi ya Bandari zetu za Afrika Mashariki.

Ni kweli kwamba baadhi ya viongozi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki wamekutana Kampala, na viongozi hawa vile vile wamekutana tena Kenya, ikijumuisha mikutano ya Wakuu wa Nchi za Kenya, Uganda na Rwanda. Ni dhahiri hicho ni kiashiria tosha Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba tunaelekea kutengwa.

La pili, ghafla kumezuka mvutano kuhusu wapi Bunge la Afrika ya Mashariki likae. Kwa mujibu wa Protokali ya Afrika ya Mashariki, Bunge la Afrika ya Mashariki linakaa Arusha. Lakini ghafla pamekuwepo na *madai* ya Wabunge kutoka nchi nyingine za Afrika ya Mashariki kutaka Vikao vya Bunge viwe vinazunguka kwa maana vikae Tanzania, vikae Uganda, vikae Kenya, Rwanda na Burundi, kwa maana ya *Members* wote wa Afrika ya Mashariki.

Jambo hili linaonekana kuungwa mkono na wengine wote isipokuwa Tanzania. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kiashiria gani cha ziada mnachokitaka? Kwa sababu hata huyo msuluhishi mnaye mzungumza kwamba mmejaribu kumshawishi pengine atafute mawasiliano naye ni sehemu ya hilo hilo kundi ambalo linaloonekana kuelekea kuitenga Tanzania. (*Makofi*)

*Politics* ni *lobbying*. Wenzetu wamekuwa makini katika ku-*lobby*, wenzetu wame-*lobby* katika *International Community*, wenzetu wame-*lobby* katika *International*

*Media*, na sisi kwa upande wetu sina hakika tumefanya nini?

**NAIBU SPIKA:** Swali.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Tumefanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu haoni sasa ni muda muafaka Serikali iunde chombo maalum cha kushughulikia mgogoro huu kwanza kutoka ndani mwetu, kikae kiweze kuchunguza jambo hili, kisha kione kishirikishe watu gani katika *International Community*, kwa sababu siamini kwamba ni Sera ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kugombana na majirani zake?  
(*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimesema kwamba, kilichohitajika hapa kwa kweli Mheshimiwa Freeman Mbowe ni busara tu. Busara zikitumika tunaweza kabisa tukatoka hapo tulipo. Mimi sidhani hata kama Tanzania tunahitaji sasa kutafuta jopo la ku-*lobby* na nini hata kidogo.

Kwa sababu chanzo chake ni kauli ya Rais, au ushauri wa Rais alioutoa katika moja ya vikao tena vya ngazi ya juu walipokuwa Addis Ababa. Na jambo lile ni jema tu. Kwamba jamani tunajua mna tatizo la kutokuelewana baina ya Rwanda na vikundi vya waasi.

Ushauri kwamba mimi kwa maoni yangu, busara nzuri hapa ni kuona namna ya kukaa pamoja tuone wapi

tumekoseana, tuone kama tunaweza tukasuluhisha hili jambo kwa maslahi ya wananchi wa nchi zetu zinazohusika.

Kwa kweli ukiutazama ni ushauri mzuri tu. Katika mazingira ya kawaida, ni ushauri ambao unatolewa, unaweza ukasema mimi katika hali tu tuliyonayo mzee si lazima tufanye hayo mambo, mimi ninaendelea na msimamo wangu na ukaendelea tu. Tatizo ni pale ambapo jambo hili limesemwa katika mazingira ambayo ni ya kirafiki ya upendo kabisa. Lakini linatoka nje sasa linachukuliwa kama vile ni bango la uhasama mkubwa kati ya nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namba niungane na Mheshimiwa Rais. Tanzania haina sababu hata kidogo kama msingi wake ni huu. Wa kusema pengine tujenge uhasama kati ya nchi hizi mbili. Tunajua nafasi ya Tanzania ni nini katika *East Africa*. Tunajua hata katika nchi zote za Maziwa Makuu nafasi ya Tanzania ni nini. (*Makofi*)

Nchi hii, ndiyo imekuwa kimbilio la wakimbizi wa nchi zote hizo miaka yote. Leo kauli hii kweli ndiyo izifikishe nchi hizi ambazo zote kwa namna moja au nyingine tumesaidiana katika kutatua migogoro yao ya ndani kwamba leo sasa ni sababu ya kuweza kufikia hapo. Mimi siamini hilo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi ninachoweza kufikiria tu hapa ni kwamba tuendeleo kulitazama jambo hili kwa uzito wake. Tusipuuze, lakini nina hakika kwamba itafika mahali watu wataona kwamba kama jambo lenyewe ni hili, hapakuwa na sababu yoyote ya kufikia hatua hiyo. (*Makofi*)

Sasa wazo lako la jopo na kujaribu kuanza ku-*lobby* pengine ni jambo ambalo Mheshimiwa Rais pengine hivi ninavyozungumza naye ananisikiliza, lakini ninahakika ukimuuliza atasema sasa nika-*lobby* wapi. Kwa lipi? Kwa hili!  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mimi sidhani hata kidogo.  
(*Makofi*)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa nimwulize swali moja Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaelewa kwamba elimu duniani kote inaonekana kuwa ndiyo suluhisho la vikwazo vyote ambavyo vinasababisha uchumi na hata maendeleo ya kijamii pamoja na ya kisiasa kwa Taifa lolote lile vieweze kuondoka.

Hapa Tanzania, kupitia *programme* ya *Big Result Now* kwa maana ya Matokeo Makubwa Sasa, inaonekana kwamba ndani ya Wizara ya Elimu hali haiko shwari. Ninasema hivyo kwa sababu ninayo mitihani hapa ambayo imeandaliwa na Wizara ya Elimu na kuweza kuwapelekea vijana wetu wa Elimu za Msingi, kupitia programu hii ya matokeo makubwa sasa waweze kuandaliwa ili waweze kuja kulitumikia Taifa letu.

Lakini ukikamata kwa mfano mtihani huu wa lugha ya Kiingereza, kwenye kipengele tu kimoja cha Ufahamu kwa maana ya (*Comprehension*) inasikitisha sana unapoweza

kukutana na baadhi ya maswali ambayo haiingii akilini kwa mtu yeyote ambaye kwamba anaona kwamba ni kitu gani ambacho mwanafunzi alipashwa kupimwa nacho.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ningelipenda nikuulize swali moja.

Je, uko tayari kuweza kuwashughulikia watu wote ambao wametunga na kupitisha mtihani huu mbovu ambao hauwezi ukapima maarifa, ujuzi, mwelekeo pamoja na tabia ambazo wanafunzi wamekusudiwa waweze kuzipata wawapo shule?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Uliza swali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kwa sababu mtihani uko chini ya viwango?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba sana wote wanaofuata waende kwenye swali moja kwa moja kwa sababu dakika zetu ni kidogo sana, na nina orodha ndefu hapa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Moses J. Machali, wewe umepata karatasi ya Maswali. Ambayo ni maswali kwa ajili ya mtihani, kama ulivyosema. Nilitaka kuuliza ni mtihani upi sasa maana hukufafanua vizuri. Ni hiyo iliyopita au ni hiyo inayokuja? *(Kicheko/Makofi)*

Ndiyo. Nifafanulie tu kwa sababu vinginevyo itakuwa vigumu kidogo.



**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kwamba huu ni mtihani ambao umeandaliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Darasa la Saba katika mchakato wa kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanaandaliwa kikamilifu. Lakini ni mtihani ambao uko chini ya viwango na umefanywa tarehe 9 Julai, 2013.

**WAZIRI MKUU:** Kwa hiyo, wewe umepata karatasi ya maswali ambayo kwa kawadia huwa ni siri mpaka wakati wa mtihani wenyewe.

**MBUNGE FULANI:** Umeisha fanyika.

**WAZIRI MKUU:** Umeisha fanyika?

**NAIBU SPIKA:** Liweke wazi Mheshimiwa Machali kwa kifupi sana.

**WAZIRI MKUU:** Mbona niliuliza...

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mtihani ambao umeishafanyika.

**WAZIRI MKUU:** Sawa sasa. Swali hili kwa sababu unaniuliza mimi unanipa kazi ya kuwashughulikia wale waliotunga mtihani huo kwa kile ambacho kwa uelewa wako umekiona kiko chini ya kiwango na hakiwezi kumsaidia mtoto wa darasa la saba.

Ninachoweza kukuambia sana sana. Hilo jambo Waziri wa Elimu nadhani amesikia. Tutamkabidhi hiyo kazi.

*Professionally* mimi siyo mwalimu wala sihusiki na masuala haya kwa maana ya utunzi wa mitihani yenyewe. Waliangalie ili tuone ni majibu gani watakayonipatia halafu mimi nitakueleza kwamba ni mambo gani wameyabaini katika utunzi huo wa mitihani. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Moses Joseph Machali nitakuomba uweke mezani.

Waheshimiwa Wabunge ninaomba tusaidiane wote kwa pamoja tuwe tunaangalia saa. Bahati mbaya na Katibu ameondoa saa ya upande huu. Ninao watu kumi ambao wanachangia hapa. Tusipokuwa makini ni shida. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa majibu yake.

Ninaomba ni-*declare* kwamba mimi ni Mwalimu ki-taaluma. Kwa kuwa mtihani huu nina hoja zenye idhibati kwamba ni mtihani dhaifu na hafifu usiofaa. Kwa mfano swali moja linasema: *What do we call a citizen of Tanzania.* Na mengineyo mengi.

Je, kwa kuwa Wizara hii hii, ni wazi kwamba wale watu ambao wameruhusu kitu hiki kiende kikafanyike hawakuwa makini ndiyo maana wameruhusu jambo hili liende likafanyike, Kuna sababu gani Serikali yako isiweze kuchukua hatua hakuna suala la kufanya uchunguzi kwenye suala hili, ni jambo ambalo liko wazi Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MBUNGE FULANI:** Ni kweli.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Machali, hapa tunachozungumza ni uendeshaji tu wa shughuli za Serikali, wewe una bahati kwamba ni Mwalimu. Mimi si mwalimu, umepata bahati umeona orodha hiyo ya maswali, na ukayapa tafsiri na umetoa hukumu tayari. Unaponiambia mimi kwamba nichukue hatua kwa watumishi waliotunga ndilo ninalokuambia siwezi. *(Makofi)*

Hilo jambo acha lilirudi kwenye Wizara ya Kisekta, watazame hayo unayoyasema, nitakapokuwa nimepewa maelezo naweza sasa nikajua ni hatua gani stahiki niweze kuchukua. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushuru kwa kunipatia fursa hii adimu ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Je Mheshimiwa Waziri Mkuu anafahamu kwamba utoaji wa Vitambulisho vya Taifa, ulioanza Februari, 2013, hadi leo hii mwisho wa mwezi Agosti, 2013, ni Jimbo moja tu la Kigamboni ambako wameandikishwa wote.

Mheshimiwa Rais amewahi kuzungumzia kuhusu vitambulisho hivyo na vitakavyofaa mpaka kufika kupigia kura mwaka 2015. Hali hii inaonekana kidogo kusuasua.

Je, unaweza kuliambia Bunge hili Tukufu, nini kinaendelea na azma iliyokusudiwa kwamba Watanzania

wote wanaweza wakapata vitambulisho hivi vya Taifa kabla ya uchaguzi wa mwaka 2015 na kusuasua huku kwa *NIDA* kunakoendelea, ni nini kauli ya Serikali?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, analolisema Mheshimiwa Eng. Mnyaa, lina ukweli kwa kiasi fulani kwa sababu zoezi lile wametenga maeneo wanakwenda hatua kwa hatua au kanda ukitaka kutumia lugha nyepesi zaidi. Inaonekana kama vile linaweza likachukua muda mrefu na iko hofu na sisi wewe tu, kuna wengine kama wawili hivi wameniambia kwamba sisi tungelipenda vitambulisho hivi vipatikane mapema kabla hatujafikia kwenye uchaguzi mkuu.

Nilipozungumza na Mtendaji Mkuu ndiye aliyenipa haya maelezo haya kwamba ni kweli linatoa picha hiyo lakini jitihada zinafanyika kubwa ili kuhakikisha zoezi hilo linakamilika mapema kabla hatujafika kwenye hatua ile ya Uchaguzi Mkuu. Sasa kwa sababu ni *concern* ya kila mtu itabidi tuliangalie tuone kama kuna namna nyingine ya kuweza kuharakisha zaidi au kupanua wigo wa zoezi lile ili liweze kuwa na matokeo ambayo ni ya haraka zaidi.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Bunge hili tunategemea kupitisha Muswada wa kura ya maoni, kura ya maoni huenda ikafanyika kabla ya Uchaguzi wa 2015. Tume ya Uchaguzi hadi hivi leo haijaboresha Daftari la Wapiga Kura.

Je, kuna uwiano gani au utatuambia nini sasa kwamba ikiwa vile vitambulisho tutaweza kufanikiwa

kulipata kabla ya mwaka 2015. Je, hii kura maoni tutatumia chombo gani cha kupiga kura hii ya maoni?

**WAZIRI MKUU:** Mimi nafikiri acha tulitazame maana hili ni letu ni la Serikali tunajua mpango ulivyo hoja yako nimeielewa na hofu hiyo uliyonayo wala siyo ya kwako peke yako wako wengi ambao wana hofu hiyo. Lakini sisi tumejiaminisha kwamba tutaweza kufanikisha zoezi hilo. Lakini hatuwezi kupuuza au kufanya jambo hili kama dogo hapana na mimi *I will take it up* halafu tutaona kama kweli tutafeli tutafanya nini lakini nadhani hatutashindwa kulifikisha pale ambapo Watanzania wanataka. (*Makofi*)

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu kumejitokeza katika kukuza uchumi wetu kuna tatizo kwa zaidi ya miaka 20 hivi sasa mabasi hayasafiri usiku na wananchi wamekuwa na mahitajio makubwa sana.

Je, zuio hili litakuwa ni la kudumu maisha au ni lini Serikali itaondoa zuio mabasi yaweze kusafiri masaa 24?

**WAZIRI MKUU:** Labda tujitumainishe Mheshimiwa Mangungu kwamba haitadumu siku zote kwa sababu hatua hii ilichukuliwa kutokana na ajali ambazo zilikuwa zinajitokeza hasa usiku kwa wingi ndiyo maana wakafika mahali wakaweka ule utaratibu.

Lakini napenda niamini kabisa kwamba kadiri muda unavyokwenda, kadiri barabara zinavyoboreshwa inawezekana maamuzi haya ambayo kwa kweli yaliamuliwa kukidhi mazingira fulani inaweza pengine

ikaondolewa na utaratibu ni wa kawaida na watu wakasafiri kama tulivyokuwa tunafanya zamani.

Lakini ni kweli itabidi elimu kubwa itolewe kwa madereva na pengine kuingilia kati hata kuweka utaratibu mahususi badala ya dereva mmoja tu ndiye anaendesha gari usiku kucha wakati mwingine inaleta taabu.

Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba pengine ni hatua tu ilikuwa ya mpito lakini kama hofu bado ipo ya ajali basi ni juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani kuangalia tuone namna gani tunaweza kuboresha muda.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Kumekuwa na tatizo la uporaji katika mabasi ambayo yanatembea hata mchana, mfano mzuri ni vijana wa *Clouds FM* walikuwa wanasafiri kutoka Kigoma lakini mabasi ya abiria yameporwa kutoka Bukoba kwenda Biharamulo ni tatizo ambalo limekuwepo na Naibu Waziri Mkuu aliyetoa agizo la kusitisha hii yupo Bungeni hapa.

Je, Serikali inawahakikishiaje wananchi kuhusu usalama wa usafiri na mali zao?

**WAZIRI MKUU:** Nilitaka nimwombe Mheshimiwa aliyekuwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu aje atoe maelezo lakini kwa bahati mbaya utaratibu hauruhusu. (*Makofi*)

Analolisema Mheshimiwa Mangungu ni kweli, tumekuwa na matukio ya hapa na pale ambayo ni ya uvunjifu tu wa amani tu kwa upande wa Tanzania wale wanaosafiri kwa njia salama kabisa. Lakini Serikali vilevile

imekuwa ikichukua hatua kadhaa kujaribu kudhibiti jambo hilo, tulifika hatua hata kuweka askari kusindikiza mabasi kwa hiyo mimi nadhani ni kitu ambacho tunakijua na tunajitahidi sana kukisimamia kwa karibu sana.

Lakini tunatoa rai mara nyingi sana kwa Tanzania hasa kwenye yale maeneo ambayo yana tabia hiyo au dalili hizo kwa mara nyingi na wenyewe waisaidie Serikali kuweza kufichua baadhi ya majambazi ambao ndiyo yanayofanya makosa hayo.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 18(1) kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa mawazo yake nje bila kuathiri sheria za nchi. Na kwa kuwa Waziri au Kiongozi yeyote ni katika watu ambao kwa mujibu wa ibara na kifungu cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano nilichokitaja yuko huru kuwa maoni yoyote na kutoa mawazo yake nje.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, unatoa kauli gani kwa Chama cha Siasa kuwazuia watu wake kuwa huru na kutoa maoni hasa yanayohusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Sijui kama swali hili limeeleweka vizuri, Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa bahati mbaya ameweka usiri mwingi pale sasa sielewi chama gani

hicho cha siasa na kimefanyaje kuwazuia watu. Maana angenisaidia kutaja Chama fulani labda kilifanya hivi.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nirudie kama hujafahamu.

**WABUNGE:** Haaaaa! Taja chama.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Chama cha Mapinduzi, CCM...  
(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Chama hicho kimefanya nini, wapi, nini yaani... Mheshimiwa Khatibu kuwa muwazi unauliza kitu gani moja kwa moja. (*Makofi*)

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba niulize swali la pili utanifahamu zaidi. Kwa kuwa uamuzi uliochukuliwa dhidi ya Mheshimiwa Mansour Yussuf Himid, ambaye alikuwa Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar... (*Makofi*)

*(Hapa mic ilizimika ghafla)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haji, swali ni moja na swali hilo halibadiliki linabakia kuwa moja kuwa sawa na Wabunge wengine. Mheshimiwa Waziri Mkuu lile la kwanza sijui kama...

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina hakika Mheshimiwa Haji katika hili sidhani kama



unanitendea haki, maana hata chama chako chenyewe mlifanya hivyo. *(Makofi)*

Maana tusioneane hapa. *(Makofi/Vigelegele)*

Ingawa Mbunge bado yupo na anaendelea na Bunge kama kawaida. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Kwa kuwa mchakato unaendelea sasa hivi wa kuandika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rasimu tumeishaipata uchaguzi ni matokeo ya Katiba, Bunge, Serikali ni mtoto wa Katiba na kwa kuwa vinajionyesha viashiria mbalimbali ambapo tunaweza tusipate Katiba mwezi wa nne mwaka ujao, viashiria ambavyo viko vingi vya misimamo ya makundi mbalimbali ikiweko ya kisiasa na uongozi inabidi utumie hekima ku-*anticipate* ni kitu gani kitatokea endapo muda uliopangwa hatutapata Katiba hiyo.

Je, Serikali imejiandaa vipi kuwa na *fall-back position* ili kuweza kuifanya Serikali kuwa *pro-active* badala ya kusubiri mpaka tukio litokee ili liweze likawa *reactive*?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, anachokisema Mheshimiwa Mbatia ni tahadhari ni nzuri mimi nafikiri kwa Serikali lakini na Watanzania wote tu kwamba katika mazingira ya mchakato wa kuandika Katiba lolote pengine linaweza likatokea kwa sababu linategemea mambo mengi.

Ninachoweza kusema tu kwa uhakika ni kwamba Serikali imeshalitazama hilo inalijua na *of course* tumekuwa na njia mbalimbali za kujaribu kuona je, likitokea hili, je kama litatokea hili kwa hiyo, yako mawazo yote haya na yote tunayazingatia.

Kwa hiyo, napenda niamini kwamba kama itafika matokeo ambayo yatakuwa yamejitokeza yakawa yale ambayo yanaonyesha kwamba hatutafika mwisho wa safari basi nadhani kwa mawazo yaliyomo Serikalini ninafikiri tutakuwa na kauli wakati huo kwa sababu tusianze kudhani kwamba halitawezekana hapana.

Kwa hiyo, mimi nafikiri tuendeleo kuamini litawezekana isipokuwa tu kama ikitokea hiyo *then* tunaweza tukaja na kauli fulani hivi.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na nashukuru majibu ya Waziri Mkuu, kwa kuwa ku-*anticipate* na kuweza kuwa na *mitigation measures* endapo jambo hili litatokea na ili kupanua wigo zaidi haoni kwamba ni busara kwa kuwa Serikali ni imekuwa dhamana hii lakini yako makundi mengine katika jamii ambayo ni muhimu pia ambayo yanashiriki katika kiasi kikubwa katika mchakato huu wa Katiba na nia yao ni kushirikishwa katika meza ya mazungumzo kabla ya *deadline* haijafikia na endapo ikitokea hivyo basi unakuwa na *fall back position* ya (a), (b), (c) au (d) ili ikakubalika badala ya kuanza kurushiana maneno wakati muda tutakuwa hatuko nao tena na tutakuwa *reactive* zaidi badala ya kuwa *pro-active*?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ushauri mzuri tu mimi sidhani kama una tatizo hata kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana muda wa nusu saa umeshapita, ahsante sana kwa kujibu maswali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumeweza kupata maswali sita (6) lakini tunapenda katika kipindi hiki cha nusu saa tuwe tunapata maswali manane (8). Kwa hiyo, bado tunaendelea kusisitiza umuhimu wa kuwa na maswali mafupi. Katibu tuendeleo.

### **MASWALI NA MAJIBU YA KAWAIDA**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali ya kawaida, Ofisi ya Waziri Mkuu, naomba nimuite Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 29

### **Wawekezaji Waliopewa Mashamba ya Hanang'**

**MHE. ROSE K. SUKUM** aliuliza:-

Kufuatia mikataba ya wawekezaji wa mashamba ya Murjanda, Mulbadaw, Setcheti na Gidagamowd, kutonufaisha Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' imesababisha mgogoro na wananchi wanaozunguka maeneo hayo ambayo hayalimwi na mwekezaji huyo:-

(a) Je, ni kwanini Serikali inaendelea kumkumbatia mwekezaji huyo wakati wakulima wa Hanang' kwa umoja wao wana uwezo wa kuwa wawekezaji kwa kulima mashamba hayo na kuinufaisha Halmashauri?

(b) Je, Serikali inawaambia nini wafugaji wa Hanang' wanaolishia mifugo yao kwenye maeneo ambayo hayalimwi na mwekezaji huyo lakini wanapokamatwa hupigwa faini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba ya ngano ya Murjanda, Mulbadaw, Setcheti na Gidagamowd yalikuwa ni sehemu ya mashamba saba (7) ya ngano yaliyokuwa chini ya *NAFCO* yaliyojulikana kama *Hanang' Wheat Complex* wakati wabinafsishaji mashamba ya Murjanda, Setcheti na Gidagamowd yaliuzwa kwa njia ya ufilisi kwa kampuni ya *Ngano Limited* na shamba la Mulbadaw, liliuzwa kwa kampuni ya *Haydom Lutheran Hospital and Development Limited*.

Aidha, mashamba ya Gawal na Warret yalikabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' kwa ajili ya kugawiwa wananchi kwa shughuli za kilimo na ufugaji. Shamba la Basotu halijauzwa na Serikali kupitia Shirika Hodhi

ya mali za Masharika ya Umma (CHC) linakamilisha taratibu za kubinafsisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Aprili, 2013 Serikali ilifanya tathmini kubaini matumizi ya mashamba ya ngano ya Mulbadaw, Murjanda Setchet na Gidagamowd. Tathmini hiyo ililenga kujua eneo linalolimwa na maeneo yanayobaki bila kulimwa, uzalishaji wa kila shamba mahusiano ya wawekezaji na jamii inayozunguka mashamba hayo na manufaa yanayopatikana kwa jamii kwa kuwepo kwa wawekezaji wa mashamba hayo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini hiyo ilionyesha mambo makuu mawili kama ifuatavyo,

(a) Wawekezaji katika mashamba makubwa hawatumii maeneo yote ya mashamba yao.

(b) Kuna migogoro kati ya jamii inayozunguka mashamba na wawekezaji kama vile wananchi kuvamia mashamba ya wawekezaji kwa kulima na kuchungia mifugo bila ridhaa ya wawekezaji na wakati mwingine wawekezaji kuwabugudhi wananchi. Aidha, kuna migogoro ya mashamba na vijiji vinavyozunguka.

Ili kutatua changamoto hizo imemwagiza mwekezaji kuandaa mpango wenye malengo ya muda mfupi wakati na mrefu ili kuhakikisha analima mashamba hayo yote, endapo atashindwa kufanya hivyo hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yake. Aidha, wawekezaji na wananchi wameelekezwa kuunda Kamati ya pamoja ya viongozi,

wananchi na wawekezaji ya kushughulikia migogoro inayojitokeza.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba ya uwekezaji yaliyoko wilayani Hanang' yametolewa kisheria na kwa taratibu zote za Serikali. Hivyo ni mali halali ya wawekezaji na kuingiza mifugo kwenye mashamba haya ni kinyume cha sheria. Katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa ardhi ya kilimo na ufugaji Serikali iliwigawia wananchi wa Hanang' mashamba ya Gawal na Warret yenye ukubwa wa hekta 10,400 kwa ajili ya matumizi ya malisho na kilimo.

Ninawahasa wananchi wa Wilaya ya Hanang' wanaozunguka maeneo ya mashamba ya uwekezaji waache kuzamia na kuchunga mifugo katika mashamba hayo wakati kuna mazao ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima.

Napenda kuwakumbusha wawekezaji kuanzisha miradi itakayowanufaisha wananchi ili kuleta uhusiano mzuri. Pia natoa wito kwa viongozi wa Wilaya, Halmashauri na wanasiasa waendeleo kushirikiana na wananchi pamoja na wawekezaji ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili kuepusha migogoro.

**MHE. ROSE KAMILI SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, majibu ya Mheshimiwa Waziri hayakukidhi haja. Swali langu lilielekea kwenye suala la kwamba mwekezaji halipi inavyopasa cess ya Halmashauri ya Hanang. Kwa wastani shamba hilo au mashamba hayo ambayo yana eka 30,000 angezilima angeweza kupata kiasi cha shilingi bilioni 18 kwa maana ya kwamba eka moja

inatoa gunia kumi za ngano na cess ya Hanang ingekuwa ni kiasi cha shilingi milioni 540 lakini mpaka sasa hivi mwekezaji analipa kiasi kidogo sana cha milioni 100 tu.

Je, haionekani kwamba hii ni hasara kwa Wilaya Hanang kwa huyu mwekezaji ndiyo maana nimesema kwamba wapewe watu wengine wana Hanang waweze kulima hayo mashamba kwa sababu *NAFCO* ilikuwa inazalisha vizuri na hao wana Hanang wanaweza.

Swali la pili, ni kwamba migogoro ya mwekezaji pamoja na wananchi inatokana na yeye kuacha maeneo yale kama pori, sasa linapokuwa kama pori hata kama sheria inamlinda kwamba ni eneo lake na sheria gani inayomchukulia hatua yeye kuacha eneo la Hanang kama pori badala ya kulima na analima nusu ya mashamba hayo tu? Ahsante sana. Nataka majibu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rose Sukum. Majibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji ambaye ndiye Mbunge wa Hanang.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ni-*declare interest* mimi ni Mbunge wa Jimbo la Hanang. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge naomba vilevile niwajulishe kwamba Mheshimiwa Rose Kamili Sukum ni Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara alikuwa ni Diwani wa Kata ya Basoto ambayo mashamba hayo yapo.

**MHE. ROSE KAMILI SUKUM:** Nijibu swali langu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, kuweka swali lake bayana ambalo halikuwa bayana kwenye swali la msingi. Kwa sababu mambo ya cess hayamo kwenye swali la msingi, lakini ninamshukuru ameweka bayana hilo swali sasa ninalijua kwamba yeye alikuwa anataka kujua habari ya cess.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyoeleza kwamba maeneo yote ya mashamba katika jibu langu la msingi hayalimwi na kwamba ni kweli vilevile tija ya mashamba hayo hayajafikia pale ambapo tungetaka yafikie.

Kwa hivyo, uzalishaji wa mashamba yale kwa vyovyote vile utakuwa chini na kwa hivyo kuathiri ulipaji wa ushuru kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Hanang; na ndiyo maana tumewambia watupe mipango yao ya matumizi ya maeneo waliyopewa ili hatimaye ushuru utakaolipwa Wilaya ya Hanang uwe kama vile Mheshimiwa Rose Kamili Sukum anavyotaka na mimi ninavyotaka uwe shilingi milioni 540.

Kwa hivyo, ni kazi yetu sisi kuwahakikisha kupitia Serikali mimi Waziri na kupitia Halmashauri yetu ya Wilaya ya Hanang kuona kwamba wawekezaji wanalima na kama hawalimwi kama tulivyowaambia tuchukue hatua stahiki kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi na ndivyo



vilivyokuwa nafuatilia mashamba hayo kila siku kama Mbunge wa Jimbo la Hanang. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuhusu migogoro, migogoro ya wawekezaji na wananchi ipo nchi nzima na hususan na Hanang nayo ipo. Ili kuweza kutatua migogoro hii tumewaelekeza wananchi wamekubali na mwekezaji amekubali kwamba tutakuwa na Kamati ya pamoja endapo inatokea migogoro wakae pamoja kuona namna ya kuondoa migogoro hiyo na imetokea awali wameishaifanya hivyo.

Ninaomba katika maeneo yote yenye uwekezaji kuwe na Kamati ya wananchi wanaozunguka eneo lile na wawekezaji kusudi migogoro ambayo inaweza kutatuliwa kwenye maeneo yale iweze kutatuliwa na ninamwomba Mheshimiwa Rose Kamili Sukum ashirikishe na mimi kuona kwamba wawekezaji wanatekeleza wajibu wao, wananchi nao wanashirikiana na Serikali yao kuweza kuona kwamba mashamba yale yananufaisha Wilaya yetu ya Hanang. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu ya uhakika kutoka kwa Mbunge wa Hanang. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele.

Na. 30

**Mikopo Kwa Benki Mazao SACCOS**

**MHE. KAIKA S. TELELE** aliuliza:-

Je, Serikali inaweza kukipatia mkopo kikundi cha Benki Mazao SACCOS cha akinamama wa Ngaresero ili kuimarisha biashara yao na hivyo kupunguza umaskini wa kipato?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kikundi cha Benki Mazao cha akinamama cha Engaresero ni kikundi ambacho kimesajiliwa tarehe 4 Julai, 2013 kwa usajili namba NGOR/DC/GBG/016 kwa mujibu wa Azimio la Baraza la Madiwani la mwaka 2008.

Kikundi hiki kinajishughulisha na kununua, kuhifadhi na kuuza mazao yakiwemo mahindi na maharage. Kikundi hiki kina idadi ya wananchama wapatao 300. SACCOS ni Vyama vya Akiba na Mikopo ambavyo husajiliwa kwa mujibu wa taratibu za usajili wa SACCOS. Hivyo, Kikundi cha Benki Mazao cha akinamama cha Engaresero siyo SACCOS.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kupitia Wadau wa Maendeleo yaani Shirika la OXFARM ilikiwezesha Kikundi cha Benki ya Mazao cha Akinamama cha Engaresero kwa kuwajengea Ghala la mazao na kuwapatia mtaji wa kuanzia kiasi cha Tshs. 15,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana imekuwa ikitoa mikopo kwa vikundi kulingana na uwezo wa Bajeti kupitia utaratibu ufuatao:-

Kikundi husika hutakiwa kujaza fomu za maombi na kuzirejesha kwenye Halmashauri, baada ya hapo wataalam wa Kamati ya Mikopo huzipitia fomu zote zilizowasilishwa katika kipindi cha mwezi moja (1). Vikundi vilivyokubaliwa na Kamati ya mikopo ya Wilaya hupatiwa mafunzo na kisha kuingia Mkataba na Halmashauri kuhusu namna ya kurejesha mkopo husika na baada ya hapo kikundi husika hupewa mkopo.

Kikundi husika hutakiwa kurejesha mkopo ndani ya miezi 12 kwa riba ya asilimia 10 kwa akinamama na asilimia 15 kwa Mfuko wa Vijana. Kwa kufuata utaratibu huu Kikundi cha Benki Mazao cha Akinamama cha Engaresero nacho pia kinaweza kupatiwa mkopo kwa utaratibu huo na taratibu zingine za uwezeshaji.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kiasi kikubwa nimeridhika na maelezo ya Serikali juu ya swali hili. Lakini napenda pia nitumie nafasi kwa niaba ya wananchi wa Ngorongoro na hasa Kikundu cha Ngaresero cha Benki Mazao kushukuru sana Shirika la *OXFARM* kwa kujenga hilo ghala na kuwapa mtaji wa milioni 15,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilikuwa nataka nitoe ushauri wa bure kwa Serikali kwamba uwezo wa

Mfuko wa Wanawake na Vijana katika Halmashauri zetu kuendelea kutoa mikopo namna hii kwa ajili ya akinamama na vijana uwezo wake ni mdogo sana. Je, Serikali inaweza ikafikiria katika bajeti ijayo kuangalia uwezekano wa kuongeza bajeti katika Mfuko huo ili iweze kutoa mikopo zaidi kwa vijana na wanawake? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninamshukuru sana na ninampongeza kuona kwamba vikundi vinapaswa kuimarishwa kwa kupewa mikopo pale vinapohitaji mtaji.

Vilevile ni kweli Mifuko ya Wanawake na Vijana katika Halmashauri zetu hazitoshelezi mahitaji ya mitaji ya akinamana na vijana. Kwa hivyo, kadiri inavyowezekana nina hakika Serikali haiwezi kusita kuongeza Bajeti katika mifuko hii miwili.

Lakini vilevile naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba na Waheshimiwa Wabunge wote kupitia kwako Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba kuna mifuko mingine ya uwezeshaji ambayo vilevile kama Waheshimiwa Wabunge wataweza kufuatilia ile mifuko wanaweza wakaongezea mitaji juu ya mitaji ile ya mifuko hii miwili ambayo ipo kwenye Halmashauri zetu.

Na. 31

**Utekelezaji wa Ahadi za Rais**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka maji katika Jimbo la Mbozi Magharibi, ahadi aliyotoa katika Mkutano wa hadhara wakati wa kampeni za Uchaguzi Tunduma tarehe 29 Agosti, 2010?
- (b) Je, mpaka sasa ni ahadi ngapi alizotoa Mheshimiwa Rais zinazotafsirika kimwonekano zimeshatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Jibu la swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali na Mitaa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Karibu Bungeni mzee tulikukosa sijui ulikuwa wapi? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka huduma za maji katika Jimbo la Mbozi Magharibi.

Katika kutekeleza ahadi hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kwa kushirikana na Wizara ya Maji imekamilisha

utafiti wa vyanzo vya maji na kubaini kwamba vyanzo vyenye uhakika ni eneo la Chapwa na maji ya mtiririko ya Mto Nkana uliopo maeneo ya Kata ya Vwawa. Vyanzo hivi viwili vikitumika vizuri vitapunguza au kumaliza kabisa tatizo la maji katika Mji wa Tunduma na maeneo ya Mpemba na Chiwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Julai, 2013 Serikali imefanikiwa kuchimba visima virefu 5 katika vijiji vya Itumbula, Chilulumo, Mnyuzi, Namtambalala na Iyendwe ambavyo vitatumika kama vyanzo vya kusambaza maji katika vijiji husika. Mradi wa maji katika kijiji cha Namtambalala umekamiika na wananchi 2,779 wananufaika na mradi huu. *(Makofi)*

Ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji cha Chilulumo unaendelea kwa kujenga matanki 3 ya maji, nyumba moja ya pampu na mtandao wa mabomba wa kilomita 3.5.

Aidha, Wizara ya Maji katika Bajeti yake ya mwaka 2013/2014 imetenga jumla ya milioni 100 katika kupanua mtandao wa maji ya Mji wa Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri imesaini makubaliano katika Mpango wa Matokeo Makubwa sasa *(BRN)* wa kusambaza maji katika eneo la lote la Mbozi Magharibi. Serikali imetenga bilioni 9 kupitia Wizara ya Maji kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji kuanzia kipindi cha 2013/2014 hadi 2015/2016.

Lengo la mpango huu ni kuwezesha Jimbo la Mbozi Magharibi kuwa na maji safi na ya uhakika ifikapo mwaka 2015/2016.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za Mheshimiwa Rais ambazo zimetokelezwa katika Jimbo la Mbozi Magharibi mpaka sasa ni upanuzi wa Kituo cha Afya cha Kamsamba kwa gharama ya milioni 300 ambapo ujenzi wa Wodi na chumba cha upasuaji umekamilika Julai, 2013, upatikanaji wa gari la wagonjwa la Kituo cha Afya cha Kamsamba lenye namba za usajili STK 7368 kwa sasa ST 224A ya mwaka 2010 na ujenzi wa daraja la kuunganisha Mkoa wa Rukwa na Mbeya katika kijiji cha Kamsamba ambapo tayari *TANROADS* Mkoa wa Mbeya imefanya usanifu wa mradi huo.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika kipindi changu chote nilichokaa Bungeni sasa hivi miaka miwili na miezi nane katika michango yangu, maswali ya msingi pamoja na ya nyongeza, nimeuliza ama nimechangia mara 27 kuuliza suala la maji, hivi Serikali haioni kabisa kwamba jitihada ninazofanya za kutaka kupeleka maji katika Jimbo la Momba na kwa Watanzania siyo za kwangu mimi kama Silinde ni kwa ajili ya wananchi. Hivyo Serikali sasa hivi haioni haja sasa ya kupeleka haraka na kutwambia ni lini sasa wananchi watapata maji hayo kwa uhakika?

(b) Lakini katika ahadi za Mheshimiwa Rais ambazo zinakwenda kutekelezeka ahadi ya ujenzi wa daraja la kuunganisha Mkoa wa Rukwa pamoja na Mbeya, hii ahadi bado kabisa haijatekelezeka. Sasa tuambiwe ni lini sasa itatekelezeka kwa sababu sasa hivi tangu Rais ameahidi ni mwaka wa tano?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaelewa *concern* ya Mheshimiwa Mbunge, sisi wote hapa ni Wabunge, ukizungumza *issue* ya maji hapa huwezi ukazungumza tu unai-*brush off* hivi kama ni jambo la kawaida.

Ninaweza ikaelewa Mbozi mimi nimefika najua tatizo hili ni kubwa pale Mheshimiwa Silinde anapozungumzia.

Tulichosema hapa katika Mpango wa muda mrefu kama tumewaingiza katika *Big Results Now*, tumeweka bilioni 9 pale, mimi sioni *seriousness* nyingine sijui nitoe wapi sasa? Yaani tukikuingiza kwenye *BRN* na hilo ni Jimbo la Mbozi Magharibi limeingizwa pale.

Sasa kama tumeishaingiza hapo nifanyaje sasa nibebe *file* hapa begani ndiyo ujue kwamba sasa nipo *seriously*. Yaani sisi tuweike hapo kwa sababu ya hii kelele ambayo umekuwa unapiga wewe tukaiweka kwenye *BRN* tukaingiza pale.



Lakini wakati huo huo ukimsikiliza Mheshimiwa Maghembe anavyozungumza hapa Tunduma ule ni Mji mdogo ule, na sasa hivi umekuwa ni Mji pale sasa ni Mamlaka ya Mji. Maeneo yote ya Miji Midogo na Mamlaka za Miji zote Tanzania nzima Serikali imesema hapa kwamba zote tutahakikisha kwamba wanapata maji safi na salama.

Tumeacha hilo tumekwenda kwenye milioni 100 ambazo tumepeleka pale zipo pale na hao wote Wabunge walisimama hapa na wote wakisimama hapa kila mmoja atakueleza matatizo hayo.

Nakuomba Mheshimiwa Silinde uione *seriousness* ya Serikali katika jambo hili na tuangalie kabisa na macho yetu na midomo yetu wala hatutanii, sisi tutaondoka na watu tutakwenda kule kuhakikisha kwamba matokeo haya yanapatikana kweli kama tulivyosema.

La pili, amezungumza habari ya daraja hapa, daraja hili linalozungumzwa hapa akisimama hapa Mheshimiwa Mwakyembe, akisimama hapa Mheshimiwa John Pombe Magufuli, wakisimama wote wale wanaohusika watakwambia huwezi kujenga daraja bila kuwa na kitu kinachoitwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii imeishakamilisha, mzee wangu sauti hii kama unavyofahamu siyo ugomvi mimi ni msisitizo tu hapa nataka kufanya. Mheshimiwa Silinde hatwendi pale kukuwekea daraja la magogo, pale tunakwenda kukuwekea daraja la uhakika. Kwa hiyo, kazi hii hapa tunavyozungumza imekamilika. Sasa hatua

inayofuata sasa ni kwenda kulijenga daraja yenyewe na ndicho tulichokiri hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie na Bunge lako Tukufu hii kwamba jambo hili sisi tutalisimamia kuhakikisha kwamba daraja lile linajengwa pale.

Na. 32

### **Upungufu wa Walimu wa Masomo ya Sayansi**

**MHE. SUSAN A. LYIMO (K.n.y. MHE. MHONGA S. RUHWANYA)** aliuliza:-

Shule za Msingi na za Sekondari za Mkoa wa Kigoma zina upungufu mkubwa wa walimu wa Sayansi na baadhi ya shule hazina kabisa walimu hao:-

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuupatia Mkoa wa Kigoma walimu wa kutosha wa Sayansi katika shule za msingi na Sekondari?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kukabiliana na upungufu wa walimu wakiwemo walimu wa masomo ya Sayansi kwa kuongeza udahili wa walimu

wanafunzi katika vyuo mbalimbali, kuhamasisha watu binafsi na Mashirika yasiyo ya Serikali kuanzisha Vyuo vya Walimu na kusisitiza kila Chuo Kikuu kuwa na Kitivo cha Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2012/2013, Mkoa wa Kigoma ulipangiwa walimu 666 wa shule za msingi walioandaliwa kufundisha masomo yote ikiwemo masomo ya sayansi na walimu wa sekondari 464 asilimia 11 wakiwa walimu wa masomo ya Sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kujenga mazingira mazuri ya kuongeza uhitimu wa walimu wa masomo ya Sayansi kwa kutoa kipaumbele kwenye Bodi ya Mikopo kwa walimu wa masomo ya Sayansi, kuwaajiri walimu wote wa masomo ya Sayansi na kuimarisha ufundishaji masomo ya Sayansi kwa vitendo.

Aidha, Halmashauri zitaendelea kusisitizwa kuwapanga walimu maeneo yenye upungufu na kutumia vizuri fedha za uhamisho kuweka uwiano sawa wa walimu hususan wa masomo ya Sayansi katika shule mbalimbali.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa huwezi kupata walimu wa Sayansi bila kuwa na maabara; na kwa kuwa hapa nchini kwetu kumekuwa na tatizo kubwa sana la maabara.

Je, Serikali inajipangaje kuhakikisha kwamba tunapata maabara?

(b) Kwa kuwa; sasa hivi shule zetu za Kata nyingi hazina maabara na vilevile tumeendelea kujenga shule hizo bila kuwa na maabara.

Je, ni kwa nini sasa Serikali isije na sera maalum ili kuwe ni msingi au muhimu sasa kwamba shule yoyote isijengwe bila kuwa na maabara ili tuweze kupata walimu wa kutosha wa masomo ya Sayansi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hili tatizo linalosemwa ni kweli tumekuwa nalo katika shule hizi ambazo tumezianzisha.

Lakini kama tumesikiliza taarifa ambazo zimekuwa zinatolewa na Serikali hapa mara kwa mara tumekuwa tunajitahidi kuhakikisha kwamba sasa wanafunzi wetu hasomi kwa nadharia tu wanasoma kwa vitendo pia. Tumeulizwa hapa maswali yote mawili ni kama vile yanafanana. Naomba niyajibu kama ifuatavyo:-

Kwamba kuna jitihada gani?

Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika mahali na tuliletewa hapa maabara ambazo ni *mobile* ninakumbuka zikaonyeshwa hapa na Halmashauri zetu zote zikaelekezwa kwamba zijielekeze katika kununua maabara hizo ambazo ni *mobile*.

Hilo la kwanza tumelifanya na wakisimama hapa Wabunge mbalimbali watasema kwamba hicho kimefanyika. Lakini katika MMES II tunayoizungumza sasa hivi tumezitaka Halmashauri zote zitupatie shule mbili ambazo tunazijenga zikamilike katika utimilifu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii tunavyozungumza sasa hivi inafanyika na Wabunge ni mashahidi kwamba hizo shule ziko wanaweza wakawa wametofautiana kuhusu wapi ijengwe na vitu vingine vya namna hiyo na kazi hiyo sasa hivi tunavyozungumza hapa inaendelea. Lakini wakati huo huo kwa jitihada hizo hizo tumezitaka shule zile ambazo zina maabara ambazo zimekamilika waendeleo kushirikiana na shule zile ambazo hazina hizo maabara ili waweze kusaidiwa katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho. Jambo hili linasemwa hapa la kwamba tuzuie sasa shule zisijengwe mpaka zitakapokuwa na shule ambazo zitakuwa na maabara. *Good talk*. Maamuzi haya yalikuwa ni maamuzi makubwa na mazito na ulimwengu ulitushangaa. Tumefika mahali tukaseme tungefanyaje. Wale Wacuba walipofika mahali wakasema nchi yetu tunataka watu wetu wajue kusoma na kuandika wala hawakuwa na shule hizi ambazo wanaziita *yeboyeyo* na *Voda Fasta*, walikuwa wanasoma chini ya mti.

Lakini *seriously speaking* walikwenda wakafika mahali wakafanya maamuzi makubwa katika nchi yao, wakaamua kwamba wawasomeshe watoto wakati huo

huo waendeleo kujenga maabara vyote kwa pamoja viende sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi umeonyesha kwamba tungekaa tusifanye maamuzi yale tuliyofanya tungechukua miaka mpaka mwaka 2015 ndio leo mngepata haya matokeo tunayoyaona hapa. Kupanga ni kuchagua, tulichochoagua ni kusema tuanze shule hizi wakati huo huo tunaendelea kutafuta walimu wakati huo tunazijengea maabara vyote viende kwa pamoja na sambamba maamuzi haya yalikuwa ni maamuzi ya msingi kama Taifa kwa ajili ya kuleta ufanisi katika eneo la elimu.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa hili tatizo la upungufu wa walimu liko sana katika Wilaya ya Kondoa. Kwa kiwango kikubwa hata cha kupelekea matokeo ya mtihani wa darasa la saba mwaka 2012 Wilaya ya Kondoa kushika nafasi ya mwisho Kitaifa.

Je, Serikali inawaambia nini wazazi na wananchi pamoja na wanafunzi wa Wilaya ya Kondoa ambao nina hakika saa hizi wanasikiliza? Serikali inasema nini kuhusu upungufu huu mkubwa? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Mwanri majibu, ni kweli kabisa Kondoa inahitaji msaada maalum.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tumekwenda kwa Mheshimiwa Mhita

tumekwenda pale kukagua shule nyingi sana mabati mengi yalipigwa pale yametokana na Mbunge huyu. Mbunge huyu ame-*contribute* sana.

Nataka niseme kabisa *it is our judgement* kama Wizara iliyoko chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Mheshimiwa Zabein Mhita amefanya kazi kubwa sana katika jimbo lake na katika Wilaya yake. Hiyo hatuna wasiwasi kabisa na jambo hilo.

Sasa jambo analolizungumza hapa na ambalo ndilo lililoulizwa na Mheshimiwa Ruhwanya. Moja ambalo tumefanya ni habari ya udahili kuhakikisha kwamba unaongeza idadi ya walimu wanafunzi wanakwenda kujifunza kule unaongeza idadi yao na hicho tumefanya Mheshimiwa Majaliwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Hawa Ghasia wamekuwa wanajibu hapa kwamba tumeongeza idadi ya wale wanaokwenda kusomea.

Tumesema kila chuo hata kama hakifanyi kazi ile ya elimu kianzisho pale kitivo ambacho kitashughulika na mambo ya kupata walimu. Tumesema wakati huo huo kwamba mwalimu yoyote atakayejiunga katika ualimu akasoma masomo ya sayansi hakuna cha kusema Utumishi, akitoka ni *automatical* anakwenda moja kwa moja kufundisha anaajiriwa. Tumesema ile Bodi ya Mikopo itoe kipaumbele kwa wanafunzi wa namna hiyo. Yako mambo mengi ambayo tunazungumza hapa. Sasa anauliza kwamba tunasema nini kuhusu eneo lake?

Tatizo ambalo tumeliona na ambalo ningewaomba Wabunge watusikilize vizuri kwa sababu litawasaidia wakati

mwingine mgawanyo wa walimu tatizo liko palepale Makao Makuu ya Halmashauri. Hii ya Kigoma iliyoulizwa hapa wana walimu 252, wana shule 48 kwa sababu mfano ninaoutoa unafanana na ule wa shule ya Mheshimiwa Ruhwanya, wana shule 42 ambazo hazina walimu.

Lakini ukichukua walimu 252 gawanya kwa mbili maana yake ni walimu 126 maana yake kila shule ingeweza ikapata walimu wawili. Lakini tunazo shule 48 pale Kigoma hazina walimu. Tumetenga fedha ndicho tunachokisema na hilo ndilo jimbo la Mheshimiwa Mhita. Ziko Shilingi bilioni 18 zimetengwa kwa ajili ya kupeleka kwenye Halmashauri.

Tunataka fedha hizo zitumike kwa ajili ya kuwa na uwiano mzuri watawanywe hao walimu waende wote katika Halmashauri wasikae Makao Makuu ya Wilaya pale na Halmashauri ya Kigoma ambayo iliuliziwa ambayo nilikuwa nimejiandaa hapa tumewapelekea Shilingi bilioni 1.8. Nitakwenda kuangalia kwamba Kondoa tumewatengea shilingi ngapi muende mkagawanye hawa walimu waende mpaka huko kwenye hizo Halmashauri.

Baada ya hapo tuje hapa tutakuja kugawa hawa walimu kama mnavyotaka ili tuweze kuenea, kitu kinachozungumzwa hapa ni walimu wa masomo ya Sayansi.



Na. 33

**Kuongeza Bajeti ya Vyu vya  
Maendeleo ya Wananchi**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Serikali huwa inatenga fedha za kuendeshea Vyu vya Maendeleo ya Wananchi nchini lakini imekuwa ikipeleka fedha kidogo sana na kuvifanya vyuo hivyo kujiendesha kwa taabu, na vile vyuo vinavyoonekana vinafanya vizuri huwa vinatafuta vyanzo vyao wenyewe vya mapato; na kwa sababu inasemekana kuwa Bajeti ya Mwaka 2013/2014 imeongezeka:-

Je, Serikali itakuwa tayari kuongeza Bajeti ya Vyu vya Maendeleo ya Wananchi kikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi *Singida FDC*?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Bajeti ya mwaka 2013/2014 Serikali imeongeza Bajeti ya Vyu vya Maendeleo ya Wananchi kutoka shilingi milioni 347,956 mwaka 2012/2013 hadi shilingi bilioni 1,555. Fedha hizo zitatumika kuendesha vyuo vyote vya Maendeleo ya Wananchi kikiwemo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yetu kuwa bajeti ya Vyuho vya Maendeleo ya Wananchi itaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Hii ni kutokana na azma ya Serikali ya kuwa na Chuo cha Ufundi Stadi kwa kila Wilaya. Hadi sasa Vyuho vya Maendeleo ya Wananchi 25 vimeanza kutoa mafunzo kwa mfumo wa Ufundi Stadi (VETA) sanjari na mafunzo yanayotolewa katika Vyuho hivi kwa kuzingatia madhumuni ya kuanzishwa kwake.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa Vyuho vya Maendeleo vinafanya kazi nzuri sana kuandaa vijana wetu kujitegemea ama kupata ajira katika taasisi mbalimbali za Serikali. Na kwa kuwa vyuho hivi vimekuwa vikipata fedha ndogo sana mfano Chuo cha Maendeleo ya Singida.

Mwaka 2010 hawakutengewa hata senti tano kwa ajili ya kununua vifaa vya kufundishia pamoja na mwaka 2011. Mwaka jana vikatengewa Sh. 300,000/= tu.

Je, Mheshimiwa Waziri hivi jirani yako Mheshimiwa Waziri wa Fedha pale hawezi kukusaidia fedha ili uweze kuvinusuru vyuho hivi ambavyo vinafanya kazi kwa mazingira magumu?

La pili, kwa kuwa vyuho hivi hata fedha za chakula ambavyo hutolewa kwa tenda wakandarasi hawa wanafanya kazi kwa madeni kwa miezi mingi hata mwaka hata kufika mahali wanakata tamaa wanasitisha huduma.

Je, Serikali sasa itakuwa tayari kupeleka fedha hizi chuoni moja kwa moja ili vyuo hivi vijitegemee vyenyewe viwe vinanunua vyakula wakati wa msimu wa vyakula kwa bei nafuu kuliko ilivyo sasa?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kumekuwa na ufinyu wa Bajeti ndiyo maana fedha zimekuwa hazitoki.

Lakini kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba mwaka huu Serikali imetoa shilingi bilioni 1.555 kwa ajili ya kuendeshea vyuo hivi tofauti na huko nyuma. Hapo hapo ningependa nijibu swali lake la pili kuhusu fedha za chakula. Fedha hizi zitatumika pamoja na mambo mengine kwa kununulia vyakula na vyakula hivyo vinanunuliwa moja kwa moja kwa wazabuni ambao wamewatafuta wao wenyewe kule kwenye vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke kwamba vyuo vingine vina miradi kwa hiyo Serikali imeruhusu fedha zile zitumike kwa hivi Vyuo vya Wananchi kwa kununulia vyakula. Ahsante sana.

Na. 34

### **Upatikanaji wa Leseni za Udereva**

**MHE. AHMED JUMA NGWALI** aliuliza:-

Serikali inafahamu kuwa watu wengi wameomba leseni za udereva kwa muda mrefu bila mafanikio na

wengine wamekata tamaa kwa sababu Serikali haijaeleza wazi sababu za kuchelewa huko kwa upatikanaji wa leseni kwa waombaji:-

Je, Serikali inasema nini juu ya tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianza mchakato wa utoaji leseni mpya za udereva kwa mfumo wa kielektroniki kuanza tarehe 1 Oktoba, 2010. Hadi kufikia Agosti 20, 2013, jumla ya leseni za udereva 827,284 tayari zilikuwa zimekwishatolewa. Zoezi la utoaji wa leseni za udereva linafanywa kwa ushirikiano baina ya Jeshi la Polisi Tanzania na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Jukumu la Jeshi la Polisi ni kusaili madereva waliomaliza mafunzo katika vyuo vinavyotambulika na kuwafanyia majaribio ya udereva (*Driving License Test*) na wale wanaofaulu hupatiwa madaraja ya leseni zinazostahili.

Aidha, jukumu la Mamlaka ya Mapato Tanzania ni kukusanya Ada za Leseni na kutoa leseni kwa madereva. Majukumu yote haya hufanywa kwa njia ya kielektroniki baina ya Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu wa sasa, hakuna bakaa ya leseni ambazo hazijatolewa au zinazosubiri kutolewa isipokuwa zile ambazo zipo katika hatua ya kutolewa. Madereva wengi wameshindwa kupata leseni mpaka sasa ni wale ambao pamoja na masharti mengine hawajapitia Vyuvo vya Udereva ambavyo vinatambulika kisheria.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja tu la nyongeza, kama ifuatavyo.

Kwa kuwa leseni za Tanzania hazitumiki Kimataifa. Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya leseni hizo kutumika Kimataifa hasa ukitilia maanani uwepo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao unaendelea kuimarika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa sasa leseni zetu hazitumiki Kimataifa lakini hilo tunalichukua tutali-*consider* kwa sababu sasa hivi tumo katika *Regional Intergration* na ni muhimu sana kupata leseni ambazo *at least* zitaanza kutumika katika ukanda huu wa Afrika Mashariki. Kwa hivyo wakati utakapofika tutali-*consider* hilo kama kawaida. Ahsante sana.

Na. 35

### **Hati ya Kusafiria Nje Kwa Askari Polisi**

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA** aliuliza:-

Hati ya Kusafiria Nje (*Passport*) ni haki ya kila raia wa Tanzania wakiwemo na Askari Polisi lakini imekuwa vigumu sana kwa Askari Polisi kupata hati hizo:-

Je, kwa nini imekuwa vigumu kwa Polisi wa K Tanzania kukubaliwa kuwa na hati ya kusafiri nje?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mnyaa kwamba Hati ya Kusafiria ni haki ya kila raia wakiwemo Askari Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali haiwanyimi Askari Polisi kupata Hati za Kusafiria bali hutakiwa kupata Hati hizo kwa kufuata utaratibu maalum. Hatua mojawapo ya taratibu hizo ni kuwa na barua toka kwa Mwajiri wake inayomruhusu kusafiri nje ya nchi kama wanavyofanya watumishi wote wa Serikali na watu wote walioajiriwa katika Sekta mbalimbali. Utaratibu huu umewekwa ili kudhibiti mienendo ya watumishi na kulinda maslahi ya Mwajiri.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri masuala mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwamba anakubaliana na

mimi kwamba kupata *passport* ni haki ya Askari wowote kama raia wengine.

Lakini kwa kuwa wanaonyimwa hizi *passport* ni miongoni mwa hao hao askari. Na kwa kuwa hili ni Jeshi la Polisi na amri za Kijeshi zinatumiwa. Ebu Mheshimiwa Waziri uliambie Bunge hili pale mwajiri atakapokataa hatua gani zichukuliwe au hatua gani huyu Askari ambaye ameomba *passport* na amefuata taratibu zote na mwajiri amekataa nini kifanyike unatoa ushauri gani kwa Askari hawa. La kwanza.

Lakini la pili, kwa kuwa haki hii ni ya Kikatiba ambapo anapaswa mtu aipate *passport* aende anapotaka isipokuwa pale ambapo avunji sheria.

Je, utaratibu gani unapofanya ikiwa haki hii anakoseshwa mtu huyu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi linaongozwa na *Police General Order (PGO)*. Utaratibu wa kukata rufaa na kulalamika inapokuwa hawatendewi haki Askari wanaufahamu na mamlaka ya mwisho ni ya Waziri. Hivyo wote wataendelea kufuata utaratibu huo kwa mujibu wa taratibu hizo za Kijeshi.

Na. 36

**Mgogoro wa Ardhi Baina ya Kikosi cha  
Jeshi 601 KJ Na. 663 Na Wananchi**

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA** aliuliza:-

Mgogoro wa ardhi kati ya Vikosi vya Jeshi 601 KJ na 603 KJ na Wananchi wa maeneo ya Mlima Nyangunguruna na maeneo mbalimbali ya Kata za Ilemela ni wa muda mrefu na haujapatiwa ufumbuzi licha ya Serikali kuahidi kuumaliza mgogoro huo ilipojibu Swali Na. 179 Julai, 2011 na kwa sababu Waziri wa wakati huo hakufanya ziara maeneo hayo kama alivyokuwa ameahidi na sasa hali ya Wananchi wa eneo hilo inazidi kuwa mbaya kutokana na kuzuiliwa kuendeleza makazi yao:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuondoa vifaa vya kivita katika makazi hayo ya Wananchi na kuwaruhusu waendeleze makazi yao?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kuendelea kuviacha vifaa vya Kijeshi kwenye maeneo hayo kunahatarisha maisha ya Wananchi na ni kinyume cha haki za Binadamu?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mbunge wa Ilemela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali haina mpango wa kuondoa vifaa vya Kijeshi katika Kata ya Ilemela kwa sababu vifaa hivyo vinatumika katika kulinda Uwanja wa Ndege na Jiji la Mwanza. Hata hivyo, Wizara yangu inao mpango wa kuwalipa fidia wananchi ili



waondoke katika eneo hilo na kuwaacha Askari wa Jeshi waendeleo na shughuli zao za ulinzi.

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa suala hili limechukua muda mrefu. Si nia ya Wizara yangu kuchelewesha mpango wa kuwalipa fidia wananchi. Hali hii inatokana na ukosefu wa fedha.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni hatari kwa wananchi kuishi karibu na Wanajeshi. Wizara yangu inao mpango wa kupima eneo hilo na hatimaye kuwalipa fidia wanayostahiki ili wakaanzishe makazi yao katika maeneo yenye salama. Nitahakikisha kwamba suala hili linapatiwa ufumbuzi wa kudumu katika Bajeti ya mwaka 2014/2015.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Waziri amekiri kwamba suala hili ni la muda mrefu hasa kwa kuzingatia kwamba ni zaidi ya miaka 2 tangu wananchi hawa wa maeneo ya Ilemela, Nyangunguruna na maeneo mengine mbalimbali kuzuiliwa kuendeleza makazi yao jambo ambalo limewasababishia kuwarudisha nyuma kimaendeleo kwa kiasi kikubwa sana.

Lakini pia kwa kuwa Waziri amekiri kwamba kwa sasa wananchi hao wanaishi kwenye mazingira hatarishi hasa kwa kuzingatia kwamba vifaa vya kivita viko katikati ya makazi yao jambo ambalo linaweza kusababisha maafa kama yale ya Mbagala na Gongo la Mboto. Ningependa kumwuliza swali Waziri ni lini wananchi hawa watalipwa fidia hiyo?

Suala la pili, kwa kuwa sio wananchi walioingilia maeneo ya Jeshi bali ni Jeshi ndilo ambalo limeingilia maeneo ya wananchi. Wakati huo ambapo Serikali inatafuta muafaka wa suala hili viko vitendo vikubwa vya unyanyasaji vinapoendelea na baadhi ya Wanajeshi kujichukulia hatua mkononi na kimsingi ninakiuka misingi ya haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari kuongozana na mimi kwenda kukutana na wananchi hawa kuona adha kubwa wanayoipata kwa sasa ambayo inawafanya badala ya kufurahia kuwa Watanzania, wanavumilia kuwa Watanzania? Naomba majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye maelezo yangu katika swali la msingi, ni kwamba wananchi wanastahiki kulipwa fidia na hasa kwa wale wananchi ambao wanaishi kwenye maeneo hayo. Kama nilivyosema, Wizara yangu itafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba tunayapima maeneo hayo na hatimaye kuwalipa wananchi wanaostahiki na tutayafanya hayo katika bajeti ya mwaka 2014/2015.

Swali la pili, niko tayari kufuatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kuwaona wananchi na kuwasikiliza kero zao, na tunaweza tukafanya hilo baada ya kumaliza shughuli za Bunge hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Swali la nyongeza Mheshimiwa Buyogera.

**MHE.AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Bila kuathiri majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba nipate tamko la Serikali kulingana na matatizo yanayojitokeza kwenye Makambi ya Kijeshi. Kwa kuwa Kasulu tuna Kambi iliyoanzishwa la JKT na bado miundombinu pale haijawa mizuri: Je, ili kuondoa tatizo hili la mipaka lisijitokeze baadaye, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni wakati muafaka sasa kuandaa fedha na kwenda kupima ile mipaka mapema ili kuweka uzio katika eneo la Jeshi la JKT pale Jimboni kwangu Kasulu?

**NAIBU SPIKA:** Ni Kambi ya Bulombora au?

**MHE.AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, JKT pale Mutabira ilipokuwa Kambi ya Wakambizi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Majibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa – Mheshimiwa Vuai Nahodha.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Wizara yangu inayo dhima na wajibu wa kupima maeneo yote yenye mgogoro kati ya Jeshi la wananchi au kati ya JKT na wananchi kwa upande mwingine. Kwa maana hiyo, basi Wizara yangu itatekeleza jukumu hilo wakati wowote itakapopatiwa fedha. Nimesema tatizo kubwa linalotukabili ni ukosefu wa fedha. Lakini tutaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha juu ya jambo hili na pale ambapo fedha hizi zitatolewa, basi Wizara yangu haitasita kutekeleza jukumu hilo haraka iwezekanavyo.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Uchukuzi, Swali la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu.

Na. 37

**Kupigwa Marufuku Abiria Kujisaidia Pembezoni  
mwa Barabara katika Safari Ndefu**

**MHE. JUMA SURURU JUMA** aliuliza:-

Serikali ilipiga marufuku magari ya abiria kusimama njiani ili abiria wajisaidie pembezoni mwa barabara kwa lengo la kulinda mazingira, afya za watu na kudumisha heshima na utu wa abiria.

(a) Toka zoezi hilo lianze, tumefanikiwa kwa kiwango gani?

(b) Je, Serikali imechangia nini katika kuweka mazingira bora ya kujisaidia kwa wasafiri wawapo safarini?

(c) Kwa yale maeneo ambayo yapo mbali na sehemu ambazo huduma hizo hupatikana, abiria wanahitaji huduma hiyo wakiwa safarini. Je, Serikali inasema nini katika mazingira kama haya?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a), (b) na (c).

(a) Utekelezaji wa agizo la kuzuia abiria wa mabasi ya masafa marefu kujisitiri vichakani ulianza rasmi tarehe 01 Septemba, 2012. Vituo vya kujisitiri vinavyoweza kutumiwa na abiria vilitangazwa na tayari wenye mabasi wameelekezwa kutumia vituo hivyo. Aidha, vituo vingi ni vya kulipia kati ya Sh.100/= hadi Sh. 200/=. Katika ukaguzi uliofanyika mwezi Novemba, 2012 ilibainika kuwa zaidi ya 90% ya magari yanayotumia barabara kuu yametii agizo hilo. Elimu inaendelea kutolewa ili kuhakikisha utekelezaji unafanyika kwa asilimia mia moja.

(b) Serikali kupitia *SUMATRA* imechangia kwa kuandaa mchoro wa jengo la huduma kwa wasafiri ambalo wawekezaji binafsi au Halmashauri za Wilaya wanaweza kuwekeza hususan katika maeneo ambayo hayana huduma hiyo.

(c) Serikali kupitia *SUMATRA* imewaagiza wamiliki kuweka utaratibu wa kuwatangazia abiria mara kwa mara maeneo ambako huduma hiyo inapatikana ili watoe taarifa mapema iwapo wanahitaji huduma hiyo na hivyo *bus* kusimamia eneo lenye huduma ya kujisitiri.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nilitaka kujua suala moja tu. Ni vituo vingapi vinavyofanya kazi kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma na viko maeneo gani?

**NAIBU SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi, Mheshimiwa Dkt. Tizeba – Naibu Waziri wa Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam viko vituo vingi vya kujisitiri. Kwa kuanzia ni kwamba, kila stendi ya *bus* katika Halmashauri zote zinazopitiwa na barabara hii kuu ya Dodoma - Dar es Salaam, kuna maeneo ya kujisitiri, lakini sambamba na maeneo ya stendi, vituo vyote vya mafuta vilivyoko katika barabara hii kuanzia Dar es Salaam mpaka Dodoma wameelekezwa kufungua vyoo vyao ili abiria wanapohitaji huduma hiyo waweze kupata huduma hiyo na wenye vituo wanakubali na kutii ombi hilo.

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo ni swali la Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mbunge wa Viti Maalum.

Na.38

### **Idadi ya Wahanga wa Ajali za kwenye Maji**

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR** aliuliza:-

Katika ajali nyingi zinazohusisha usafiri wa vyombo vya majini, huwa ni vigumu kupata idadi halisi ya watu wanaoathirika na ajali hizo. Je, Serikali ina kauli gani kuhusu jambo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdallah Amour Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali anayoiongelea Mheshimiwa Mbunge siyo ya sasa ila ni ya siku za nyuma ambapo ajali za kuzama meli na vyombo vingine vya majini vilivyosajiliwa ziliambatana na changamoto ya kufahamu idadi halisi ya watu au abiria waliokuwa katika vyombo hivyo kabla ya ajali husika kutokea. Mwaka 2011 Serikali ilitunga kanuni zinazoelekeza namna ya kutayarisha na kuweka kumbukumbu za watu wanaopanda kwenye vyombo hivyo vya majini, *merchant shipping (Counting and Registration of Persons on Board Passenger Ships) Regulations*.

Kanuni hizo zinawaagiza wamiliki wa vyombo hivyo kutayarisha kumbukumbu na taarifa za abiria kabla ya kuanza safari. Aidha, mmiliki wa Bandari au Mwalo ambao chombo kinaondokea, anawajibika kuhakiki taarifa za abiria kabla ya chombo husika kuondoka bandarini au kwenye Mwalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa rai kwa wananchi wanaotumia vyombo vya usafiri majini kwamba wahakikishe wanafuata utaratibu wa kukata tiketi kwenye ofisi halali za wamiliki wa vyombo na waepukane na tiketi za ulanguzi. Utaratibu huo utawasaidia kuorodheshwa kwenye orodha ya abiria (*passengers list*) waliobebwa na vyombo husika, hivyo, kuwa rahisi kwao kutambulika wakati wowote ule.

Aidha, Serikali imevielekeza vyombo husika na usimamizi wa usafiri wa majini kutoa elimu kwa umma ili kuhakikisha ujumbe huu unawafikia wananchi na unazingatiwa na wadau wote wanaohusika na usafiri wa

majini. Hatua kali zinachukuliwa kwa wale wote wanaobainika kukiuka Sheria, Kanuni na taratibu zinazosimamia uorodheshwaji na utunzaji wa kumbukumbu za abiria.

**NAIBU SPIKA:** Majibu ya swali hilo fupi, Mheshimiwa Dkt. Tizeba – Naibu Waziri wa Uchukuzi.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba kuna Kanuni na Sheria, lakini tatizo kubwa liko katika usimamizi, ndiyo maana ajali hizo zinatokea kila siku na kwa makosa yale yale. Je, utawahakikishia vipi wananchi kuhusiana na usimamizi wa Sheria hizi?

Swali la pili, ni kwa nini hatujaona kuchukuliwa hatua kwa wale wanaoshindwa kusimamia Sheria hizi za usalama wa wananchi? Mpaka lini mtaanza kuwachukulia hatua? Mpaka sasa bado mnawalinda. Asante sana.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Uchukuzi - Mheshimiwa Dkt. Tizeba.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usimamizi ni la kibinadamu zaidi na ndiyo maana kila siku hata kwenye Sheria za namna gani makosa ya namna hiyo huendelea kutokea.

Kwa hiyo, wajibu wa Serikali ni kuhakikisha kwamba watumishi na watendaji wanaokuwa katika Taasisi hizi za Usimamizi ni wenye maadili na wanaojali na kuheshimu kazi zao. Ni jambo lingine anapotokea mtendaji mmoja mmoja



anakiuka maelekezo na Kanuni za utendaji wa kazi na anapobainika mtu wa namna hii anachukuliwa hatua stahiki za kinidhamu.

(b) Siyo kweli kwamba wanaokiuka na kusababisha ajali za namna hii hawachukuliwi hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ajali zote kubwa ambazo zimetokea, wako watu ambao wamechukuliwa hatua, wengine wamepata vifungo, wengine kesi zao bado zinaendelea na watahukumiwa baada ya uchunguzi kufanyika na kubainika ni nani aliyehusika hasa na kusababisha ajali hiyo au kwa uzembe au kwasababu nyingine yoyote, kama uchunguzi utakavyokuwa umebaini.

**NAIBU SPIKA:** Tuelekee Zanzibar kwa swali la mwisho kabisa kwa siku ya leo.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya sababu zilizosababisha madhara yaongezeke na kuwa makubwa katika ajali zile zilizotokea Zanzibar, ni kushindwa kufika katika eneo la tukio haraka kutokana na ufinyu wa vyombo vya mawasiliano.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kueleza ni mkakati gani wa mawasiliano na hatua gani zimefikiwa ili kuweza kupata vifaa vya kisasa vya mawasiliano vitakavyoweza kubaini mwendo kasi, lakini pia vitavyotambua eneo la ajali kwa haraka na hatua za haraka zichukuliwe wakati ajali zinapotokea?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kufika kwenye kitukio inategemea na taarifa ya tukio lenyewe imetolewa saa ngapi? Wanaokuwa kwenye tukio lenyewe, wakichelewa kutoa taarifa kwenye maeneo ambayo yanajulikana, basi ni lazima *response time* itakuwa ndefu kwa sababu wale wanaopaswa ku-*react* wanakuwa hawana taarifa kwa haraka.

Tunacho kituo Dar es Salaam, kwa mfano, kwa usafiri wa baharini *MRCC* pale Kigamboni; wasafiri wote wa vyombo, Makapteni wameelekezwa kwamba likitiokea tukio wapige simu namna ya kuwafikia watu wa kituo cha *MRCC*. *MRCC* watakachofanya ni kuvitaarifu vyombo vingine vyenye kuweza kutoa msaada kwenye tukio kufika pale mara moja kutokea pande zote mbili yaani Zanzibar, Dar es Salaam, Tanga na kwingineko kutegemea na tukio hilo linatokea karibu na wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tuko katika hatua za mwisho za kuandaa Muswada wa Sheria ya kutafuta na kuokoa *Search and Reque Bill* ambayo tumekwishaahidi hapa Bungeni kwamba tunatarajia katika Bunge la mwezi Novemba tutaleta Muswada huo kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru, kipindi cha maswali kimekamilika. Sasa naomba nije na matangazo yafuatayo:-

Naomba kumtambulisha mgeni ambaye yuko katika ukumbi wa Bunge ni Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba - Mheshimiwa Ponsiano Nyami. Mheshimiwa Nyami alikuwa

Mbunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kati ya mwaka 1995 – 2010. Alikuwa akiwawakilisha wananchi wa kule Namanyere, Jimbo ambalo hivi sasa ni Majimbo mawili ambako Mzee Keissy anatoka. Karibu sana Mheshimiwa Ponsiano Nyami! Karibu sana Mjengoni!

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni madaktari 15 wa Afya ya Akili kutoka Chuo Kikuu Tanga. Wale pale, Waheshimiwa Wabunge! Wapo Hospitali ya Mirembe Dodoma kwa ajili ya mafunzo zaidi kwa vitendo juu ya Afya ya Akili na wameamua kututembelea Bungeni hapa. Eeh, Waheshimiwa! (*Kicheko*)

Vile vile wako wanafunzi 100 kutoka Shule ya Sekondari Nzuguni Dodoma. Wanafunzi wa Nzuguni, karibuni sana wanangu, mnapendeza kweli! Karibuni sana Shule ya Sekondari Nzuguni, Dodoma. Karibuni sana mjifunze kuhusu Bunge linavyofanya kazi, nyie pamoja na Walimu wenu, karibuni sana. Tuna wanafunzi 100 kutoka Shule ya Sekondari Kikuyu Dodoma. Nadhani watakuwa *basement* hawa.

Tuna wanafunzi 28 kutoka Shule ya Sekondari ya *Heritage* Kibaha. *Heritage*, Kibaha simameni. *Oooh*, mnapendeza kweli! Hongereni na karibuni sana wanafunzi wa *Heritage*, Kibaha kwa kuja kutembelea Bunge lenu. Tunawapongeza sana nyinyi pamoja na Walimu wenu, karibuni sana. Kuna Mwenyekiti wa NUWA Mkoa wa Kilimanjaro, Ndugu Mfutakamba pamoja na wana-NUWA wenzake kutoka Kilimanjaro ambao ni wageni wa

Mheshimiwa Mwanri. Karibuni sana Bungeni na tunawakaribisha Dodoma pia.

Matangazo mengine ni kutoka kwa Mheshimiwa Mgimwa - Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwamba leo saa 7.00 mchana wakutane ukumbi wa Msekwa 'C'.

Mheshimiwa Lembeli - Mwenyekiti wa Ardhi, Maliasili na Mazingira anawaomba Kamati hiyo wakutane saa 7.15 mchana *basement*.

Mheshimiwa Brig. Jen. Mstaafu Hassan Ngwilizi anaomba Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge wakutane saa 7.15 mchana ghorofa ya pili ukumbi Na. 219.

Mheshimiwa Ana Margareth Abdallah - Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, anaomba Kamati yake wakutane Ukumbi Na. 231ghorofa ya pili na katika kikao hicho ambacho Mheshimiwa Ana Abdallah anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kukutana, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wahudhurie kikao hicho. Kwa hiyo, ni Kamati mbili; Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ya Mheshimiwa Lowassa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mheshimiwa Ana Margareth Abdallah, zinaombwa kukutana Ukumbi Na. 231 saa 7.15 mchana.

Tangazo la jumla kutoka Ofisi ya Utawala, Bunge inawaomba Waheshimiwa Wabunge ambao hamjarejesha

fomu zinazohusu Bima ya Afya ya Wabunge mlizopewa mzijaze, mzirejeshe ili mchakacho uweze kuendelea.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji wa Mwaka 2013**

*(The National Irrigation Bill, 2013)*

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masauni. Kabla ya Mheshimiwa Masauni; Waheshimiwa Wabunge mnasimama simama, mnatuchanganya. Kama mnasimama kwa maana ya hoja; au kuna *issue* gani? Nafikiri ni Mheshimiwa Masauni, peke yake. Ahsante.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni Ibara ya 64(a).

Mheshimiwa Naibu Spika, leo asubuhi wakati wa maswali ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mbunge Haji Kai wa *CUF*, alisema kwamba Chama cha Mapinduzi kimemfukuza Ndugu Mansour kwa sababu ya msimamo wake wa kupingana na Sera za Chama cha Mapinduzi kwa maana ya *specifically* katika kupinga muundo wa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo ambayo yametolewa na Katibu Mwenezi wa CCM, hakuna

kipengele ambacho kinazungumza kwamba Ndugu Mansour alifukuzwa kwa sababu alisema anataka Serikali ya mkataba. Lakini pia Chama cha Mapinduzi ndiyo Chama pekee ambacho kilikuwa kimeweka utaratibu mzuri wa kuchukua maoni kuanzia ngazi ya matawi kwa wanachama wote, na maoni yale yalitoa fursa kwa wanachama wote wa CCM kutoa maoni yao kwa uhuru kabisa, na ndipo wanachama wengi wakaja na msimamo ambao ulikuwa unalinda Muungano wetu, lakini pia kutilia maanani umuhimu wa ku-*address* changamoto za Muungano zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Kai alithibitishie Bunge lako hili Tukufu kwamba ni wapi Chama cha Mapinduzi kilieleza kwamba Ndugu Mansour alifukuzwa kwa sababu ya kusema kwamba anataka Serikali ya mkataba?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, ulikuwa unampa taarifa au ni nini, Mheshimiwa Masauni? Mheshimiwa Masauni, nia yako ilikuwa ni kumpa taarifa ya hilo ili aweze kuipokea? Au ni nini?

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, athibitishie!

**NAIBU SPIKA:** Kwani Mheshimiwa Kai ulisema nini? Hebu tukumbushe kwa dakika chache sana.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikumbushe? Kwanza kwa kujibu hilo, Mheshimiwa Mansour ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati ya Maridhiano, na Kamati ya Maridhiano msimamo wao ni kuwa na Serikali yenye mamlaka kamili ya Zanzibar. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Naona jambo hili lisituchukulie muda. Tunaendelea na uchangiaji wa hoja zilizopo leo. Maana naona Mheshimiwa Haji Kai anatuletea mambo ambayo ukisema habari ya Zanzibar kuwa na mamlaka kamili, utaamsha mashetani hapa; hoja ya umwagiliaji itaondoka yaanze mambo mengine. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Mnyaa atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuanza kuchangia mchana huu wa leo katika hoja iliyopo Mezani ambayo ni Muswada wa Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwanza nitoe pole kwa Serikali, baada ya miaka 50 imetoka usingizini.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane na tumsikilize mchangiaji.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya miaka 50 takribani Serikali imetoka usingizini na kuleta Muswada huu ambao maudhui yake ni muhimu sana kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitachangia katika maeneo mawili. Eneo la kwanza la ujumla linahusiana na kilimo na umwagiliaji, lakini eneo la pili tutakwenda kwenye vifungu vyenyewe vya sheria hii, kwamba katika lile eneo la kwanza ambalo linahusiana na kilimo na umwagiliaji, baada ya takribani miaka mitatu mpaka minne kuanzia pale ilipokuwepo Sera ya Taifa ya Umwagiliaji, leo Muswada umewasilishwa. Hii ni kusema kwamba ni bora fedheha kuliko lawama ingawaje katika hali ya utaratibu wanasema bora lawama kuliko fedheha. Siyo haba! Muswada umefika na tutauchangia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sera hii ya Taifa ya Umwagiliaji ambayo leo chimbuko lake imefanikisha kupatikana Muswada huu, kilimo cha umwagiliaji ni muhimu sana kwa Taifa hili na ndiyo kilimo pekee ambacho kitalihakikishia Taifa hili kuwa na mazao ya chakula pamoja na mazao ya biashara kwa mwaka mzima ambapo tunahitaji sana chakula pamoja na mazao ya biashara. Lakini vilevile kutokana na tabianchi, kilimo cha umwagiliaji ndiyo kilimo pekee ambacho kitasaidia uwepo wa chakula ambapo uzalishaji unakadiriwa kuongezeka kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na mipango mbalimbali. Kuanzia mwaka 2000/2001 hadi mwaka 2004/2005 kumekuwepo na *scheme* kama 75 za umwagiliaji. Ni kweli ongezeko kufuatia umwagiliaji huo uliokuwepo, kwa mfano, kama kilimo cha Mpunga kiliweza kuongezeka na kikatoka tani 767,000 mpaka kufikia angalau tani 900,000.



Kwa hiyo, hii ni dhahiri kwamba kilimo cha umwagiliaji kinapotekenezwa katika njia ya ufanisi ulio bora na utalaam ukapatikana, basi uzalishaji unaongezeka kwa kiasi kikubwa. Eneo la hekta moja ambazo katika hali ya kawaida inaweza kutoa tani tatu, katika kilimo hiki cha sayansi cha umwagiliaji, eneo hilo hilo linaweza kutoa tani nane mpaka tani tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Muswada huu pamoja na kuchelewa, umekuja wakati muafaka na tunategemea endapo utekelezaji wake utasimamiwa ipasavyo kama ilivyoelezwa katika vifungu vya Muswada huu, huenda matarajio na neema ya nchi hii ikapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sera ya Taifa ya Umwagiliaji inaonekana zimetajwa hekta milioni 29.4 kwamba ndiyo hekta zinazofaa kwa umwagiliaji, zikachambuliwa kwamba kuna hekta milioni 2.3 kwamba hizo za umwagiliaji mkubwa (umwagiliaji bora), kuna hekta milioni 4.8 kwa umwagiliaji wa kati na hekta zilizobakia milioni 22.3 kwa umwagiliaji mdogo mdogo. Inatajwa kwamba tuna hekta milioni 44 za kilimo kwa ujumla.

Sasa zinapotajwa namna hii katika masikio ya Watanzania, inakuja ile picha kwamba Tanzania tuna eneo kubwa sana la kilimo la kutosha kabisa. Pengine upande mmoja siyo sahihi, kwa sababu tukitizama sensa iliyopita takribani Watanzania sasa tupo milioni 43; sasa ukitazama zile hekta zinazotajwa milioni 44 kwa ujumla, lakini za umwagiliaji ni milioni 29.4, miaka kumi ijayo Watanzania pengine tutafikia milioni 50. Hilo ni tatizo kubwa linajionesha

kwamba kumbe tutakuwa na eneo dogo wastani wa hekta moja kwa Mtanzania; itakuwa imeshapita, pengine ule wastani wa hekta moja kwa Mtanzania mmoja, itakuwa imeshapita kwa lile eneo la kilimo. Tutakuja kugundua kwamba kumbe tuna eneo dogo sana au chache sana kwa ajili ya kilimo hasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunachofikiria *behind* ya Muswada huu, inaonekana kuna wawekezaji ambao tuna tamaa kwamba waje wawekeze katika nchi hii. Tunasahau kwamba katika Muswada huu ni vyema kama ni wawekezaji, basi wawe wa kizalendo, ndio wa kuwapa nguvu zaidi. Haya maeneo kuchukuliwa makubwa kwa idadi ya ongezeko la watu ni kitu ambacho tunakwenda pengine kuongeza migogoro kwa kipindi kijacho tu cha miaka kumi ikiwa hatutakuwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ipo migogoro ya wafugaji ambao utatuzi wake bado haujafikia mahali vilivyo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kutoa tahadhari au wachangiaji wengine kwamba tunapotaja mamilioni ya hekta, lakini ukweli wa mambo pengine miaka michache ijayo tutakuwa na ardhi ndogo sana ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hizo hekta milioni 29.4 za umwagiliaji ambazo tayari zimeshatumika zinatamkwa kwamba ni milioni 1.5; maana yake tulichofanya hivi sasa ni asilimia tano tu ya umwagiliaji. Ndiyo kusema kwamba pengine kulikuwa na sababu nyingi, pengine kulikuwa hakuna huu Muswada, lakini baada ya kupitishwa Muswada huu, upo uwezekano ongezeko la umwagiliaji likawa kubwa sana na nchi hii ikafarijika kwa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ilikuwa ni sehemu ya kwanza. Lakini sehemu ya pili ya Muswada huu, ukiutazama Muswada huu na kama tukiuchambua vilivyo, una makosa makubwa sana kuanzia ile sehemu ya kwanza ambayo ni *preliminary provision*. Sehemu ya kwanza kabisa tayari huu Muswada una makosa makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe masikitiko yangu makubwa kwamba Muswada huu umepitiwa na Kamati inayohusika ikiongozwa na Mwenyekiti mahiri, msomi ambaye namstahi, namheshimu sana. Lakini pia Muswada huu umepitiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani, Muswada huu tayari umechangiwa na baadhi ya Wabunge wengi, lakini makosa yaliyomo mimi naweza kuita ni *fatal problems*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama matumizi ya Muswada huu, kuna Wizara mbili; Wizara inayohusiana na kilimo na Wizara inayohusiana na mambo ya maji, ndiyo wahusika wakubwa wa Muswada huu. Kwa bahati mbaya sehemu ya kwanza ya *short title and commencement*, Muswada huu haujaeleza chochote, unatumika upande gani wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Muswada huu haujaeleza chochote: Je, unatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar au Jamhuri nzima? Maudhui yake unasema: "*The National Irrigation Act*" au kwa Kiswahili unasema: ni "Muswada wa Taifa wa Umwagiliaji."

Sasa tunaposema Taifa, sisi wengine, wengi wetu tunavyoelewa, unaposema Taifa, unazungumzia Taifa la Tanzania. Ukizungumza Tanzania kwa Katiba tuliyonayo ya Jamhuri, unazungumza Zanzibar na Tanzania Bara. Sasa

hata kabla ya Katiba mpya kuja, ikiwa itakuwa Serikali moja, mbili au tatu, tayari dhamira ambayo siku zote tunasema ile *good will* waliyoifanya Mwalimu Julius na Mzee Karume kila siku inapotea, ndiyo hii ambayo inaoneshwa katika Muswada huu. Ile *good will* ipo wapi? Muswada huu hauelezi chochote!

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo siyo Wizara ya Muungano. Kwa hiyo, Wizara ya Maji siyo Wizara ya Muungano. Muswada hausemi chochote! Tuelewe vipi? Sasa hili ni jambo zito ambalo tunashindwa kuelewa, Kamati iliyopitia Muswada huu na Kambi Rasmi ya Upinzani jamani hamkuona kwamba kuna Wizara ya Kilimo Zanzibar, na Kuna Wizara ya Kilimo hapa? Au ndiyo ile tunayothibitisha siku zote kwamba inatumiwa jina la Tanzania Bara iliyojificha katika koti la Muungano? Ndiyo hii! Kwa sababu unatunga Muswada huu utumike wapi kama haujaelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezoea Bunge hili Miswada yote ya Sheria pale kwenye *preliminary provision* inaeleza Muswada huu au sheria hii itatumika Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara au itatumika upande mmoja tu wa Jamhuri ya Muungano. Hicho ni kitu cha kawaida tumekizoea.

Leo Muswada huu umepitia Kamati zote, umepitia *process* zote, mpaka umefika, unawasilishwa Bungeni hauelezi chochote na tumebana kimya. Nini maana yake? Maana yake tunajivalisha madaraka ambayo siyo yetu, kukimeza kile kizanzibar kilichokuwa kidogo! Ndiyo maana yake? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kawaida mtu kuleta *schedule of amendment* akiona jambo kama hili. Lakini vilevile tuna uzoefu, *schedule of amendment*, wale wanasheria wa Bunge wanatusikia, tayari hili ni matatizo yaliyo wazi; ukileta *schedule of amendment* inategemea vilevile na upande mwingine wa *majority* vipi? Utakubali au utakataa?

Kwa hiyo, naweza kuleta *schedule of amendment*, lakini kama upande wa *majority* utakataa, ndiyo inakuwa kazi bure. Kwa hiyo, niseme tu kwamba huyo Waziri mhusika wa Muswada huu atupatie *schedule of amendment* ya jambo hili ili isiweze kupingwa. Vinginevyo nina sababu za kutosha za kulishawishi Bunge hili wakatae Muswada huu. Kwa sababu ikiwa utapita, tukaukubali ina maana na sisi Wabunge tunahusika katika kuivunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya (3) ambayo inazungumza...

*(Hapa kengele ya ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyaa, ni kengele ya pili. Nakushukuru sana. Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kusema kwa kifupi tu. Naona mambo mengi wenzangu wameyazungumza sana.

Mheshimiwa Spika, kama wenzangu walivyosema, ni muda mrefu tangu hii nchi imepata uhuru. Tuna miaka 50 sasa ya uhuru wetu. Moja ya maandiko ya zamani ya Marehemu Mahatma Ghandhi aliwahi kuzungumzia, anaita *seven deadly sin*. Anasema *wealthy without work*, yaani watu wanataka watajirike pasipo kufanya kazi. Nazitaja tatu tu. Mojawapo inasema *commerce without morality*, na anasema, *politics without principle*. Nimezitaja hizo tatu ambazo ninataka nizizungumzie.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandiko yake haya ya kizamani anajaribu kutukumbusha kwamba hivi vitu vyote visipofuatwa katika maisha ya mwanadamu, jamii huwa inakuwa kwenye *chaos*.

Wiki tatu zilizopita Jimboni kwangu nilibahatika kuwa na *dinner* au niliwaalika Waisrael wawili ambao tulikuwa tunaongea, wanafanya kilimo cha umwagiliaji. Walitoa maneno ambayo mimi yaliniumiza kidogo. Walisema kama wao wangepewa nchi ya Tanzania, wangeiambia dunia iache kuzalisha chakula, ifanye mambo mengine, wao wangeilisha dunia. Walisema, kwa ardhi tuliyonayo, hali ya hewa tuliyonayo pamoja na *water bodies*, mito, pamoja na maziwa tuliyonayo yanaweza kabisa kuilisha dunia na tukaifanya dunia ifanye mambo mengine, Tanzania tukawa tunalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo, pamoja kwamba na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo, tumekuja na huu Muswada, ambao mara nyingi tumeweka fedha katika Bunge letu. Mimi nilijaribu kuungana kidogo na Mheshimiwa Kafulila, jana alizungumza hapa kwamba siamini kama

*home work* ya kutosha imefanyika. Inawezekana tunajaribu kutoa majibu ambayo hayaulizwi. Inawezekana tunajaribu kutoa jibu ambalo kimsingi haliulizwi. Nini tatizo la rasilimali zote tulizonazo? Nilijaribu kufikiri jinsi ambavyo nchi ya Israel ilivyo ndogo na jinsi ambavyo wanafanya kazi na wao wanaweza waka-*export* matunda, nyanya wakati sisi tuna miinuko mizuri ambayo tunaweza tukalima mazao mazuri sana, tuna mabonde mazuri kwenye *Rift Valley* ambako tunaweza tukazalisha mpunga, tuna maeneo mazuri sana ambayo kila aina ya vitu vinavyoweza kuzalishwa katika nchi hii, vinawezekana!

Sasa nikawa najjuliza kwamba: Je, tatizo ni Sheria hii au tatizo ni mipango mibovu tuliyonayo? Nilipojaribu kuwadadisi Waisrael hawa walisema kinachotusumbua kwenye nchi yetu ni *mind set*. Sasa inawezekana tumeleta Sheria hizi, tukiangalia katika maeneo mbalimbali ambayo tumezileta hizi Sheria: Je, zimejibu maswali ambayo tunayo katika jamii zetu? Tujiulize, kwa mfano, Sheria zinazohusiana na ujangili, zimesababisha ujangili usiwepo? Sheria zinazohusiana na madawa ya kulevya ambazo tumezileta katika Bunge letu, zimesababisha madawa ya kulevya yasiwepo? Haya ndiyo masuala ambayo pamoja na kuuchangamkia Muswada huu, tulipaswa sisi kama Taifa na kama Serikali, haya masuala tuwe tumeyajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ardhi kubwa inayoonekana ina uwezo wa kuzalisha chakula kingi cha umwagiliaji, ni kwa nini mpaka sasa hii hali haijatokea? Ni kwa nini kwa Taifa kama hili kuwe na njaa? Mimi nilikuwa nadhani, kama Serikali, tunatoa majibu ambayo hakuna mtu anayeuliza.



Kuna mtu mmoja anaitwa Flurton Chin aliwahi kuishi kule Marekani, alikuwa ni Askofu miaka ya 1955, aliwahi kusema *civilization is always in danger when those who have given the right to command have never learned how to obey*. Tunapata matizo sana, wale ambao wamepewa dhamana ya kuamrisha, wao wenyewe hawajawahi kujifunza kuwa watii.

Ni wakati muafaka kwa Serikali ambayo ilipaswa kwanza itambue hawa watu ambao tumewapa dhamana, ni tija kiasi gani wanaiweka kwenye maeneo ambayo tumewapa? Kwa sababu *we get pay for the value we bring at the market place*. Hawa ambao tumewapa dhamana kwa miaka 50 ya uhuru wetu na Mahatma Gandhi amesema kupata utajiri bila kufanya kazi ni kwa kiwango gani?

Ndugu yangu ameuliza hapa jana kwamba tunapokuwa na Mhandisi anayejua huu utaalam, ni *value* gani ambayo ameiweka kwenye *market place* ambayo inasababisha alipwe, Taifa hili liwe linamlipa? Badala ya saa zote kuja na sheria ambazo kimsingi, mwenzangu jana hapa amekuja na takwimu, Sheria zote tulizonazo Tanzania zinazotekelezeka ambazo zinakuwa *enforced* ni asilimia 37.

Kwa hiyo, hata kama tukileta sheria nyingi, kama wale watu ambao tumewaweka kwenye *market place* hawaleti ile *value*, maana yake tunapoteza muda kama Taifa. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani Wizara wakati mwingine ni vizuri ikafanya *home work* ya kutosha kwa sababu hizi Sheria tunazo nyingi sana kwenye makabati yetu. Tuna sheria



nyingi sana katika kila maeneo. Tunazo Sheria za *Traffic*, lakini bado matatizo yako makubwa, hakuna *Law Enforcemet!* Sasa hatuwezi kuwa na *Law Enforcement* kama wale ambao walitakiwa wasimamie hizo sheria wao wenyewe hawajahi kujifunza kuzitii hizo sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani, pamoja na sheria tunazozileta, ni vizuri Wizara na kama Taifa kwa pamoja hebu tuangalie, tatizo ni Sheria au tatizo ni mitazamo na fikra tuliyonayo kama wananchi?

Kwa hiyo, ilikuwa ni vizuri zaidi tukaangalia kwa nini katika kipindi cha miaka 50 pamoja na utajiri tulionao, pamoja na maeneo oevu tuliyonayo, hizi *wet lands* pamoja na miinuko mizuri tuliyonayo, ni kwa nini tumefika mahali tuna-*import apple* mpaka leo kutoka Afrika Kusini? Tuna-*import* matunda mpaka leo kutoka Afrika Kusini! Tumeshindwa kutengeneza hata *juice* zetu wenyewe hapa, tuna-*import* pamoja na maeneo mazuri tuliyonayo. Je, tukiweka hii Sheria itatufanya tusi-*import apples* kutoka Afrika Kusini? Itatufanya tusiagize matunda Afrika Kusini kama tunavyofanya leo tu kwa sababu tumeleta hii Sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukawa na Sheria nzuri imeandikwa, lakini kama hatujabadilika namna ya utendaji kazi, kama wenyewe hatujabadilika kifikra, hii ni kujaza na kuharibu makaratasi bila sababu na kujaza sheria nyingi katika hii nchi yetu.

Kwa hiyo, natoa ushauri kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri uko hapa, ni vizuri tungefanya *home work* ya kutosha. Hizi sheria zimekuja nyingi sana, lakini kila siku tunalalamika

hapa, Wizara zote, pamoja na sheria nzuri tunazozileta tumekuwa na matatizo. Ningeshauri Wizara, hebu tufanye *home work* ya kutosha, nini kiini cha matatizo? Hao Wahandisi tulionao wameleta tija kwa kiwango gani mpaka sasa? Ni aibu kwa Taifa hili, kama wenzangu walivyosema.

Mwenzangu jana amezungumza kwamba inaonekana Serikali ime-*paralyse*, haifanyi katika maeneo mengi, pamoja na Sheria hizi zinazoletwa kwa sababu hao hao wanaotakiwa wasimamie wameshindwa kusimamia. Ni vizuri tukafanya *assessment*, hawa wanaoitwa Wahandisi wameleta tija kiasi gani? Kwa mfano, mimi nikienda kwa Mhandisi yeyote hapa, hata nyie Mawaziri; na Waziri mwenyewe ni Mhandisi; nitakwenda kujifunza kitu gani kuhusiana na umwagiliaji? Yeye mwenyewe analeta tofauti gani? Nami kama Mwanathiolojia, kama mwenzangu jana alivyozungumza hapa.

Kwa hiyo, haya ni masuala ambayo kama Taifa, pamoja na sheria nyingine kuwa nzuri na upungufu uliopo, kama hatutabadika *mind set*, kama hatuta-*change*, watu wataka walipwe bila kufanya kazi. Bahati mbaya tumekuwa na wanasiasa ambao hawana *principle*, hatufuati taratibu, tumekuwa ni watu ambao tunaongea lakini hatutembe katika namna tunavyotakiwa tutembe, ndiyo maana inaleta shida katika Taifa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mimi ningekuomba, pamoja na mambo mazuri hapa, mimi nadhani inahitaji *transformation* kubwa katika Wizara, ni namna gani watu waweze kufikiri ili urithi ambao Mungu ametupa katika Taifa letu tuweze kuutendea haki na uweze kuwa na tija katika

Taifa letu, kuliko tukiendelea kujaza sheria ambazo kimsingi hukaa kabatini na wala hazibadilishi chochote. Kwa sababu tuna sheria nyingi sana katika nchi hii lakini zimekaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba niseme tu hayo kwa kifupi. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru.

Kuna tangazo moja lilikuwa limebaki, limechelewa kufika Mezani kwangu, linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mitaa LAAC - Mheshimiwa Rajab Mohamed anawaomba Wajumbe wa LAAC saa 7.15 mchana wakutane Ukumbi wa *Basement*.

Waheshimiwa Wabunge, bado tuko Iringa, sasa namwita Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, pia kuwapongeza na kuwashukuru sana Mawaziri wa Kilimo, pia Kamati ya Kilimo ambayo imeleta Muswada ili tuweze kuujadili hapa Bungeni na hatimaye kuupitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 80 ya wananchi wa Watanzania wanategemea kilimo na kilimo siku zote tumesema kwamba ni uti wa mgongo, na vile vile tulianzisha Kilimo Kwanza, lakini nafikiri huu Muswada ndiyo utaboresha mambo haya. Kwa hiyo, nasema hivi, hii Sheria ilicheleweshwa sana kuletwa hapa Bungeni. Wananchi sasa hivi, nikitoa mfano tu katika Mkoa wetu wa Iringa na hasa

Jimbo la Iringa Mjini, toka nimekuja hapa Bungeni, nimekuwa nikilalamika sana na pesa ambayo inacheleweshwa kwenye Jimbo letu hasa kwenye miradi hii ya umwagiliaji. (*Makofi*)

Kwenye Jimbo la Iringa Mjini kuna mradi wa *Kitwilu Irrigation*, katika Kata ya Kitwilu; kuna mradi wa *Mkoga Irrigation* katika Kata ya Isakalilo, lakini tumekuwa tukilalamika kwamba ni lini Serikali itaboresha hii miradi? Tumekuwa tukiilalamikia sana. Lakini ni imani yangu kwamba Muswada huu ukipitishwa, malalamiko yatakuwa hakuna. Nawashukuru sana Wajumbe na Wanakamati wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, wameainisha na wameonyesha vitu vingi sana ambavyo wanasema kwamba Serikali iviangalie, pengine naweza hata nikavinukuu, kwamba sheria hii isimamiwe kwa umakini kwa lengo la kumlinda mkulima wa kilimo cha umwagiliaji anufaike zaidi.

Hii ya pili anasema, wakati wa utekelezaji wa Sheria hii hasa katika kutenga maeneo ya umwagiliaji, wananchi wa eneo husika washirikishwe kikamilifu ili kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza katika utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji. Wamesema vitu vingi sana ambavyo Serikali inatakiwa iviangalie kuboresha hii sheria ili tuweze kuipitisha sasa tuweze kwenda. Sasa hivi hatuwezi kutegemea mvua kutokana na tabianchi. Tumeshona nchi nyingi sana zinazofanya kilimo cha umwagiliaji, hazipati matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu tuna maeneo makubwa sana ya kilimo, lakini tumekuwa hatuyatumii inavyopasa. Nawaomba wenzangu wote waliopo hapa,

hata kama ni Wapinzani, usiwe mpinzani kupinga kila kitu. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge kazi yetu ni kuishauri Serikali.

Kama kuna vitu ambavyo wanaona kwamba havijakwenda sawa, tukae pamoja tuupitisha huu Muswada ili Sheria iweze kuwanufaisha wananchi. Lakini huwezi kupinga kila kitu wakati sisi wenyewe kila siku tunalia, kila siku tunalalamika kwamba miradi ya umwagiliaji Iringa ipo, wananchi wameweka nguvu zao nyingi sana, Halmashauri zimeweka nguvu zao nyingi sana, lakini Serikali haileti pesa. Lakini tuna imani sasa kuna sehemu ya kwenda kuisemea, kuna sehemu ya kuibana kwa sababu imefafanua kabisa katika Sheria yao kwamba nani tumwone ili aweze kuleta pesa. Kwenye huu Muswada, kuna vifungu vingi wamesema kwamba watatafuta pesa yao wenyewe kuhakikisha kwamba sehemu zote zinaboreshwa, vikundi ambavyo vilikuwa vinashughulika na mambo ya kilimo vitakopeshwa pesa. Sasa mimi nashangaa kuona kwamba watu wanaukataa kuupitisha huu Muswada. Ni kwa sababu tu ni Wapinzani? Siyo kazi ya upinzani kupinga kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ni vizuri sana na mimi nichangie kwa sababu wananchi wa Iringa tunategemea sana kilimo katika Mkoa wetu wa Iringa na wananchi wa Iringa wasingenielewa kama nisingesimama na kuchangia Muswada wa Sheria hii kuweza kupitishwa ili waweze kunufaika.

Wananchi wa Iringa hasa Iringa pale Mjini, mimi nimeshatembelea vijana waliopo Kitwilu, wanapenda sana mambo ya kilimo cha mboga mboga cha matunda na

vitungu. Lakini nina imani kwamba sasa vijana wale hawatashawishiwa hata kufanya maandamano au vitu vyovyote kwa sababu watakuwa wako *busy* na kilimo. Kilimo kile kitawasaidia. Lakini kitu kikubwa, baada ya kilimo, tutatafuta masoko, na imeelezwa wazi kwamba masoko yapo. Serikali yetu ilishakwenda mpaka Sudan ya Kusini huko ikaona jinsi ambavyo wananchi wale wanahitaji sana mambo ya mazao.

Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba tukiupitisha huu Muswada, mambo mengi yatakuwa sawa. Kama kuna mambo ambayo hayatakuwa sawa, basi tutafanya marekebisho. Lakini naomba niwaambie Wabunge wenzangu wote, kwamba leo hii tuupitisha huu Muswada ili tuanze kusonga mbele, tusirudi tena nyuma kusema kwamba urudishwe huu Muswada halafu tuanze tena kuleta, itachukua muda mrefu sana kuutekeleza huu Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, niwashukuru wananchi wa Iringa pia. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Pauline Gegul, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, niseme kwamba hatupingi tu kwa sababu ni Wapinzani, tunapinga *with reasons*. Tuna sababu za kutosheleza. Lakini siyo

sababu nyepesi nyepesi, ni sababu nzito kwa maslahi ya wananchi na kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze moja kwa moja ni sababu zipi ambazo Kambi ya Upinzani tunapinga Muswada huu? Zimeelezwa ipasavyo katika hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeeleza ni kwa nini tunapinga Muswada huu? Kwanza, umeandaliwa kwa kukurupuka, hakuna maandalizi ya kutosha na ndiyo maana mchangiaji mmoja alisema kwamba hata haiku-*capture* upande wa Zanzibar. Lakini kuna sababu mlizotoa katika kuanzisha Muswada huu. Serikali imeeleza sababu kuu nne. Sababu ya kwanza wanasema, nanukuu: "Madhumuni ya kuanzisha Muswada huu ni kwa sababu kumekosekana mfumo wa kisheria wa kulinda na kuendeleza ardhi inayotumika kwa umwagiliaji."

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Sheria nyingi sana. Tuna Sheria za Maji na tuna Sheria za Ardhi. Lakini utekelezaji wake ukoje? Nani anafuatilia? Tumesema kwamba mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji visiingiliwe, watu wasiende kuvivuruga. Lakini hivi tunavyoongea, ukiangilia vyanzo hivyo vinavurugwa sana na Serikali hii haichukui hatua. Siyo kwamba hatuna Sheria, tuna sheria, utekelezaji wake ukoje?

Kwa hiyo, hata hiyo sababu ya kwanza ni nyepesi. Lakini sababu ya pili iliyotolewa kuanzishwa kwa Muswada huu nyepesi sana, kwamba hayo maeneo mengi hayaendelezwi. Kutokuendelezwa kwa maeneo hayo,



wachangiaji wengi wamezungumza kwamba tatizo la nchi yetu ni kutokipa kipaumbele kilimo chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema Kilimo ni Uti wa Mgongo wa nchi hii. Hebu angalia bajeti ya Kilimo yenyewe, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo juzi tu alitueleza jinsi gani hata fedha za pembejeo za kilimo Shilingi bilioni 112.4, ni chache kiasi gani? Ukiangalia ni jinsi gani yule mkulima ambaye ana ardhi hiyo anataka kuiendeleza anashindwa kwa sababu kwanza tu pembejeo za kilimo unazompatia, zile mbegu tu mkulima wa Watanzania anapelekewa kilo 10 za mahindi za mbegu. Atakwenda kuiendeleza hiyo ardhi kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukumbuke mwaka 2012 mlituletea trekta za Suma JKT, tunapita hii njia hapa tunaona lile jengo lipo patupu kabisa, hakuna chochote! Hizo trekta mpaka leo hazipo. Unategemea huyu mwananchi ataendelea kwa jembe la mkono, kwa miaka 52 ya uhuru? Tatizo siyo Muswada umekosekana, tatizo ni Serikali iliyokaa madarakani kwa miaka 52 ya uhuru, imekufa ganzi. Hawajui mahitaji ya Watanzania, hawajui mahitaji ya wakulima. Unampelekea mbolea ya Urea akapandie wakati kwenye ardhi yake haitaki! Lakini tunawaambia kila wakati tunaposimama.

*(Hapa kengele illia)*

**MBUNGE FULANI:** Hapana.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Hapana, hiyo kengele mnachakachua!



**MBUNGE FULANI:** Kwa kweli!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika naomba muda wangu uuangalie vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Inakukumbusha tu urudi kwenye hoja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Siyo kwa kengele!

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya tatu ni kutokutekelezwa na kuhujumiwa kwa miundombinu. Lakini kwenye Muswada huu, unaona Serikali za Mitaa hamkuwasema ipasavyo. Muswada umeshuka tu kwenye Tume, kwenye Mkoa na kwenye Wilaya. Lakini ukiangalia Serikali za Mitaa hata zile skimu tulizonazo, hamjawapa kipaumbele katika kusimamia. Hivi ndugu zangu mnategemea kwamba nani atalinda hizo skimu ambazo mnakwenda kuziandaa? Kwa sababu Muswada huu kwa kiasi kikubwa Serikali za Mitaa wamepuuzwa, ambao ndio wako na wananchi na wako na ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala zima la uelewa mdogo wa wananchi. Mmezungumzia kwamba wananchi hawa hawaelewi, wanatakiwa waeleshwe. Lakini kumbukeni kwamba miradi mingi ya maendeleo iko kwa hao wananchi na wanachangia.

Tatizo kubwa wasilolielewa wananchi, angalia Mikutano ya Vijiji, taarifa za Mapato na Matumizi zinasomwa mara ngapi? Mikutano Mikuu ya Mapato na Matumizi, ukiangalkia kwenye Halmashauri zetu, hakuna mtu

anayehangaika na wananchi kupata mahesabu yao kwa mambo ambayo wameyachangia. Kwa hiyo, tatizo siyo uelewa wa wananchi; tatizo ni ufisadi uliokithiri. Hakuna mtu anayemwajibisha yule wa chini, wananchi wanachangia, wanavunjwa moyo kwa sababu haya mahesabu hayasomwi kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kipengele (b) cha gharama. Kwa kweli Muswada huu unakwenda kuwabebesha Watanzania gharama kubwa sana. Ukiisoma kuanzia ibara ya 3(6) lakini ibara ya (6) ya (10) mpaka (11) zinaanzishwa Ofisi za Mikoa na Tume inaamua popote pale kuanzisha Ofisi. Lakini pia Tume itaajiri watu ambao inaona wanafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo siyo watumishi. Watumishi tunao, hata katika Halmashauri na katika Serikali tunao. Lakini angalia hizi gharama ambazo zote zinakwenda kuanzisha hizi Ofisi nchi nzima, pamoja na hao watumishi. Ni pesa kiasi gani zitatumika kuwalipa? Naishauri Serikali kwamba badala ya kutumia fedha nyingi kuanzisha Ofisi na watumishi na hizo samani za Ofisi, ni vizuri hizo pesa tuka-*inject* sasa kwenye kilimo ili iwasaidie wananchi hao kuboresha kilimo chao. Lakini kikubwa zaidi, nimeona ni jinsi gani ambavyo Serikali mmesahau mlikotoka.

Mwaka 1972 katika nchi hii mfumo wa Serikali za Mitaa ulifutwa. Lakini mwaka 1980 mnakumbuka Chama cha Mapinduzi wakati wa uchaguzi Mheshimiwa Mkuchika anakumbuka; mwaka 1980 CCM walishauri na wakalaumu sana mpango wa Serikali kukurupuka na kufuta Serikali za Mitaa na mnakumbuka mwaka 1976 *out break* ya *cholera*,

miaka hiyo hatukuwepo lakini tunasoma kwenye vitabu, jinsi ambavyo Serikali ilikuwa na hali mbaya na wananchi wanahangaika, miundombinu hairekebishwi, dawa hazipatikani, mkashauri kwenye uchaguzi wenu wa mwaka 1980 kwamba Serikali za Mitaa zirudishwe.

Katika Muswada huu madaraka yote ya Serikali hizi zinachukuliwa, zinapelekwa kwenye ngazi ya Mkoa. Mkoa mmewapa kazi za Serikali za Mitaa na mmesahau *Decentralization by Devolution*, mmesahau kwamba mamlaka tuwapelekee wananchi wa chini. Baba wa Taifa alisema kwamba hakuna uamzi mbovu uliowahi kufanyika katika nchi hii kama kupuuza Serikali za Mitaa.

Katika Muswada huu mnaeleza madaraka yote, majukumu yote yatafanywa na Ofisi za Mkoa. Kwa hiyo, ndiyo sababu ambazo nasema kwamba, huu Muswada sio vizuri tukaupitisha kwa afya ya wananchi wetu kwa sababu, kwanza utafeli na hautaweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini muhimu la mwisho ni suala la Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri wake kwenda kutwaa maeneo ya wananchi. Ni jambo ambalo limezungumzwa katika Ibara ya 17 na Ibara ya 18 kwamba Waziri anaweza akatangaza amri kwenye gazeti akasema eneo fulani likatwaliwe; Waziri anaweza akaunganisha maeneo mawili ya maeneo hayo ya umwagiliaji bila kuangalia *set-up* ya Mitaa yetu na vijiji vyetu; lakini pia Mheshimiwa Rais anaweza akatwaa maeneo hayo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi tuna ugonjwa wa Katiba. Tanzania tumekumbwa na ugonjwa wa Katiba. Serikali, imekumbwa na ugonjwa wa Katiba. Chochote ambacho hakiendi vizuri utasikia subirini Katiba Mpya inakuja. Mbona hapa Madaraka ya Rais bado mnaendelea kuyabeba? Mbona hapa Madaraka ya wananchi bado mnayachukua? Waziri unaweza ukatangaza eneo lolote likienda likapelekwa kwa watu ambao wana fedha zao wakaendeleza kilimo cha umwagiliaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri kwamba Ibara ya 17 na 18 haina afya kwa wananchi wetu, kwa sababu hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee - Waziri Kivuli wa Ardhi wa Upinzani haijajibiwa. Tulishauri katika Bunge hili kwamba, hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee, ijibiwe kwamba Serikali na Wizara ya Ardhi wakae chini, watafute *Data Bank* ya nchi hii, ya ardhi tulizonazo. Mpaka leo ile hoja haijajibiwa na bado mnakuja na mambo yale yale!

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wakisikia kwamba tunapitisha Muswada kama huu, kwa kweli watatushangaa sana. Kwa hiyo, nishauri kwamba Wizara zote zikae, za Maji, za Ardhi na Kilimo, mwangalie kuna ardhi kiasi gani kabla hamjampeleka Mheshimiwa Rais kwenye vishawishi vya kutoa maeneo haya na kabla Waziri husika hajatoa amri, maana ni amri, siyo ombi, ni amri kwenye gazeti. Kabla hamjafanya hayo, mkayatimize yale ambayo tuliwapa mkayafanye wakati tunasubiri ni jinsi gani Watanzania hao watapata haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa kuhusu madaraka ya Waziri wa Fedha, Ibara ya 55 ya Muswada

huu inasema kwamba, Waziri wa Fedha anaweza akaamua tu baada ya kuwasiliana na Tume, kuwapatia fedha kiasi ambacho wanataka pale ambapo wanakuwa wamepungukiwa. Lakini ukiangalia Bunge hili Tukufu ndicho chombo ambacho kinachopitisha bajeti ya nchi hii. Nahoji mamlaka ya Waziri wa Fedha, kupatia tu fedha za walipa kodi kwamba wanaipatia Tume. Mimi naomba Kifungu hiki kiangaliwe upya, kwa sababu haiwezekani Waziri wa Fedha akachukua madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Pauline Gekul. Kama nilivyoeleza, sasa namwita Mheshimiwa Subira Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa na mimi kutoa mchango wangu kwenye Muswada huu, na ninaanza kusema nauunga mkono kwa asilimia mia moja. Lakini naomba nimpe taarifa Msemaji wa mwisho aliyesema kwamba, Halmashauri zimepuuzwa kwenye Muswada huu na nimwelekeze, hata kwenye hotuba yao ya Kambi Rasmi ya Upinzani, ukurasa wa 15, Msemaji wao anasema, mfano, Kifungu namba 13 (1) kinachoanzisha ndani ya Halmashauri Idara ya Umwagiliaji. Kwa hiyo, Halmashauri, kwa mujibu wa Hotuba yao, hata yeye Msemaji wa Kambi ya Upinzani ameona Muswada Kifungu Namba 13 unatambua na umeelekeza uanzishwaji wa Idara ya Umwagiliaji ndani ya Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu na pia naomba nimsaidie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali, haikurupuka. Mimi Sio Msemaji wa Serikali, lakini suala la kilimo siyo la Muungano. Kwa hiyo, Muswada huu ambao umeletwa humu ndani ni Muswada ambao unaangalia mambo ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nadhani Serikali ilikuwa imejipanga, kwa kuwa imeanzisha Sera ya Kilimo Kwanza, mwaka huu imeiweka ndani ya vipaumbele sita. Imeona umuhimu wake, ndiyo maana katika utekelezaji wa Sera ya Kilimo Kwanza katika nguzo ya pili namba 1(4) ilijielekeza kwamba, itaongeza bajeti ya umwagiliaji mpaka mwaka 2015, ili kuongeza hekta milioni saba. Kwa hiyo, ni imani yangu, kama Serikali ina malengo yake, lakini lazima ijipange inayatekeleza vipi?

Kwa hiyo, uanzishwaji wa Tume hii ya Umwagiliaji, nilidhani ni mikakati ya kuona namna gani malengo yaliyowekwa kwenye Sera ya Kilimo Kwanza na namna mpango huu wa utekelezaji wa kipaumbele hiki cha kilimo katika mpango wa *Big Results Now* unafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono kwa misingi hiyo, na kwamba kwa kuwa Halmashauri zimetambuliwa, na kwa kuwa uundwaji wa Idara siyo suala la Baraza la Madiwani, Baraza la Madiwani halina mamlaka ya kuanzisha Idara. Ni Wizara ya *TAMISEMI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwa kuwa mimi natokea Mkoa wa Pwani na tunayo mabonde; bonde la Mto Rufiji, Bonde la Mto Ruvu, nadhani uanzishwaji wa Tume hii kupitia

*scheme* ya umwagiliaji ya Yavayava, Mkuranga, kupitia *scheme* ya umwagiliaji ya Segeni – Rufiji, kupitia *scheme* ya Chauru, Ruvu, ninaamini kwa kuanzisha Tume hii na kama Serikali ilivyoshauriwa na Kamati yetu ya kuongeza mafungu katika Idara hii ya Tume ya Umwagiliaji, nina uhakika 80% ya wakazi wa Mkoa wa Pwani wanaotegemea kilimo, mkombozi wao ni Tume hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tumeona uhaba wa Wataalamu kwenye sekta hii ya Wahandisi wa Umwagiliaji na ndiyo maana kulikuwa na Ofisi za Kanda, kushushwa Idara hii kwenye ngazi ya Halmashauri kwamba, Halmashauri yenyewe ndiyo itakuwa inapanga miradi hii, inafanya upembuzi yakinifu, mimi nina hakika kwamba kilimo katika maeneo yetu kitafanikiwa. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tuunge mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine la ushauri wangu sasa, kwa kuwa tumekuwa na *scheme* za umwagiliaji, na kwa kuwa mafungu yaliyokuwa yanawasilishwa pale ni kidogo kidogo na ndiyo maana utekelezaji wake ukawa unakwenda pia kidogo kidogo, naomba kwa kweli, kama ushauri wetu wa Kamati tulivyoshauri, kama Serikali imedhamiria, na tunajua imedhamiria ndiyo maana imeweka mojawapo ya kipaumbele, zipo sekta nyingi zina changamoto; lakini tumeona kilimo ni kipaumbele. Tunaamini kilimo hiki kikizalisha ndipo mapato yatakapokusanywa.

Naomba kwa kweli, kama ambavyo Muswada huu unavyosema na kama ambavyo Kamati imesema, kanuni



zitungwe haraka na utekelezaji ufanywe haraka. Mimi naomba tuupitishwe ili Serikali ifanye kazi yake iliyokusudiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika bajeti ya Wizara ya Kilimo, tulishauri kama Waheshimiwa Wabunge, tuangalie kwamba, kwa sababu, unaweza ukawa na *resources*, lakini ukizitawanya; hebu tuangalie mipango ambayo tumepanga mfano *SAGCOT*, kama tunatarajia, tumechagua Mikoa sita ya kuzalisha, tuziangalie zile *scheme* za Mikoa ile zimalizike, ili iweze kuzalisha chakula kwa ajili ya nchi yetu. Lakini pia, tukimaliza *scheme* za Mikoa sita zikaja *scheme* za *SAGCOT*, tukaja *scheme* za Mikoa mingine, mimi naamini kwamba kilimo katika masuala ya umwagiliaji kinaweza kikapata mafanikio. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho, niseme, kwa kuwa tunatambua mabadiliko ya tabianchi, naomba Watanzania wenzangu, kwa kweli kuendelea kutegemea kilimo cha mvua, tumeona athari zake. Kuendelea kutegemea kilimo cha mvua na namna ambavyo tunaendelea kuteketeza misutu yetu, namna ambavyo tunachangia mabadiliko ya tabianchi, hata kama Tume hii itaundwa, Muswada huu najua utapita, lakini kama tusipojipanga katika utunzaji wa vyanzo vile vya maji, utunzaji wa maeneo haya ambayo tunajenga *scheme* za umwagiliaji, kwa kweli, hata kama tunaweza tukasema masuala mengine siyo ya Serikali, ni sisi wenyewe wananchi tuone umuhimu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuishukuru Serikali; pia nishukuru tumepata *scheme* ya umwagiliaji



Misozwe – Muheza; tumepata pia *scheme* ya umwagiliaji maeneo ya Mashewa – Muheza.

Tunaomba pia upembuzi unaoendelea katika maeneo ya Potwe – Muheza uendelee na pia maeneo ambayo nimejielekeza katika mchango wangu huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii, hasa ukizingatia mimi natokea Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Kilombero. Kwa hiyo, unapozungumzia umwagiliaji, basi mimi natoka kwenye mazingira kama hayo. Huu Muswada na Idara mbalimbali zilizoanzishwa katika Wizara hii ya Kilimo ni kitu muhimu sana na tungeona matokeo kabla ya Muswada huu kuwepo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unasema kilimo labda kimezorota sana nchini Tanzania au umwagiliaji haupo eti kwa sababu Muswada au Sheria ilikuwa haipo. Lakini Wizara ilishaanzisha nia. Sasa leo watuambie, tangu walipoanzisha nia na Watendaji walianzisha nia, kitu gani kilichowafanya washindwe kufanya kazi zao? Serikali imechukua hatua gani kwa Watendaji hao? Kwa sababu ilianzishwa kwa nia ya kuboresha kilimo. Kimetokea nini? Watuambie! Sasa wanakuja na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo pale ninapokwenda na wachangiaji wengi, hasa wanayosema Wapinzani. Kwa wale wanaoitwa Wapinzani, wale ambao wanakwenda

kwenye vikao ambavyo ni *Caucus* kuweka msimamo wa pamoja ili kuona kwamba wanakuja kupinga yale ambayo ni ya wachache, lakini nasema hivi, wananchi ndio watakaohukumu.

Kama ilivyokuwa kodi za simu, wananchi vijijini wanalia, lakini tunaonekana Wabunge wote tulipitisha, tunakwenda. Lakini linakuja anguko lingine la *NHC* kwa kuwaambia walipe 10% kwenda kodi Serikalini, wakati hiyo *NHC* faida yake unakuta ni Shilingi milioni nne kwa mwaka. Lakini kwa thamani ya nyumba wanazojenga kwa kodi iliyopitishwa hapa Bungeni, watalipa Shilingi bilioni tano. Itabidi wakakope benki wailipe Serikali na *NHC* ita-*paralyse*. Bunge hili ndiyo tunafanya haya mambo!

Kwa hiyo, hii ni kazi ya *CCM*, siyo sisi ambao tunaitwa Wapinzani! Tuseme kweli ili *Hansard* zinakili na ikitokea siku matatizo yanatokea ndani ya nchi hii, hata wajukuu zetu watakuja kuangalia, tulizungumza nini? Kwa hiyo, ni lazima tuseme, hatuogopi kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha Muswada huu Na. 9, kinasema kwamba, Mkoa ndiyo utafanya uteuzi wa Wataalamu wenye uzoefu. Hivi *SUA* iko pale inafanya kazi gani? Si inazalisha Wataalamu? Kwa nini wasipate nafasi ya kuajiri basi? Watu waombe, watu waajiriwe! Kwa nini msemi eti watatafuta watu wenye uzoefu ambao wataingia kwenye hiyo Tume? Kwa nini msemi kwamba itasimamia ajira badala ya kuteua? Mtateua mpaka lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika vifungu mbalimbali vinapishana. Kifungu Namba 13, kinaeleza utendaji wa majukumu yake ya Kitaalamu, Mhandisi wa Umwagiliaji wa Wilaya atawajibika kwa Tume.

Kifungu cha 13 (7), kinasema yule Mkuu wa Umwagiliaji pale katika Wilaya hatawajibika kwa Mkurugenzi, atawajibika kwa Tume katika ngazi ya Mkoa. Lakini Mkurugenzi amwezeshe kifedha katika *own source* anazokusanya, sijui na wapi? Sijui *DADPS*, itaingia huko, mimi sijui! Sasa inakuwaje Mkurugenzi amwezeshe katika masuala ya Ofisi katika masuala ya fedha, lakini asiwajibike kwa Mkurugenzi, aende akawajibike kwa ngazi ya Mkoa? Hapa kuna mgongano wa hivyo vifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaposema haina maana kwamba tunapinga kila kitu, lakini tunasema ili mwangalie kwa makini ili mwone kwamba, hata kama mtalazimisha kupitisha hii Sheria kwa uwingi wenu, lakini mjue kwamba kuna tatizo katika hii Sheria. Ni bora mkawasikiliza wachache mkaona ni namna gani ya kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasema hivi, kuna haja gani ya kuunda Tume? Kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa mpaka sijui wapi? Kwa nini msiboreshe Idara ya Umwagiliaji katika Wizara? Wale wafanyakazi waliokuwa wa Idara wanafanya kazi gani sasa? Wako wapi? Mnawapeleka wapi? Watoto wetu kwa nini msiwape ajira wako huko mtaani? Chuo cha *SUA* kimesomesha Wataalamu siku nyingi, kwa nini leo hamwachukui hawa watu ambao wako huko mtaani hawana ajira, kwenda kuboresha kilimo chetu? Tatizo kweli

ni Sheria? Tatizo la kilimo hapa nchini kwetu ni Sheria? Hebu niulize, kule Kilombero kwenye mradi wa umwagiliaji Ziwinali, umeanza tangu mwaka elfu mbili sijui na ngapi sina kumbukumbu vizuri, lakini mpaka leo haujakwisha; lakini ukienda Ziwinali pale Kilombero kwenye ule mradi mamilioni yameishaingia, lakini ule mradi ukiwauliza wananchi, wanasema hakuna maji yanayotiririka kipindi chote cha mwaka.

Mradi umejengwa katika eneo kavu, maji yanakuja kipindi cha masika na kipindi kingine hakuna maji. Utauita ni mradi wa umwagiliaji huo? Wataalamu wapo wapi? Ma-engineer wapo wapi? Nia njema ya Watendaji wetu; ni usimamizi ndiyo unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa Serikali za Mitaa, tumekwenda kukagua mradi wa maji hapa kwa Badwel, hapo Bahi. Ule mradi kwanza pale hakuna maji; ule mradi wamejenga mfereji, hakuna bwawa. Wanasema wanasubiri bwawa lijengwe, maji yatakayotoka Kondoa. Ni kitendawili, mabilioni ya hela yameingia pale!

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji huko Njagi – Kilombero; mpaka leo wakandarasi wameshabadilishwa karibu mara tatu kwa mradi mmoja. Mradi hauna maji, ukiuliza wenyeji wanakwambia hapa maji yanayokuja ni machache kuliko mashamba yaliyoko bondeni. Lakini Serikali imeingiza fedha, fedha zimeteketea, mradi mpaka leo haujaanza. Sasa ni nini? Nia njema za Watendaji, ufisadi umejaa!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vema mkaboresha hizo Idara na pesa zikaingia. Lakini nia njema ya Serikali iko wapi? Mfuko? Yaani leo mnatwambia hapa kwamba Tume hii itapata hela kwenye kuuza *scraper*?

Leo Serikali inazungumzia *scraper* kweli katika kuboresha kilimo? Eti mitambo chakavu, kweli? Aibu! Hii nchi leo inategemea kuboresha kilimo kwa *scraper*! Haiwezekani. Lazima mbadilishe mwelekeo, lazima mbadilishe mtazamo.

Asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima, nami ni mtoto wa mkulima. Leo mnasema mnaboresha kilimo cha umwagiliaji, naiuliza Wizara, kila siku nasema hapa, watu wamelundikana na mipunga kule Kilombero, masoko yako wapi? Kwa nini hamtuletei masoko? Leo mkianzisha hicho kilimo cha umwagiliaji mazao yakiwa mengi, tutakwenda kuuza wapi? Hebu tuuze kwanza yale ambayo tunayo, halafu mkileta hiyo ndiyo tutajua kweli hawa wenzetu wanataka kutufanyia mema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kibaya zaidi, kama walivyochangia wachangiaji wengine, mbolea inakuja wakati tayari watu wameshalima, wameshapanda, mipunga imeshakuwa mikubwa na mahindi yamekuwa makubwa, mnaleta mbolea.

Bado mnatakiwa mjipange, mkitueletea Sheria, haitusaidii kuboresha kilimo. Wanatakiwa watu wenye nia njema ya nchi hii, wazalendo, kwa kutumia Wataalamu waliokuwepo kuziimarisha Idara zilizoko ndani ya Wizara

zenu, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji ili tupate chakula cha kutosha na akiba tuuze nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi, watu wa kutoka nje hawana nia njema sana na sisi. Nchi yetu ni tajiri. Huu mpango wa kutuletea michele kutoka nje ambayo tayari wao kule wamethibitisha haija-*expire* wakati tayari imesha-*expire*, wamelima kwenye mbolea ya ajabu, kwao wanalisha ng'ombe, mnatuletea huku mnaacha kutuboreshea tulime wenyewe mchele wetu na mahindi yetu mazuri ili tuwalishe Watanzania, hii nchi tunaipeleka kubaya. Mnatutakia nini *CCM*?

**MBUNGE FULANI:** Waambie!

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Eeh, Serikali ya *CCM* mnatutaka nini Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lazima tuchangie Watanzania wajue kwamba mnakotupeleka siko. Hata mkitubeza, lakini ukweli utabaki pale pale kwamba lazima tubadilike katika mifumo, katika mitazamo, mshirikishe jamii nyingi; sijui kama hii mmekwenda pale *SUA*, mmewaambia wale Wataalamu, wamewapa utaalamu, wamesema sasa kilichokosekana hapa ni Sheria, eeh! Lakini mkienda huko chini kwa Watanzania wenyewe, kweli Sheria ndiyo tatizo la nchi hii? Tatizo la umwagiliaji nchi hii ni Sheria? Siyo sheria! Ni nia njema ya Watendaji na uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi kuendelea. Nashukuru sana kwa kunipa hii nafasi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mwidau.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Lakini kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutuletea Muswada huu, ili kuweza kuboresha Sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze tu kwa kusema ninachokiona hapa ni hofu iliyopo miongoni mwetu inayoendana na kiu ya Wabunge, kuhakikisha Watanzania wanaondokana na umasikini kupitia kilimo cha umwagiliaji. Hiyo ni hofu tu. Lakini hofu haiwezi kujibiwa na hasa katika suala la utawala bora bila kutunga Sheria madhubuti itakayokwenda kusimamia hofu hiyo na kuweka utekelezaji wenye tija kwa kuleta maendeleo katika nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana mimi nasema kwamba naunga mkono Muswada huu, ninaamini unachoambiwa Mheshimiwa Waziri baada ya Muswada huu kuwa sheria, ni usimamizi wa dhati. Nilichokiona hapa na ninashukuru Waheshimiwa Wabunge na Mbunge mwenzangu aliyetoka kuchangia sasa hivi amesema, wakati mwingine watendaji ndiyo ambao wanaangusha nia njema ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi na si Chama cha Mapinduzi ndicho kinachowaangusha,



hapana! Wale watendaji mle ndani wana itikadi mbalimbali na huwezi ukajua wana itikadi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nachotaka kumwambia Mheshimiwa Waziri, asikubali haya yatokee.

**MBUNGE FULANI:** Sawasawa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Leo tunampa nyenzo ya kwenda kukomboa maisha ya Watanzania kupitia kilimo cha umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri ukakae macho, ukasimamie sheria hii ili ikafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niendeleo kusema, nina hofu sana na hawa ambao wamebainishwa hapa na Mheshimiwa Susan Kiwanga, inawezekana wengine wanaitikadi tofauti na wanafanya makusudi ili tusiende mbele. Mheshimiwa Waziri kasimame imara, mara zote utawala bora utaongozwa na sheria na ukishaongozwa na sheria, ukisimamiwa vizuri malengo yatafikiwa na nia njema ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya kuwakomboa wananchi itapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia kwenye Muswada wenyewe, niseme mambo mengine mawili. Jumuiya ya *SADC*, baada ya kufanya utafiti wa kina ikagundua kwamba, tena siyo katika Tanzania tu ni katika nchi zote za *SADC*, uko upungufu katika eneo la umwagiliaji. Sasa hivi kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi, kumekuwa na vurugiko kubwa la misimu ya mvua na hivyo kusababisha sekta hii ya kilimo cha umwagiliaji isiende mbele. Jumuiya hiyo ikagundua katika nchi hizi za *SADC*,



ukosefu wa miundombinu ya kuvuna maji pamoja na miundombinu ya kisasa ya umwagiliaji, ni tatizo linalopelekea sekta ya umwagiliaji kuwa nyuma na kutokukidhi mahitaji ya chakula katika nchi za Jumuiya ya SADC. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Jumuiya ya SADC iligundua kwamba matumizi mabaya ya maji, tena siyo katika Tanzania, nchi za SADC, kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na kutokuwa na ufanisi mkubwa katika kilimo cha umwagiliaji. Pia kuna gharama ya kuanzisha mifumo ya umwagiliaji na matumizi mabaya ya vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yaliyotolewa na SADC, nikishayasema haya, sasa nitarudi kwenye Muswada na nitawaambia Watanzania sheria hii inasema nini. Nchi za SADC walisema ni lazima sasa kuwepo na sheria za kukuza na kuboresha usimamizi wa vyanzo vya maji ili kukuza kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi na mapendekezo ya SADC pia ilikuwa kutekeleza kuwepo kwa mipango mizuri ya usimamizi kijimbo kulingana na hali halisi katika kila nchi ya SADC ikiwemo nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mapendekezo ya SADC pia ilikuwa ni kuboresha teknolojia nyepesi za gharama nafuu katika kilimo cha umwagiliaji na kukuza matumizi mazuri ya vyanzo vya maji kupitia mipango mizuri ya kisheria na kuingiza dhana ya ufugaji wa samaki kwenye miundombinu ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sheria hii sasa pia inaendana na maazimio mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamefanyiwa utafiti mkubwa wa kina, kama mtu hana imani na watafiti wetu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi lakini hata hawa watafiti nje ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kupitia *SADC* wameyasema hayahaya ambayo leo ndiyo tunayafanyia kazi katika Bunge hili. *Bravo* Serikali ya Chama cha Mapinduzi, endelea mbele na Muswada huu wa Sheria kwa sababu hata *SADC* imeona, imefanya utafiti wa kikanda na imefikiri kwamba iko haja ya sheria kutungwa ili zikidhi haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukienda kuangalia hayo, ndiyo yanayojitokeza kwenye Muswada ambao leo uko mbele yetu. Muswada huu una nia ya kwenda sambamba na *Tanzania Development Vision* ya 2025. Muswada huu una lengo la kujibu maswali ya *Millenium Development Goals* ambapo sisi ni wanachama na tunazitekeleza. Muswada huu unaenda kujibu hoja za *Rural Development Strategy* ambayo tunakwenda kuitengeneza kupitia katika sheria hii ya umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaposema tunakwenda kuanzisha Tume hii, Tume hii inarudisha utawala bora wa usimamizi wa rasilimali za umwagiliaji. Badala ya kuziacha kwenye Kanda, badala ya kuziacha Wizarani huko, sasa tunakwenda kuhakikisha kwamba mfumo wa kiutawala na dhana ya umwagiliaji inashuka mpaka kwa wananchi kule vijijini. Nimesoma hapa *Rural Development Strategy* ndiyo inaeleza hayo. Kwa hiyo,

unaona kabisa hii sheria ndiyo inakwenda sasa kujibu maswali hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mradi wa umwagiliaji kijiji cha Ndongosi. Mradi ule unasimamiwa na Ofisi ya Bonde la Maji na Makao Makuu ya Ofisi ya Bonde la Maji kwa sasa kabla ya sheria hii iko Mtwara. Hebu fikiria kama hatutarudisha kuwa na ofisi katika Wilaya kama ilivyosemwa hapa, hivi wale wananchi wa Ndongosi wanapokwama kwenye mradi wa umwagiliaji kule Ndongosi, waanze safari mpaka Mtwara kwa mfumo uliopo sasa, tunataka kwenda mbele ama kurudi nyuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inatupeleka mbele na sijui kwa nini tunakuwa na kigugumizi katika hili. Nakubali na ile hofu kama nilivyosema mwanzo, wako Wabunge wanahofu, ni kweli na ninarudia kusema Mheshimiwa Waziri, sheria hii ukitaka Watanzania waone manufaa yake, ni lazima hofu hii ya Wabunge iondolewe kwa usimamizi wako mzuri na kuhakikisha *resources* hizi za maji zinapatikana na kilimo cha umwagiliaji kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutakuwa sisi tunajitendea haki wenyewe kama hatutakubaliana na sheria ama na Muswada huu kwamba, kwa mfano, kifungu cha 4 kinasema, Tume inaweza kuwekeza kwenye maendeleo ya umwagiliaji kwa kadiri itakavyokuwa inafaa. Mpaka sasa tumetegemea kunyang'anyana rasilimali za umwagiliaji, fedha za kuendeleza umwagiliaji, hakuna chombo kinachosimama chenyewe kuhangaika kutafuta nyongeza ili rasilimali hizi ziwafikie Watanzania. Kifungu cha (4) kinaonyesha nia njema na kazi kubwa inayopewa chombo

ili kuweza kukidhi maswali ya Watanzania kuhusu vyanzo vya fedha na mambo mengine yatakayosaidia kuendesha sekta ya umwagiliaji, naunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha (5), hicho sasa naomba niishauri Serikali. Katika kifungu hiki cha (5), sheria haijasema ni namna gani itakwenda kuingiliana na Sheria ya Maji (*The Water Act*). Kwa sababu sheria hii sasa inayokwenda kuipa Tume mamlaka ya matumizi ya maji, inatakiwa iende sambamba na Sheria ya Maji ili huko mbele tusiwe na mgongano. Haya ni maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri tukiyasema wewe utaangalia tunafanyaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 27, kinataja makundi na *scheme* za umwagiliaji lakini nashauri Mheshimiwa Waziri kupitia kwa Mheshimiwa Naibu Spika, makundi haya yote yametajwa lakini hatuna kundi ambalo litasimama kama ni kundi la umwagiliaji kwa maana ya uanzishaji wa *scheme* za Taifa. Tuwe na *scheme* zile ndogondogo, mwaka 2008/2009, Wizara hii kupitia hotuba ya bajeti, ninayo hapa, hotuba ya bajeti ya mwaka 2009/2010, imefundisha wakulima mpaka kipindi hicho walikuwa siyo chini ya 600, imefundisha wataalamu kwenye masuala ya umwagiliaji wasiopungua 150. Nafikiri kwamba haya ndiyo makundi ya umwagiliaji yanayotakiwa kutambuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuyatambue makundi ya wakulima wadogowadogo, tuyaboreshee zana za uzalishaji na kwa kupitia Muswada huu, tukiwasimamia vizuri, kilimo kitaendelezwa vizuri sana na wale wakulima

wadogowadogo kama zilivyokuwa *scheme*, nina *scheme* nzuri sana kwenye bonde la Mto Pesi, linatoa ukombozi mkubwa sana kwa wananchi, nina *scheme* kubwa sana Nakahuga, inafanya kazi nzuri sana, nina *scheme* nyingine nzuri sana pale Gumbiro, ni kazi nzuri sana ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tuna *scheme* nzuri sana ipo pale Mpitimbi, naomba niwaambie Watanzania tukisimamia vizuri sheria hii, hakika maeneo hayo niliyoyataja ndani ya Jimbo la Peramiho, unaona kabisa hali za wananchi zinavyokwenda haraka. Ukifika pale Mto Pesi na Nakahuga, wananchi wanaezeka nyumba zao bati kwa sababu ya kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, nachotaka kusema hapa, ni kusisitiza katika makundi haya, kwenye kifungu hiki cha 27, wakulima wadogowadogo wawezeshwe, wapewe nyenzo za kazi, wapewe zana bora za kisasa, wawezeshe kwa namna moja ama nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kengele inikute nikiwa nasema lakini naomba kusisitiza, *SADC* wametoa maagizo, wamefanya utafiti kwenye nchi zote za *SADC*, kwa hiyo, leo sisi Watanzania hapa, tunapokwenda kushughulikia sheria hii, naomba niwaambie Watanzania, sisi tumewahi, sina uhakika nchi nyingine za *SADC* kama wanayo sheria kama hii ya kwenda kujibu hoja za kiutafiti zilizofanywa kwenye nchi za *SADC* na kutoa ushauri wa kuwa na sheria itakayoenda kusimamia ufanisi mzuri wa kazi kupitia kilimo hiki cha umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ninakuomba Mheshimiwa Waziri, hatungependa kurudishwa humu ndani tukaulizwa ufanisi mbovu wa sheria hii. Hapo sisi wote na Wabunge wa

Chama cha Mapinduzi hatutakuelewa. Tunachotegemea utakwenda kusimamia vizuri sheria hii, utajibu tatizo la umwagiliaji, utaongeza tija kwenye kilimo katika nchi yetu, utaongeza chakula, utaondoa baa la njaa na aibu ya nchi yetu kuwa ombaomba wa chakula na haya yote yanaletwa ndani ili kujibu hayo ambayo ni kero kubwa ya Watanzania katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Wabunge wengi waliochangia hapa kila mmoja amegusia kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu na kwa kuzingatia kuwa zaidi ya 75% ya nguvu kazi ya Taifa ni wakulima. Tangu tupate uhuru nchi yetu ilikuwa ikihangaika sana katika suala la kilimo. Imekuja na misamiati tofauti, tulikuwa na kilimo cha kujitegemea, kilimo cha kufa na kupona, kilimo sasa, sasa tupo kwenye kilimo kwanza.

Kwa hiyo, kwa ujio wa Muswada huu wa Umwagiliaji, mimi naona itakuwa ni mwarobaini kwenye kilimo chetu, japokuwa tumechelewa lakini Waingereza wanasema *better late than never*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe Serikali na ninajua kuwa Tanzania ina uwezo mkubwa wa kuendeleza

kilimo cha umwagiliaji kwa sababu tuna vitu vyote muhimu. Tuna maji ya kutosha, tuna mito mikubwa na midogo, tuna maziwa vilevile ardhi *allhamdulillah*, Mwenyezi Mungu ametupa ardhi ya kutosha. Hapa Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia wameonyesha kuwa tuna hekta milioni kwenye ishirini na tisa na ushehe ambazo zinaweza kutumika katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kuletwa kwa Muswada huu sasa hivi, kwetu itakuwa ni ukombozi kwa wakulima endapo, kwa sababu huu ni Muswada, mapendekezo yote ambayo yametolewa na Wabunge yataweza kuboreshwa katika Muswada huu ili iwe sheria. Vilevile itakapopita sheria hiyo basi kusiwe na ucheleweshwaji wa kutunga Kanuni na taratibu nyingine. Kwa sababu kuna sheria nyingi ambazo zimepitishwa hapa Bungeni lakini mpaka leo bado hazijakuwa na Kanuni. Ningeomba katika hili, kwa sababu tunasema sasa hivi ni kilimo kwanza, basi kama kweli ni kilimo kwanza tukipe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nyeti sana ambalo linaweza likachelewesha utekelezaji wa haya yaliyomo kwenye sheria hii ni fedha. Fedha ni tatizo lakini najua Serikali wameahidi katika bajeti inayokuja kuwa Wizara hii itaongezewa fedha ili iweze kutekeleza yale ambayo itakuwa tumeyapitisha hapa Bungeni. Vilevile ukizingatia lengo kuu la Serikali kama walivyosema tunataka kuondoka katika uchumi mdogo na kuelekea uchumi wa kati na uchumi wa kati hauji hivi hivi, kuna viwanda.



Kwa hiyo, tukiwa na uzalishaji mkubwa ambao ni uzalishaji wa umwagiliaji wa uhakika, kilimo ambacho hakitegemei tena mvua, tutaweza kupata mazao, mbali ya kuwa na *security* ya chakula lakini vilevile tutakuwa na mazao ambayo tutapata fedha za kigeni na kuweza kuongeza thamani ili kuweza kuendeleza uchumi wetu. Kwa hiyo, naomba kama ambavyo tunachangia hapa basi muipe Wizara hii kipaumbele cha hali juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie kwenye vifungu. Nitaanza na kifungu cha 1 ambacho kinaelezea jina na kuanza kutumika Sheria. Hapa Mheshimiwa Mnyaa aligusia lakini naomba na mimi nisisitize. Kwa jinsi Muswada huu ulivyo ambao baadaye itakuwa sheria, hauelezi iwapo sheria hii itatumika upande upi wa Muungano.

Ningeomba kuisitiza, japokuwa suala la umwagiliaji siyo suala la Muungano lakini ni vizuri basi itamke, kwa kukaa kimya kimya bila kueleza itatumika upande upi wa Muungano inaweza baadaye huko ikaja ikaleta matatizo kwa sababu sasa tuko kwenye mchakato huu wa Katiba, hatujui Serikali moja, mbili tatu, nne, tano ambayo itapita. Napendekeza kuwa sheria itamke wazi iwapo utatumika upande upi wa Muungano kwa sababu kuna vitu vingi tena vinaingia humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 3 ambacho kinaelezea uanzishwaji wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Katika kifungu hiki cha 3(3) kinaainisha moja ya majukumu ya Tume kuwa ni kushtaki au kushtakiwa. Ni kweli tunataka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iwe huru lakini mimi mashaka



yangu makubwa hapa ni mfumo wetu wa kuendesha kesi. Mfumo wetu wa kuendesha kesi unachelewesha sana mambo.

Kwa hiyo, Tume itatumia muda mwingi na fedha vilevile ambazo zingeweza kwenda kufanya mambo mengine. Kwa hiyo, napendekeza kuwe na kifungu kidogo ambacho kitaipa Tume jukumu la kusuluhisha mgogoro wowote ndani ya muda wa miezi sita na kama itakuwa si muafaka, basi kabla ya kuchukua hatua za kulifikisha jambo hilo Mahakamani kuwe na usuluhishi. Vilevile Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataarifiwe juu ya usuluhishi huo na asimamie usuluhishi kwa niaba ya Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 3(6) ambacho kinaelezea Tume kuundwa na Bodi ya uendeshaji itakayokuwa na Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais na wajumbe wengine kumi watakaoteuliwa na Waziri.

Katika kifungu hiki mimi naona kuwa kinampa mzigo mwingine Rais wa kuteua. Kwa kweli watu wanalalamika sana, Rais atakapoteua kwa sababu sisi wenyewe ndiyo tunamlundikia uteuzi kwenye kila kitu. Mimi napendekeza kuwa sheria itamke kuwa kutakuwa na Kamati ya Uteuzi itakayoundwa kwa mujibu wa sheria na Kamati hiyo itakuwa na wajibu wa kutangaza nafasi ya Uenyekiti huo wa Tume na Watanzania watapata nafasi ya kuomba na vilevile itaainisha sifa na vigezo ambavyo vinahitajika kwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika wale wajumbe kumi ambao wataingia kwenye ile Bodi, ndiyo

kuna uwakilishi ambao umetoka Wizara mbalimbali lakini kuna Wizara moja ambayo ni nyeti sana, Wizara ya Nishati na Madini, hakuna mwakilishi ambapo tunajua kuwa *TANESCO* ni wadau wakubwa kwenye maji. Nadhani mtakumbuka katika Bunge hili kulikuwa na tatizo la Mto Pangani ambapo maji yake yalikuwa *tapped* na kukawa na tatizo kubwa la umeme. Kwa hiyo, nadhani tukipata mwakilishi kutoka Wizara ya Nishati na Madini pia itakuwa ni vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nielekee katika katika kifungu cha (5) ambacho kinaelekezea mamlaka na majumku ya Tume. Katika kifungu hiki kina maelezo mengi, kwa kweli amejitahidi wametoa maelezo mengi lakini yapo kinadharia na hayakugusia mambo muhimu. Mimi napendekeza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sheria iipe jukumu Tume kushirikiana *NEMC* na wadau wengine wa mazingira. Ni muhimu kwa sababu yanzo vya maji vinaenda kutumika na kuweka mtandao imara wa kudumu katika kupambana na tishio la jangwa. Tunajua kuna maeneo ambayo yana ukame kama Dodoma, Singida na baadhi ya maeneo ya Shinyanga. Kwa hiyo, Tume ikiweza kushirikiana vizuri na wadau wa mazingira nadhani jambo hilo litakuwa la maana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile sheria itamke namna ambavyo Tume itashirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuendeleza sekta ya umwagiliaji. Tumeona kuna baadhi ya maeneo katika Tanzania ambayo yana mitandao ya umwagiliaji, kama ukiangalia Karatu, kule

Mbulu na maeneo mengine Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wananchi wana mitandao hiyo ya umwagiliaji. Kwa hiyo, Tume itakaposhirikiana nao vizuri kwa sababu kuna baadhi ya Wabunge hapa wamechangia wakasema Serikali za Mitaa hazikushirikishwa ipasavyo. Mimi nadhani sheria hii itamke kuwa ni namna gani Tume itashirikiana nao, itasaidia kwa upande mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile sheria iweke wazi namna ambavyo Tume haitaingiliana na mamlaka nyingine ambazo zipo kisheria. Tunajua kuwa mamlaka hizo kwa namna moja au nyingine zinajishughulisha na shughuli za umwagiliaji kama RUBADA ambayo iko kule Rufiji na mamlaka nyingine nyingi. Kwa hiyo, Tume ikiweka ni namna gani itashirikiana na mamlaka hizo sheria itaweza kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sheria ieleze namna gani kuwa haitaingilia na mamlaka nyingine za nchi kama TANAPA, kwa sababu TANAPA wana maeneo yao. Kwa hiyo, ili kuepusha migogoro, tunajua kuna migogoro mingi ya ardhi, kwa hiyo, sheria hii kabla ya kupitishwa iweke bayana maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nieleke kwenye kifungu cha (8) na cha (9) ambacho kinaelezea uteuzi Mkurugenzi Mkuu na Wakurugenzi wengine wa Tume. Muswada huu unapendekeza kuwa Mkurugenzi Mkuu atateuliwa na Rais na Wakurugenzi wengine watateuliwa na Tume. Mimi naomba marekebisho yafanyike, Rais asimteue Mkurugenzi Mkuu, Mkurugenzi Mkuu aajiriwe na Tume na iwe ni nafasi itakayokuwa wazi, itatangazwa, tuwa-include Watanzania wengine ambao wana uwezo badala ya kila siku kuteua

ambapo itasaidia sana. Aidha, sifa na vigezo vya Mkurugenzi Mkuu ziwe sawa na sifa za Wakurugenzi wale wengine ili kuipa nguvu Tume ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha (9) hakikueleza idadi ya Wakurugenzi, wawe wangapi, ishirini, kumi au watano? Ni vema sheria ikatamka idadi ya Wakurugenzi au Kurugenzi ngapi zitakazoundwa na Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 14 ambacho kinaelezea uteuzi wa Wakaguzi wa Umwagiliaji. Kifungu hiki kama kilivyo, kinaipa mamlaka ya Tume kwa kuzingatia mapendekezo ya Mkurugenzi Mkuu kuteua Wahandisi wa Umwagiliaji ambao watakuwa na mamlaka chini ya sheria. Mapendekezo yangu katika kifungu hiki, Wakuguzi wapatikane kwa njia ya ushindani na sifa ziainishwe, siyo kuteuliwa, kwa sababu kuteuliwa ndiyo watakuwa walewale, katoka huku anateuliwa anakuja huku lakini zikishindanishwa, hapa tutapata wataalam. Tusiogope kushindanisha, ndiyo sehemu tutaweza kupata wataalam kuliko mtu anategemea, au anajipendekeza sehemu anasubiri ateuliwe. Pia waajiriwe kwa mkataba na ujulikane unahuishwa kila baada ya muda gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 16, kifungu hiki kinaelezea zuio dhidi ya wasio na sifa ya kuwa Wakaguzi wa Umwagiliaji. Mimi mapendekezo yangu katika kifungu hiki, kwa sababu kinatoa adhabu kwa mtu ambaye atafanya kazi ya ukaguzi ya umwagiliaji kinyume cha sheria. Wamependekeza kifungo cha miaka miwili, mimi nipendekeze kifungu cha miaka mitano, miaka miwili ni midogo, iwe kati ya miaka mitano na kumi na vilevile kama

ni Mhandisi basi afungiwe shughuli zake za Uhandisi kama ameenda kinyume na sheria kwa muda wa miaka mitano. Kwa sababu kuna watu watajifanya ni Wakaguzi na siyo Wakaguzi au watafanya ukaguzi huo kinyume na sheria.

Tumeona hapa juzi Jeshi la Polisi, kuna *traffic* ambaye amejifanya ni *traffic* kumbe siyo *traffic*. Kwa hiyo, Watanzania ni wabunifu kwenye mambo hayo. Kwa hiyo, kifungu hiki adhabu yake iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 18, upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Utoaji wa ardhi wa aina hii mimi naona utakaribisha migogoro na kwa jinsi ambavyo Waziri hapaswi kumhusisha mtu yeyote, wala mamlaka yoyote isipokuwa Waziri mwenye dhamana ya ardhi na Serikali ya Mitaa kama ilivyoelezwa humu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Mwidau.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana kwa uchambuzi wako makini. Mheshimiwa Charles Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Aloyce Bura.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba ruksa yako kabla sijaanza kuchangia

huu Muswada wa Umwagiliaji, basi nitoe pongezi kwa binadamu na nimshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juma lililokwisha lilikuwa juma zito sana, wako Watanzania walikuwa wanasafiri kwa ndege kutoka Bukoba kuelekea Zanzibar, walipofika usawa wa Mkoa wa Manyara, *engine* zao zikazima. Kwa ustadi Rubani wao, akatua kwenye maji ya Ziwa Manyara. Namshukuru Mwenyezi Mungu lakini nachukua nafasi hii kupongeza wavuvi waliokuwa wanavua kwenye Ziwa Manyara waliweza kuwavua watu wale na kuwafikisha salama katika sehemu ya usalama zaidi. Nawapongeza sana, namshukuru Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, sasa niende kwenye Muswada wetu wa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, alinifuata Mwenyekiti wa Kamati husika akaniambia Mwijage kuna maji mengi kwenu mbona hujasema lolote? Alikuwa na wasiwasi kwamba labda mimi nina msimamo asiouelewa. Nimekuja kutamka msimamo wangu na msimamo wangu ni kwamba naunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina hali ngumu. Katika Jimbo langu au Jimbo letu la Muleba Kaskazini na Kagera kwa ujumla, sasa tungekuwa tumeshaanza kupanda mahindi na maharage siku kumi zilizopita, kimsimu, tuna kalenda zetu, walizitabiri wazee mpaka leo ni jua kali. Ukienda katika maji yote yaliyozunguka Mkoa wetu, maji yanatiririka, ina maana nini, maji yanatiririka na

hamtapanda kwa msimu, kwa hiyo mtapata njaa. Basi kama walivyosema wataalam, shughuli zozote lazima zilindwe na sheria na kama wanavyosema walatino ambacho hakikuandikwa basi hakipo. Naunga mkono sheria itungwe kusudi ituongoze tufanye nini ili tuweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwasaidie au tuchangiane mawazo, hatupingani, tunaelimishana, tuelezane umuhimu wa kumwagilia. Kwa hesabu ambazo hazichanganyi watu, ututendee haki Waziri wa Kilimo, ututendee haki Waziri wa Fedha, mtueleze ni kiasi gani tunatumia kuagiza chakula kama nafaka. Mtusaidie kutueleza na kuwaeleza Watanzania wengine wasichanganywe na majadiliano yetu, tunanunua sukari ambayo inaweza kuzalishwa Kagera, Kilombero na kule *TPC*, tunatumia shilingi ngapi. Kuna mafuta ya mbegu kama alizeti, uwaeleze Watanzania kwa kwamba kwa kumwagilia tutaokoa kiasi gani mbadala, muwaeleze Watanzania waweze kuwaelewa *what are we saving* kusudi watu waelewe, msiwachanganye na hivi Viingereza na Viswahili vya ajabuajabu, wape takwimu, watu wasome takwimu, waelewe kile watakachoweza kuokoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni kwamba kwa kumwagilia, nilivyosoma maandiko ya kumwagilia, kwa kumwagilia na zikihusishwa Wizara zinazohusika, kuna Wizara moja hawahitaji, Wizara ya Uvuvi, Mheshimiwa Jenista amenidokezea kidogo. Kama Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo na Uvuvi zitahusika sawia, ina maana wavuvi tunaweza kuanza kufuga samaki kwenye mabwawa yale, kwenye majaruba yale,



tunakwenda kitu ambacho Wachumi wanaita *economies of scope*, unalima mpunga, unafuga samaki, hatma yake ni kwamba unapunguza gharama za uzalishaji, ina maana mpunga au mchele kitakuwa ni chakula ambacho ni cha bei rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya nazungumza kuwashawishi wenzangu waelewe kwa kuwapa takwimu, ni kwamba itatusaidia sasa Tanzania kuwa chanzo cha chakula cha bei nafuu ambapo tutaweza kuuza kwa nchi zilizotuzunguka na dunia nzima. Maana yake nini? Uzalishaji wa chakula, utaweza kufanya Tanzania itumie chakula kinachozalishwa kwa tija kama zao kubwa linalotupatia pato, tutasahau mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie jambo lingine, wale wanaosema tumechelewa au Muswada huu haufai uondolewe, tumekuwa tukisimangwa, Mchungaji Msigwa amezungumza kwamba Wayahudi wamekuja wakamcheka, tumekuwa tukisimagwa, Ziwa Victoria lipo, watu wanalia njaa kandokando ya Ziwa Victoria. Mkoani kwangu sehemu zote ni maji, watu wamekuwa wakilalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru mnaonipigia makofi, kamanda Silinde, sasa tunataka Muswada upite kusudi tuache kusimangwa, wakati umefika tupitisha Muswada huu tuache kusimangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mawazo ya Wayahudi kwamba tuwape nchi hii, hatutoi nchi hii kwa mtu. Kama wao wanadhani wanajua kufanya kazi, waje watueleze,



watuonyeshe mahesabu, tuwaajiri, wawe wafanyakazi wetu, wazalishe, tuuze nje halafu tuwapatie ujira wao waondoke.

Kwa msembo huo, napenda kuishauri Serikali, kama ambavyo tumefanya kwenye barabara, Wachina walipojenga barabara hawakuzichukua, Wajerumani hawakuchukua barabara zetu, sasa na watakaokuja kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji, wajenge miundombinu, wawafundishe wananchi, waondoke waende zao, wawaachie wananchi kusudi wa-*exploit* zile *opportunity*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwa upande wangu, Bonde la Mto Ngono, linazo hekta 24,000. Sikubaliani na Mbunge aliyependekeza kwamba skimu za umwagiliaji, kwa heshima zako Mheshimiwa Subira nakuheshimu, hatutakubali sisi watu wa Kanda ya Ziwa kwamba umwagiliaji uende *SAGCOT area* sisi tunaletewa chakula, chakula cha kuletewa hakinogi. Mwananchi unalima mwenyewe unakula jasho lako. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka sambamba, mabonde ya Mara, Simuyi, Geita, Mwanza na Kagera yanaanza kulimwa sasa. Waziri unaweza kuona matatizo, Waziri wa Ardhi unaweza kuona matatizo, Waziri wa Fedha unaweza kuwa na matatizo, utushirikishe sisi, tuko tayari tukakope ili mradi tunayokwenda kukopea ina tija. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo nakuja kwenye Muswada huu, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, sheria hii iko *production oriented, it should be market oriented*, uipeleke

kimasoko, uonyeshe kwamba utazalisha kuuza wapi na ndipo napokuambia uzalishe kwa tija kwa gharama ndogo kusudi tuuze nje.

Kwa hiyo, kama utaonyesha hiyo, itatuwezesha sisi watu ambao mnatuatia siyo wa *SAGCOT* kwenda kukopa popote ili mradi tunazalisha kwa tija, hatutaki kupewa chakula. Muleba Kaskazini na Muleba nzima tulipata aibu mwaka juzi, tuliomba chakula, tusingependa kuomba chakula. Yuko Mkuu wa Mkoa pale Muleba, anasema amevaa sura ya kazi, hataki kuona watu wanaomba chakula ili hali maji yapo na maji yanatiririka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikusihi, sisi tungependa ulete wataalam wako, uwaweke kwenye Halmashauri, ucheleweshaji usiwepo na sisi kazi zetu Wabunge ni kuishauri Serikali na kuisimamia. Serikali ikitengeneza mambo yaliyonyooka, mtashauri nini? Kwa hiyo, tutaendelea kuishauri lakini tutataka weledi zaidi kusudi sasa tuweze kwenda katika uzalishaji wenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upungufu umezungumzwa, nadhani yamefika panapohusika, lile la kurekebishwa lirekebishwe kusudi twende mbele. Najua waliotengeneza Muswada huu na waliopitia, wote nawafahamu karibu wengi kwa majina, malaika yeyote hakushiriki, ni binadamu. Upungufu uliopo urekebishwe kusudi twende mbele. Kwa sababu gani? Sisi tunachohitaji, tunahitaji uzalishaji wa tija kwa ajili ya soko la Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye vifungu, mimi sina vifungu vingi, ninaimani na wale waliochambua, kifungu cha 52, ukurasa 87. Ukweli wenyewe na bahati mbaya rafiki yangu Mzee Kilufi hayupo, ametoa mwaliko kwamba niende kwake kujifunza umwagiliaji, Watanzania wengi hawajui hii shughuli ya umwagiliaji. Kuna umuhimu katika ukurasa huu, muongeze kipengele cha kuwashawishi wananchi na kusimamia hii Tume kuhakikisha popote penye fursa, wananchi wanashiriki kwenye shughuli hii.

Namshukuru Mheshimiwa Kilufi popote alipo, amesema watu wa Mbarali hawasubiri Serikali, wanaanza Serikali inawakuta njiani. Kwa hiyo, wanaosubiri waletewe matrekta hapana, matrekta yapo Dar es Salaam, matrekta yako kwenye *google*, matrekta yapo popote, msiisubiri Serikali, anza safari, Serikali iwakute njiani na ndivyo Ilani ya CCM inavyosema wale watakaoanza safari watapewa *lift*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchambua kifungu kimoja cha 52, mimi naomba niishie hapo, lakini nirudi kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuwapongeza wale wavuvi wa Manyara ambao waliwaokoa wale wasafiri walioanguka na ndege. Kama alivyosema Mzee mmoja wa kwetu kwamba *disability is not inability*. Alikuwemo mvuvi mmoja aliyekuwa na mkono mmoja lakini naye alikuwa bigwa katika kuwaokoa wenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sisi tunaunga nawe katika kuwashukuru sana wavuvi hao wa Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Felister Bura atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Mohammed.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pia kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nichangie Muswada ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania hii tunaongezeka kwa kiasi kikubwa cha kutisha, kwa sasa tuko zaidi ya milioni 40 lakini ardhi aliyotupa Mwenyezi Mungu haiongezeki, iko vilevile na miti inakatwa ovyo, misitu inachomwa ovyo na misitu na miti ndiyo inayoleta mvua. Hakuna kinachoweza kutusaidia kutokana na uwingi wetu, kutokana na kuongezeka kwetu, kutokana na kufyeka kwa misitu bila kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi wa Mtanzania, ndiyo ukombozi kwa kutoagiza chakula nje ya nchi. Nimesikia Mbunge mmoja amesema kwamba tunaletewa mchele ulioharibika, tunaletewa kwa sababu hatulimi na tabia ya nchi imebadilika, wakulima hawajui ni muda gani mvua itanyesha, wakulima hawajui muda gani mvua zitaendelea. Kwa hiyo, wanalima kwa kubahatisha lakini bado kuna mito mikubwa ya maji, bado kuna mabonde, kuna maziwa ambayo hayatumiki ipasavyo. Tunataka sasa sheria hii itusaidie kutumia mabonde yetu kuzalisha mazao, itusaidie kulima mazao mengi zaidi bila kuagiza chakula tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya *The Big Result Now* yatatokana na Tume hii katika Wizara hii. Tutaona

matokeo kutokana na Tume hii ya umwagiliaji inayokwenda kuundwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wangu na Mkoa wako ni Mkoa kame, sisi tunapata mvua miezi miwili tu kwa mwaka lakini ndani ya miezi miwili kuna mafuriko kibao. Kuna Kata ya Msagali pale kila siku njia ya reli inasombwa na maji, kila siku yale maji yanapotea hayana matumizi. Kule Kilosa, kila leo, reli inasombwa na maji, maji yanaishia huko hayatumiki kwa sababu hakuna utaratibu wa kutumia maji ya mvua, tunayaachia yanapotea, hayatumiki kuzalisha. Mvua zikianza, wakulima hawawezi kuendelea na kilimo kwa sababu mvua ni nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kilimo cha umwagiliaji kitatusaidia mno. Mheshimiwa Waziri anzia Dodoma, ulishasema unaanzisha skimu ya umwagiliaji kule Furukwa, anza sasa. Baada ya Muswada huu kupita, skimu ile ianze haraka iwezekanavyo kwa sababu itasaidia Wilaya ya Chemba, Wilaya ya Bahi, Wilaya ya Chamwino na Wilaya Dodoma Mjini. Tunakusubiria, anzia Dodoma skimu ya Farukwa. Pale kuna mto mzuri sana, Mto Bububu, haukauki lakini hatuna matumizi nao kwa sababu hatuna skimu ya maji, hatuna skimu yoyote ya umwagiliaji. Kwa hiyo, ukianzisha skimu ya umwagiliaji, ni ukombozi kwetu sisi Wana-Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo Farukwa tu, tuna mabonde mazuri kule Mpwapa, tuna eneo la Msagali wakulima wanalima mpunga pale, wangeweza kulima mazao mengine kama tungekuwa na skimu ya umwagiliaji. Tuna Mto Chenyasungwi pale Msagali, wananchi

wanaweza kulima pale mazao mbalimbali na wakaondokana na umaskini. Tuna eneo la Matomondo kule Mpwapwa, naamini maeneo yale yakitumika vizuri hatuwezi kuomba chakula tena, tutasahau njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna suala la *SAGCOT* kwa Mikoa ya Kusini, siyo kwamba hatutaki, *SAGCOT* iendelee lakini Mikoa ya Kati ambayo ina shida ya chakula itizamwe kwa jicho la huruma zaidi. Kilimo cha umwagiliaji, skimu za umwagiliaji ndiyo ukombozi kwa Watanzania, ndiyo ukombozi kwa wakulima na ndiyo ukombozi kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado wananchi wangu hawa hawana uwezo wa kujenga hizo skimu. Nimeona faraja katika Muswada huu, Sura ya Sita, Ibara ya 29, kuna mambo mazuri yametajwa pale, kama utekelezaji utakwenda ulivyopangwa, ninaamini njaa itakwisha Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo machache ambayo yamezungumzwa katika Ibara ya 29 ambayo yakitekelezwa ipasavyo ni ukombozi kwa wananchi na hata kwa wakulima wadogo. Muswada unasema utawasaidia wananchi, utawahamasisha kuanzisha vyama vya umwagiliaji. Nimeona mafanikio makubwa katika uanzishwaji wa vyama vya umwagiliaji katika Mkoa wangu. Kuna skimu ya umwagiliaji pale Chamwino Ikulu, wananchi wanalima zabibu kwa kuanzisha vyama. Kwa sasa wananchi hawana pa kupeleka zabibu, hatuna soko la zabibu kutokana na kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, tukiendeleza dhana hii ya umwagiliaji, tutafika mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema kuhakikisha kuwa wakulima wote wanamiliki ardhi katika skimu ya umwagiliaji na watakuwa wanachama wa vyama vya umwagiliaji. Ni matumaini makubwa na inawapa neema nzuri wakulima ambao watajiunga kwenye vyama vya umwagiliaji. Pia, inasema kwamba itajenga uwezo wa umwagiliaji katika suala zima la ufuatiliaji na usimamizi. Kuna maeneo skimu zimeanzishwa lakini hawana vyama na wengine hawana utaalam na wengine wameshindwa kutokana na maji kukauka kwa muda mfupi. Skimu hizi zitakapoanza zitawasaidia wakulima ambao ni Watanzania na itatusaidia kuondokana na umaskini ambao unatusumbua kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine nizungumze kidogo katika kifungu cha 9 ambacho kinazungumzia uteuzi wa Wakurugenzi ambao watakuwa katika Tume hii ya Umwagiliaji. Niombe Wakurugenzi hawa wasiteuliwe, washindanishwe. Kila atakayepata nafasi uwezo wake uonekane mapema, siyo ateuliwe tu bila kuonyesha uwezo wake pale ambapo atashindanishwa na wataalam wengine. Wataalam tunao wengi katika vyo vyetu vikuu, washindanishwe tuone uwezo wa mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa kuna utaratibu ambapo Wakurugenzi hawa wanaingia mkataba na mwajiri. Sikuona katika Muswada kwamba Mkurugenzi huyu atakapoteuliwa na akashindwa kuwajibika ipasavyo, itakuwaje? Muswada uonyeshe kwamba atakaposhindwa kabla ya muda wake aachie ngazi, kwa sababu tunaona maeneo mengi shughuli zimekwama kutokana na



wasimamizi wa maeneo husika kutofanya kazi zao kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kifungu cha 14 amezungumzia uteuzi wa Wakaguzi, bado naomba Mheshimiwa Waziri washindanishwe hata hao Wakaguzi ili tuone ufanisi. Tunataka ufanisi sasa, hatutaki longolongo, tunataka ufanisi na hao utakaowaleta Dodoma Mheshimiwa Waziri tutawatembelea kuona kwamba wanafanya kazi kwa ufanisi au hawafanyi kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 21 kinazungumzia ujenzi wa miundombinu. Nachoomba ni kwamba usiwepo ukiritimba katika uombaji wa vibali. Ndiyo maana nimeomba Wakurugenzi washindanishwe. Inawezekana ukawepo ukiritimba kwa wale ambao wangependa kuanzisha skimu za umwagiliaji lakini kama hawa watu watahindanishwa, nadhani ukiritimba hautakuwepo. Ujenzi wa miundombinu na utoaji wa vibali usiwepo na ukiritimba wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba tunategemea ufanisi mkubwa katika uanzishaji wa skimu hizi za umwagiliaji na niombe Serikali yangu kwamba skimu hizi zianzie Dodoma katika eneo la Motomondo kule Mpwapwa ambako tunalima vitunguu vingi sana kwa mwaka mzima lakini hakuna skimu za umwagiliaji. Zitakapokuwepo skimu ya umwagiliaji mimi nadhani tutafanya kazi kubwa sana. Kuna wakulima wa miwa pale kiasi kwamba tungeweza kujengewa kiwanda cha miwa lakini itakapokuwepo skimu ya umwagiliaji tutafanya mambo makubwa sana.



Mheshimiwa Naibu Spika, pia nasisitiza suala la Mto Bububu kule Farkwa maana hii imeshakuwepo kwenye mpango wa Serikali kwamba, Farkwa kuna skimu ya umwagiliaji ambayo hauja-take *off*. Skimu hii ianze sasa ili iwasaidie wakulima wa Bahi ambao wanalima mpunga kwa hali ya juu sana lakini tatizo liliko pale ni maji. Hakuna maji pale Bahi na wakulima wa Bahi wanategemea maji kutoka Farkwa kule Chemba. Wakulima wa Chemba watafaidika kwa sababu wanategemea Mto Bububu kwa ajili ya wakulima wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kusema kwamba naunga mkono hoja hii, naitakia Serikali yangu mema sana katika utekelezaji wa Muswada huu, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Felister Bura. Mheshimiwa Hamad Rashid atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza, niseme tu kwamba mwaka 2009, Serikali ilileta kwenye Bunge hili Sera ya Umwagiliaji leo tunaunda *Commision*. Ukitazama Sera na mpaka tunaunda Tume hii, ni muda mrefu sana. Ni dhahiri tunahitaji vilevile kuangalia kama yale maudhui yaliyoko ndani ya Sera, kama kweli yanaendana na hii sheria ambayo tulipitisha kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni vyema Serikali ikajifunza sasa, pale inapotoa Sera basi na Sheria isichelewe sana. Kwa sababu utekelezaji wa Sera unaweza ukawa na

matatizo kama Sheria haipo kwa sababu Sera haina nguvu ya kisheria lakini Sheria ndiyo inayotoa nguvu ya Sera kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, *level* ya maji duniani kote sasa hivi imeanza kupungua sana. India ambao wanafanya *irrigation*, sasa hivi wanaenda karibu mita 300 chini kutafuta maji. Pakistan watakuwa na tatizo la chakula, India watakuwa na tatizo la chakula, Urusi watakuwa na tatizo la chakula kwa sababu *level* ya maji imepungua *all over the world*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, la kwanza ambalo ningeshauri Serikali ni kuangalia hivi vyanzo vyetu vya maji ni kiasi gani vitaweza ku-*sustain* hii *irrigation scheme* tunayotaka kuifanya. Mimi nafikiri hili ni jambo la kwanza kufanyika ili hatimaye tusije tukapata matatizo, skimu tumezianzisha, halafu maji hayapo. Kama ambavyo tumeona mahali pengine skimu zipo lakini maji hayapo. Kwa hiyo, utafiti wa kwanza ni kutizama haya maji yaliyopo tukiyatumia yatachukua muda gani kuweza ku-*sustain* hiyo *irrigation scheme*. Hilo ni jambo la kwanza ambalo ninaiomba Serikali ifanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne ni kwamba, hii sheria isaidie sana katika kupunguza urasimu. Tumeanzisha *agency* nyingi ili kupunguza urasimu. Leo bado tunaendelea vilevile kuzungumzia watendaji wakuu katika Mikoa. Mimi nakumbuka sera ya Serikali ilikuwa ni kupunguza madaraka pale Mkoani na kuyateremsha chini zaidi kwa sababu unapomweka Afisa Mkoani, mwenye taaluma nzuri ambaye anaweza kuifanya kazi hiyo Wilayani,

mimi sioni sababu kwa nini tuna *Regional Irrigation Officer*, kwa sababu kazi yake yeye ni kuratibu tu. Mnaacha *resources* muhimu unaiweka mahali kazi yake ni kuratibu badala ya kwenda kwenye *field* akasaidia kazi inayotakiwa kufanyika. Kwa hiyo, nashauri nafasi ambayo tumeiweka ya *Regional Irrigation Officer* iondolewe, twende moja kwa moja kwenye *District* ili watu waweze kufanya kazi inayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tano, ni suala la *funding*. Sheria nyingi hapa Bungeni tumezipitisha na tumeshindwa kuzitekeleza kwa sababu hatuna sheria tuliyoipitisha tukasema sheria hii tuliyoipitisha gharama zake za kuitekeleza ni kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka, nafikiri tulikuwa pamoja tulipokwenda Uganda, tukawakuta wenzetu wakipitisha sheria, wanasema sheria hii gharama yake ya utekelezaji ni hii. Kwa hiyo, unajua kabisa kwamba Tume hii unaiunda gharama zake za kuiendesha na gharama za kuitekeleza sheria hii ni kiasi gani, wana-*package* hiyo na nchi nyingine nyingi wanafuata utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri tumefikia wakati huo. Ndiyo maana utaunda Tume hii kesho, utakuja kwenye Bunge hili, utapewa kwanza pesa tu za kufanyia *management*. Mwaka mzima unapita unashughulika tu kuandaa watu na kupanga watu kwa sababu hujajua hiyo sheria utekelezaji wake utagharimu kiasi gani. Mimi nafikiri hili lazima tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha ananisikia, wenzetu wengine wanafanya hivyo, wale Marekani pesa

zao zikitoka zinajua *program* hii fedha yake ni hii na lazima itekelezwe, ikimaliza *program*, fedha imeisha na mambo yameisha. Sasa twende na utaratibu huo, badala ya kuja hivi kila siku na maneno, sheria zipo, taasisi zinaundwa hazina fedha. Mimi nakuhakikishia mwaka ujao kazi yetu kubwa itakuwa ni kupitisha pesa kwa ajili ya Tume hii kufanya kazi kwanza; siyo kwenda kufanya kazi ile tunayoitaka, aah, aah, kujipanga tu, mwaka mzima utapita, kwa sababu hakuna kitu hicho ambacho kimepangwa mapema, naomba hilo nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la sita, katika sheria yetu hii nzuri, naomba vilevile Wizara itusaidie, sisi Tanzania tuna *advantage* kubwa sana ya kuwa wafalme wa kila hali, moja ni kuwa na chakula cha kutosha, lakini lazima tuseme, hivi tunataka tani ngapi za mchele, tunahitaji tani ngapi za mahindi na tunahitaji tani ngapi za kahawa? Ukishajua hiyo idadi unayohitaji na hizo zitaku-*sustain* kwa muda gani, ndiyo unaweza kuelekeza nguvu zako kwenye hicho unachotaka kufanya.

Kadri tunavyokwenda mbele siyo ardhi tuliyonayo yote tutaitumia kwa kilimo. Viwanda vitaongezeka, watu wataongezeka, shule zitaongeka, kwa hiyo, mahitaji ya ardhi yatakuwa makubwa zaidi kuliko hata haya ya kilimo. Kwa hiyo, ni lazima mfanye *demarcation* mapema kujua kwamba katika miaka hamsini inayokuja, tutahitaji hekta fulani ili ku-*sustain* chakula chetu na cha kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo katika hili suala la Rwanda na nani, tungekuwa na *surplus* ya chakula peke yake hapa hakuna mtu ambaye angetuletea jeuri. Leo

Tanzania tukija hapa tunajisifu tuna chakula cha kutosha tuna tani laki moja ya ziada, tani laki moja ya ziada ndiyo *surplus* ya chakula kweli? Aibu!

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tufike mahali tuseme kwamba miaka hii mitano tuzalishe tani milioni tano za mpunga ili pale tulipotoka kwenye tani milioni 11 ziongezeke kutoka hapo ili tuweze kuuza nje na kadhalika. Je, skimu hizo tunazifanya wapi na wapi? Pawe *identified* ili hawa wataalam wachache tulionao, tuwapeleke katika maeneo maalum ambayo tunahakika tutapata hiyo *surplus* tunayohitaji vinginevyo tutazungumza hapa kwa nadharia, wataalam ni wachache, tunataka waende kila mahali matokeo yake hatutapata kitu chochote. Ndiyo maana tumekaa miaka hamsini na hekta laki tano za *irrigation* hazijafika mpaka leo. Naomba suala hilo tuweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la fedha za kuendesha Tume nimelizungumza, lakini napenda vilevile Mheshimiwa Waziri atusaidie katika ukurasa wa 17 wa sheria hii. Naona kuna Wizara zinajumuishwa, lakini Wizara ya Nishati na Madini haimo katika Wizara zile ambayo yenyewe ina maeneo makubwa ya ardhi lakini yenyewe ni watumiaji wakubwa wa maji. Sehemu kubwa ya madini wanatumia maji, maji hayahaya ndiyo mtakayokwenda kugombea kwenye *irrigation*. Sasa usipoitaja katika ule uwiano, nafikiri kutakuwa na tatizo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naona limeachwa ni urasimu. Katika sheria hii hatusemi kwamba mwombaji ambaye ametimiza masharti yote lini atapewa

kibali cha kupewa idhini hiyo na akinyimwa hiyo idhini ya kufanya hivyo, je, huyo aliyemnyima idhini anapata adhabu gani? Kama hatuliweki hili, utaratibu huu wa kawaida utaendelea tu. Watakuja wawekezaji wenye uwezo Watanzania tu, tena siyo wa nje, wamejipanga wenyewe vizuri, atakwenda kuomba kibali, leo atakwenda ofisi hii, kesho atakwenda ofisi hii, matokeo yake mwaka unakwisha hapati kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii naomba kabisa tubadilike sasa ili watu wawajibike. Kama mimi nimetimiza masharti yote, niambiwe ndani ya sheria hii katika muda nitapata idhini ya kutekeleza mradi wangu. Kama hilo halikutamkwa na kama hakunipa hiyo idhini apate adhabu. Sheria zetu zote zimekuwa *silent* katika upande huo, unamwadhibu mtu tu upande mmoja, kwamba asipofanya hivyo atashitakiwa lakini wewe usipotimiza wajibu wako, adhabu yako ni nini? Hili katika kila sheria zetu limekuwa kimya.

Nafikiri sasa imefika wakati, ili tuondokane na huu utaratibu wa *business as usual*, lazima tuseme kwamba, wewe ukitimiza masharti moja, mbili, tatu, nne, tano, upande wa pili nao unahitaji kutimiza masharti hayo na usipotimiza adhabu yake ni hii. Nafikiri kila mmoja atakuwa amewajibika na ataweza kutekeleza hii sheria vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sitakuwa na maneno mengi, niseme Muswada ni mzuri, tuunge mkono lakini tujifunze kwamba wakati mwingine ni vyema tunapotoa Sera na Muswada wakati huo huo uwe unatoka ili vitu viwili hivi viende pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ardhi, maji ni rasilimali muhimu sana. Bila kuzipanga vizuri, migogoro ya ardhi itaendelea, wafugaji watalalamika, wavuvi watalalamika, wachimba madini watalalamika, suala hili ni lazima liwe na *coordination* nzuri sana na sheria hii inahitaji kutamka hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Mheshimiwa Mendrad Kigola.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kuishukuru Serikali kwa kuleta Muswada mzuri ambao unaokoa maisha ya Watanzania wengi ambao wanategemea kilimo ili kuweza kuboresha uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa leo mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja. Naunga mkono kwa asilimia mia moja kwa sababu siku zote mimi kichwani nilikuwa nafikiri, hivi tutaboreshaje kilimo ambacho Watanzania wengi sana wanakitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Serikali ilikuwa na mkakati mmoja ambao ulikuwa mzuri kwa kuboresha mazingira. Tunajua kabisa watu wa vijijini ni watu wa kawaida ambao wanategemea kilimo na tunapoongelea



kilimo cha umwagiliaji, nadhani tafsiri yake labda watu wanafikiri tunamwagilia mpunga tu, siyo kumwagilia mpunga tu. Tunaposema kilimo cha umwagiliaji, maana yake tutamwagilia mazao ya biashara na mazao ya chakula. Tukisema mazao ya chakula maana yake watu watamwagilia mahindi, mpunga na mbogamboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikataza kulima kwenye mabonde, sasa tulikuwa tunafikiria, kama watu walikuwa wanalima kwenye mabonde, akinamama walikuwa wanaweza kusomesha watoto wao kwa ajili ya kuuza mbonga ambayo inatoka kwenye mabonde na sasa hivi tumeshakataza kwamba wasilime kwenye mabonde ili kuhifadhi vyanzo vya maji na hiyo ni sahihi kabisa na mimi nakubaliana, lakini tulikuwa hatuna mbadala, kwamba unawafukuza wasilime kule, unawapeleka wapi? Serikali naishukuru kwa kuleta mkakati wa kuwa na sheria ambayo itakuwa inashughulikia masuala ya umwagiliaji.

Kwa hiyo, nina imani kabisa kwamba hii sheria itasaidia sana wakulima kule vijijini, watamwagilia mboga zao, mahindi, tutaondokana na tatizo hili la njaa. Kuna mmoja amesema kwamba kwa Tanzania tukisema tuna njaa, kweli ni aibu, hata mimi nakubaliana naye ni aibu. Kwa sababu sisi tuna mabonde mengi sana, tuna maziwa mengi sana, tuna mito mingi sana, ambayo tunaweza tukamwagilia na tukauza chakula ambacho kinazidi tukapeleka nje yaani tuwe tuna chakula cha kutosheleza.

Kuna Mikoa mingine kweli tunajua kabisa hakuna mabonde labda Mikoa mikame, lakini kuna Mikoa mingine ina neema ya mabonde, kuna maziwa, kuna kila kitu, lakini



sasa tukiwa na mpango wa pamoja wa Serikali, tukawa na kilimo cha umwagiliaji, basi tutatatua tatizo la njaa. Hilo mimi nakubaliana kabisa, ni hoja nzuri kabisa na mimi nawaomba Wabunge wenzangu tukubaliane na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala moja ambalo limeongelewa na nimelisoma kwenye sheria, ambalo na-*doubt* kidogo, kwa sababu Tume kama itachukua ardhi, naishauri Serikali, Tume isichukue ardhi isipokuwa Tume itoe elimu kwa wananchi juu ya kilimo cha umwagiliaji. Nasema hivyo kwa sababu naogopa isije ikarudi ile ya madaraka Mikoani, madaraka Mikoani walichukua ardhi, wanasema hapa tuna *project* fulani, sasa ile ndiyo inatusumbua mpaka leo, kwa sababu walichukua ardhi bila kuwashirikisha vizuri wananchi, isije tena likatokea tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mfumo unapokuja, mimi naishauri Serikali kwamba Tume hii ni nzuri kwa kufanya ufuatiliaji na ili tufanye vizuri, lazima tuwe na Tume ya ufuatiliaji. Tume iende ishauri wananchi na kutoa elimu kuhusu kilimo cha umwagiliaji, kwa sababu sisi Watanzania walio wengi, kilimo cha umwagiliaji wanafikiria labda ni kilimo kile cha mifereji tu, siyo kilimo cha mifereji tu. Kuna kilimo cha umwagiliaji unaweza ukamwagilia hata kwa njia ya mabomba, sasa pale inahitaji elimu kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja nitoe mfano mzuri, kule kwangu Mfindi, kuna Mashirika yale ya *Unilever Company*, *MTC*, wale wanamwagilia chai. Ukienda kule, kilimo kinafanyika kwa ufanisi na wanafanya kazi nzuri sana, mazao yanaongezeka kwa ajili ya kumwagilia. Sasa mimi nilikuwa nauliza, je, kama tunamwagilia chai, kwa nini

tusiweze kumwagilia hata mahindi na mboga kwa njia ya kutumia mabomba, ndiyo njia za kisasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naishauri Serikali, kwa mfumo huo, kama kweli Tume hii itafanya kazi vizuri, ikajielekeza kwa wananchi, ikatoa yale maeneo kwa wananchi, sawa ardhi ni ya Serikali lakini wanamiliki wanakijiji. Naona ule mpango wa wananchi kuwashirikisha kumiliki ardhi ile, tusiupangue kwa kupeleka chombo kingine, wananchi wataanza ku-*doubt*, watajua watachukuliwa ardhi yao. Sasa hivi kuna mgongano mkubwa sana wa ardhi kati ya wananchi na Serikali, kuna maeneo mengine yamechukuliwa bila kushirikisha wananchi, sasa hili ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ijikite sana kuwaelimisha wananchi, kwanza, kutumia vizuri ardhi. Suala la pili, Serikali ijielekeze kutumia vizuri kilimo cha umwagiliaji, hii itatusaidia sana. Tukisema tunaikataa sheria ambayo inakuja kutusaidia na wananchi sasa hivi tayari tumeshawaondoa kule mabondeni, inakuja kuleta shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna mgongano kati ya wafugaji na wakulima. Kuna sehemu nyingine wafugaji wanahamia, kuna sehemu nyingine wafugaji wapo na wakulima wapo, lakini tutenge maeneo kwamba haya maeneo yanafaa kwa kilimo, haya yanafaa kwa ufugaji, hii itatusaidia sana kuondoa migogoro ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri mimi kule kwangu sina wafugaji, ila ambacho nataka niseme kwangu kule wananchi wale wanafanya kazi nzuri sana, wanalima. Mimi kwangu kule ni wakulima wote. Kuna mito mingi sana, kama Serikali itatoa elimu, kwa mfano sisi tuna Mto Ruaha, ukiangalia kwa mfano kule Idumlabani, kule kuna ardhi nzuri sana na wananchi wanapenda sana kulima lakini tuna uhaba wa mvua, kama tutaweka njia mbadala kwamba waweze kumwagilia, basi Kata ile nzima ya Itandula na Idunda, wote watumia Mto Ruaha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda pale Malangali, kuna mito, ukienda Mtambula kuna mito, hapa Nyororo kuna bwawa kubwa la miaka mingi, halitumiki, lipo tu pale. Kama tukisema kwamba tunapeleka njia ya kisasa, hii ni njia ya kisasa ya kitaalam, kwamba watu sasa lile bwawa badala ya kukaa tu, tulitumie kwa umwagiliaji, litatusaidia wananchi wa Nyororo pale, watalima vizuri na watapata mazao. Yale mazao watakayopata siyo kwamba itakuwa faida ya Kijiji cha Nyororo peke yake au Kata ya Nyororo, ile italisha Tanzania nzima kwa sababu kuna maeneo makubwa. Kuna maeneo mengine tunapanda miti lakini yanafaa kwa kilimo, tungeyatumia kwa kilimo ingesaidia sana, naishukuru Serikali kwa kuleta mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna bonde kubwa sana la Mgololo, ni zuri sana na namshukuru Waziri Mkuu, nadhani siku chache ataenda kufungua kilimo cha umwagiliaji na sisi kule kama alivyoongea Mbunge mwenzangu, tulishaanza mpango tayari, kwa hiyo, sisi sheria inatukuta. Sisi vitu

vinavyoleta manufaa kwa wananchi huwa hatusubiri sheria, siyo kitu cha hasara hicho, sisi tunakwenda mbele.

Sisi pale Mgololo tayari kuna bonde kubwa, naishukuru Serikali imejenga ile miundombinu vizuri sana na ime-cost karibu *billions*. Mimi naishukuru sana, sasa ni utekelezaji, sheria inatukuta sisi tumeshaanza. Wewe utakuwa unapinga, unalalamika na njaa, sisi hatutalalamika na njaa. Wananchi wa bonde la Mgololo nawashauri, lile bonde tulitumie vizuri. Hatuhitaji sisi kwenye bonde letu mwekezaji, tunawekeza sisi wakulima wenyewe, tuna mikono, tuna akili, tuna masikio, tuna macho na tunaona, sasa kwa nini tuanze kusema mwekezaji na tuna nguvu ya kufanya kazi, sisi tunataka Serikali itu-*support* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mgololo, naomba sana, hizi Idara ziungane. Kwa mfano, kuna hii Idara ya Ujenzi, ya Ardhi, ya Nishati, inabidi ziungane. Kwa mfano, pale sisi tuna tatizo moja kubwa la umeme, kwa sababu huwezi ukaendesha kilimo cha umwagiliaji wakati umeme hakuna.

Sisi tunahitaji tujenge viwanda vya kukoboa lakini hakuna umeme pale. Sasa wewe wa kilimo cha umwagiliaji lazima u-*integrate* na wenzako ili tuweze kufanya vitu kwa ufanisi. Pale umeme upo lakini umepita juu watu pale Lugolofu wanaangalia nguzo. Sasa kwa sababu kilimo tumeanza, nadhani mwaka huu mtashirikiana pamoja tuweze kuweka umeme pale na watu waanze kujenga viwanda pale, tunataka viwanda vianze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu hiki kilimo cha umwagiliaji, lazima kuwe kuna miundombinu ambayo

imekaa vizuri. Hizi barabara za vijijini, lazima tuhakikishe kwamba zinakwenda vizuri kwa sababu unaweza ukalima, halafu ukashindwa kusafirisha. Unaweza ukawa na mazao mengi sana kwenye magodauni lakini kama huna barabara utasafirishaje, soko utatafutaje na soko linategemea kuwa na barabara imara. Mimi naiomba Serikali, tuiseme umwagiliaji, umwagiliaji, lazima tuhakikishe kwamba miundombinu vijijini inakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Waziri wa Ujenzi, barabara katika Mikoa amejihidi sana, katika Mikoa zinapitika, tena kwa kiwango cha lami. Sasa kiwango cha lami siyo Mikoa tu, wala siyo Wilaya tu, tunalenga hata Vijijini, kwa sababu tunataka kuzalisha zaidi na wakulima sasa watazalisha. Tukienda kwenye nchi za wenzetu, bahati nzuri Wabunge tuna bahati ya kwenda katika nchi mbalimbali, tunaona hizi barabara siyo *issue*, zinapita hata kwenye Vijiji tu za lami, ni kitu cha kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuzaje uchumi kama huweki kilimo cha umwagiliaji? Kilimo cha umwagiliaji ndicho kitatufanya tuzalishe zaidi, Serikali ipate mapato zaidi na ikipata mapato mengi zaidi maana yake itajenga miundombinu ikae vizuri zaidi. Sasa wewe ukisema unapinga hii, utakuwa unapinga maendeleo, mimi nashangaa unapinga maendeleo, hakuna kupinga maendeleo, maendeleo ni yanakwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwenye Jimbo langu tumeshaanza kilimo cha umwagiliaji, namshukuru sana Waziri wa Kilimo na bahati nzuri yuko *fit*, sisi tulishaanza na sheria inatufuata mgongoni. Sasa wewe unapinga sisi

tunaendelea, sasa sijui kitatokea kitu gani, kwa sababu sisi ukituambia ni kupinga, hatutakubali. Sisi tunakwenda mbele, hatuwezi kuacha mito inakaa bure na binadamu tunaangalia tu, tunatumia akili pale, tunaiacha tu, haiwezekani. Sisi tunataka *support* na tumesema kwamba sasa tunataka tuweke kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala ya matrekta, nakubaliana kabisa, matrekta yako kila sehemu lakini wananchi wengine wameshaungana kwenye vikundi, walishaandikisha majina, matrekta mpaka leo hawajapata! Naiomba Serikali, kama kuna matrekta sehemu, basi yaje, wananchi wanahitaji matreka yale ya mkopo. Kwa mfano, kilimo cha umwagiliaji, mtu hawezi kulima heka moja, mbili, tunataka watu walime zaidi ya heka kumi, ndiyo tunasema wakulima wanalima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi kwangu ukienda Idete kule wapo wakulima wengi sana, wananchi wote wa Idete wanategemea kilimo na ni bonde zuri na pale hatuhitaji mwekezaji, wanalima wenyewe. Wale watu wanahitaji matrekta, hawana matrekta pale Idete. Mimi hata wakati ule wa uchaguzi niliwaambia kwamba hili bonde hakuna tofauti na Ulaya. Pamekaa vizuri lakini kama Waziri ukienda pale Idete, ukatembelea pale, ukaangalia kilimo cha pale, watu wanatumia ng'ombe, wanatumia majembe, wanalima sehemu ndogo sana.

Wale watu wa Idete na wale wa Holo pale, wakipelekewa hata matrekta mawili, wakafanya kilimo cha umwagiliaji, basi kile chakula tuta-*supply* sehemu nyingi. Hata watu wa Morogoro hawa wanalalamika wanasema

hawana chakula, watakuja kuchukua kwangu, hakuna shida, sisi tunawakaribisha tu. Hata watu wa Mtwara hapa, tumeona siku moja wanalalamika hawana chakula, sisi mtuwezeshe, mtoe michango kwa Wilaya ya Mfindi, kwa Jimbo langu la Mfindi Kusini, sisi tunaweza tuka-*supply* chakula cha kutosha, lakini tupate *support* kutoka Serikalini. Kama Serikali haitatoa *support* maana yake tunalima kile kilimo cha ubabaishaji ambacho hakina tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu umekuja Muswada huu ambao tunaupitisha leo, naomba ndugu zangu, Tanzania hii tuna maeneo mengi sana yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji lakini kinachotakiwa ni *creativity*, yaani kufikiri. Tusifikiri upande mmoja tu, kusema labda imekuja haraka, maendeleo yanataka harakaharaka, hayataki kusinzia. Mambo ya uvivuuvivu, watu hawafanyi kazi, hawataki kulima, wengine hawajawahi kuona hata shamba. Hapa kuna watu wengine hawajawahi kulima hata siku moja halafu wanapingapinga kwa sababu hawajawahi kulima. Hebu mtuachie sisi tunaolima tulime mashamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli kuna watu wengine kazi yao ni kuzungukazunguka tu, hamna kitu chochote. Ukimwambia una heka ngapi, hata heka moja hana, sasa unafikiri atapitisha Muswada hapa! Ukienda nyumbani kwake yeye hata heka moja hana, atapitisha wapi? Hebu mtuachie sisi tunaolima, Serikali itutengee bajeti ya kutosha tuweze kumwagilia. Bajeti inayokuja, Waziri wa Kilimo, mimi nitakuwa mbele kuhakikisha kwamba tunaongezewa fedha yaani bajeti inakuwa kubwa kwenye Wizara hii kwa sababu imelenga wananchi. (*Makofi*)



Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kuna maeneo mengi sana, tunasema asilimia 23 tu inatumika, kuna asilimia kadhaa ambayo ni kubwa iko bure, haiwezekani! Sisi tunashindwa kuwa na viwanda, viwanda vya mazao ndiyo vitatukomboa katika nchi hii. Sisi nchi yetu hatutengenezi magari, wapi tunatengeneza magari, tunashindwa hata viwanda vidogovidogo, hata vya viberiti tu hatuna, sasa tunapata hii tija ya kusema tuwe na viwanda vya kusindika chakula, tunaanza kupinga hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wananchi wengi sasa hivi wameanzisha viwanda binafsi vya kusaga unga, wameanza ku-*supply* unga, wenyewe, bila *supports* ya Serikali, wanasaga unga tayari, wanategemea wakulima. Watu wanafikiria labda biashara ya mahindi ni kuuza mahindi, unaweza ukauza mahindi, ukalima, ukasaga unga uka-*supply* kwa wananchi. Tunaweza tukafanya *international marketing*, tukauza unga nje, hii inasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri hata hapa katika Mkoa wako wa Dodoma wanalima sana alizeti. Hata kwangu kule Mtabula mpaka kule Idumlabani na watu wa lharanza wanalima sana alizeti. Sasa kama watamwagilia ile alizeti maana yake viwanda vitaongezeka, vitu vinaenda mbadala, unaongeza kilimo, unaongeza viwanda, unapata masoko nje, unaongeza pato la Taifa. Utaongezaje pato la Taifa unasinziasinzia tu, haiwezekani, huwezi ukaongeza pato la Taifa, lazima tufanye kazi na kazi sisi sehemu kubwa ni kilimo.



Mheshimiwa Naibu Spika, kila kitu tunasema wawekezaji, kwenye kilimo tulime sisi Watanzania. Hatuwezi kuwa na watu wavivu, wanakaa tu, haiwezekani! Sisi lazima tufanye kazi kwa nguvu zote na kwa kutumia akili na lazima tuuze kwenye masoko ya nje. Tunakwenda nje, wenzetu wanauza kwenye masoko ya nje, sisi hatuna *product* hata moja kwenye masoko ya nje. Hatupeleki, tunakwenda tunang'aang'aa tu, lazima tupeleke mazao kule nje na tulime kilimo bora. Hiki kinaitwa kilimo bora, maana yake kina mazao yale yanajitosheleza, *quality* ile inakuwa nzuri. Sasa wewe unalima mahindi ambayo yamenyaukanyauka tu hata mvua hayajakomaa vizuri, mhindi utapeleka wapi, utamuuzia nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, Watanzania tufanye kazi, Waziri wangu fanya kazi, nakukaribisha Jimbo la Mfindi Kusini, nitakutembeze mito yote, sisi tatalima. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mendrad L. Kigola, ahsante sana.

Tutaendelea na mjadala jioni na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Selemani S. Jafo na Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na Mheshimiwa Luhaga Mpina wajiandae.

Kwa hatua hii, naomba sasa nitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 6.50 Mchana Bunge lilisitishwa  
Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kikao chetu, na hoja iliyoko mbele yetu ni Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji wa Mwaka 2013 (*The National Irrigation Bill, 2013*).

Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Naibu Spika, anasitisha shughuli leo saa saba mchana, alisema mchangiaji wetu wa kwanza mara tutakaporudi Ukumbini atakuwa Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, atafuatiwa na Mheshimiwa Asaa Othman Hamad.

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. SELEMANI SAID JAFO, MEMBER OF PARLIAMENT FOR KISARAWA CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE NATIONAL IRRIGATION ACT, 2013"**

---

*[Made under Standing Order 86(9) & (11)]*

---

A Bill entitled "The National Irrigation Act, 2013" is amended in Clause 16 as renumbered, by deleting words "the holder of such land shall be entitled to compensation in accordance with the relevant land law or as may be

agreed upon” appearing in sub-clause (5) and substituting for them the following new words:

“the holder or holders of such land shall be entitled to be shareholder or shareholders to any project which shall be developed in such land as may be agreed upon”.

Dodoma

Hon. Selemani Said Jafo (MP.)

30<sup>th</sup> August, 2013

**KISARAWA CONSTITUENCY**

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa sababu mchana wa leo nami nimekuwa mchangiaji wa kwanza kufungua mjadala huu wenye masilahi mapana sana kwa Taifa letu hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ningelipenda kuwasihi Wabunge wenzangu, tunapokuwa katika suala zima la mjadala wa Kitaifa, tuna jambo la msingi sana tuweze kulisimamia. Toka jana ninasikiliza michango mbalimbali katika Bunge letu hili, lakini tukirejea miezi michache iliyopita, ninakumbuka siku tulipokuwa tukijadili Bajeti ya Wizara ya Kilimo, ndugu yangu Mheshimiwa Kabwe Zitto, alitaka kutoa shilingi hapa, kwa sababu ya jambo kubwa kwamba, kutoa ruzuku ya pembejeo kwenda katika suala zima la umwagiliaji. Hii maana yake nini? Maana yake Umwagiliaji ndiyo ajenda ya Taifa letu hili.

Kama tunataka tutoke hapa tulipo katika hali hii ya uchumi tuliyonayo, ni lazima tuhakikishe tunasimama katika suala zima la umwagiliaji. Ndiyo maana toka jana nimekuwa nikisikiliza nikiona watu wengine wakiibeza sheria hii, ninapata huzuni kidogo na ndiyo maana siku zote huwa nina-*refer* ule usemi wangu wa Kizaramo unaosema: "*Zilongwa mbali, zitendwa mbali.*"

Kwamba, leo hii watu mnataka umwagiliaji, sheria inakuja watu hamtaki; mnataka nini sasa! Maana Watanzania walioko nje watatushangaa sana, siku zote tunapojadili Bajeti ya Kilimo hapa, tunasema kwamba, kilimo hakiwezi kwenda bila umwagiliaji. Sheria inakuja ya kuhakikisha suala la umwagiliaji linasimamiwa, watu wanasema hatutaki. Ndiyo maana ninasema: "*Zilongwa mbali, zitendwa mbali.*" Kwamba, lile wanalosema tofauti, unataka utekeleze vitu viwili tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tuelewe, sisi wote tulikubaliana kwa pamoja hapa kutengeneza Mpango wa Miaka Mitano wa Taifa letu hili. Tulisema kwamba, tunataka tufikie Tanzania iwe nchi ya uchumi wa kati. Hatuwezi kufika katika nchi yenye uchumi wa kati kama kilimo hakitapanda kwa asilimia sita. Sasa hivi kilimo chetu kimeenda na tuko asilimia 4.2. Asilimia 4.2 maana yake hatujafika katika asilimia sita ambayo tunalenga kama Taifa. Tutafikaje katika asilimia sita; maana yake ni lazima tuhakikishe tunafanya *investment* ya kutosha katika suala la umwagiliaji. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Bunge letu linapokuja na Sheria ya Umwagiliaji, ninasema kwamba, Waheshimiwa Wabunge,

japokuwa tuna ushabiki, lakini tunaposema katika ajenda ya kumsaidia Mtanzania, lazima tusimame pamoja kama Watanzania. Ninaomba niwaambie, Watanzania tuna kila sababu ya kusimama imara hivi sasa; tuache hizi tofauti zetu za kisiasa na tuangalie Taifa letu linakwenda wapi mbele. Tuangalie nchi za wenzetu sasa hivi kuna kitu gani kinachoendelea, Watanzania tunakiwa tujifunze kila kitu.

Katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, magazeti hata juzi watu wanaona. Jibu pekee ni kwamba Watanzania tusimame kuhakikisha tunaupeleka uchumi wetu mbele. Hatuwezi kuupeleka uchumi wetu mbele mpaka tuhakikishe kwamba, tuna-*invest* vizuri sana katika kilimo. Tunajua katika nchi zote, soko kubwa sana, mahitaji makubwa sana ya kilimo yanapatikana Tanzania kwa sababu tuna ardhi ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umwagiliaji halina mjadala, kwa sababu Wataalam wa Idara ya Hali ya Hewa wanasema kwa mfano, katika Ukanda wangu wa Pwani, tulikuwa tukipokea ujazo wa mvua karibu milimita 1,580 kwa mwaka. Ndani ya miaka kumi hii imeshuka tunapata milimita 760 kwa mwaka. Ina maana waliokuwa wanatarajia kuvuna katika kilimo cha kutumia mvua hivi sasa jambo hili limekuwa gumu kweli. Kwa hiyo, jibu mwafaka ni jinsi gani tunajikita katika suala la kilimo cha umwagiliaji. Wengine wanauliza kwa nini kulikuwa na Idara na sasa hivi ianzishwe Tume?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema, ukiangalia tunachoenda kukifanya kama Taifa, ndiyo maana ninasema kuhusiana na hilo tusimame vizuri kwa pamoja.

Idara ilikuwa haiwezi kuingia mkataba wa kutafuta fedha kwa ajili ya umwagiliaji; ni nani anayebisha hapa? Ukiangalia Muswada wetu huu ambao unakwenda kuwa Sheria, inaipa fursa Tume, kuhakikisha inaingia kutafuta jinsi gani itaweza kupata fedha kwa ajili ya suala zima la umwagiliaji Tanzania. Kinachotakiwa ni jinsi gani wataalam wetu wako *committed* kuhakikisha Taifa hili linaendelea katika suala zima la umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hayo kama utangulizi kwamba, kama Watanzania, tunaposema umwagiliaji ni jambo lisilohitaji mjadala mpana au ni jambo lisilohitaji mjadala mpana kwa ajili ya ubishi. Linahitaji mjadala mpana kwa ajili ya kuangalia ni vipi Taifa letu tutalipeleka mbele. Wakulima wetu hivi sasa wako katika mazingira magumu.

Ukiangalia Muswada, watu wengine wanafahamu, kuna miundombinu ya umwagiliaji usimamizi wake umekuwa mbovu kweli kweli, kila mtu anajua hilo. Sheria hii inatuonesha kwamba, miundombinu ambayo itakuwa imetelekezwa, Tume itakuwa na mamlaka ya kuweza kuisimamia, kuitoa na kuirekebisha, ilimradi kuleta masilahi kwa Watanzania. Hili jambo ni lazima tulione.

Leo hii tunajua tuna Halmashauri zetu; lakini katika Halmashari kuna skimu ngapi zilizoshindwa kufanya kazi vizuri kwa sababu hakuna ile *commitment* ya usimamizi wa karibu? Katika hili nina imani sana, kama watu wataochaguliwa katika Tume watakuwa na uzalendo wa kutosha, tutahakikisha Taifa letu linaenda mbele kuhakikisha

tunakikuza kilimo chetu mpaka kufikia katika ukuaji wa asilimia sita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Pwani, ninyi mnajua Mkoa wa Pwani ndiyo ingilio la mito mingi sana; tuna Mto Rufiji, tunao Mto Ruvu na tuna Mto Wami. Sheria hii tuna imani kwamba, utekelezaji wake mzuri utawanufaisha Wanapwani hata kule kwangu Kisarawe na kwa ndugu yangu Mheshimiwa Malima. Kinachotakiwa ni kwa jinsi gani hii Sheria itaweza kusimamiwa. Tatizo kubwa ni kwamba, wakati mwingine kuna uzembe katika usimamiaji.

Nilivyofuatilia hii Sheria, kile kipengele cha sita kinachohusu uteuzi wa Bodi ya Wakurugenzi; Mheshimiwa Waziri kama utaridhia ni kwamba, badala ya kuwa na watu kumi katika Bodi ya Wakurugenzi, ikiwezekana muweke watu 13 na watu watatu watoke katika *Private Sectors*. Kwa mfano, kuna ndugu zetu wa *ANSAP*, kuna Taasisi mbalimbali ambazo ziko huko nje, badala ya kuchaguana katika milolongo ya Serikali peke yake, inawezekana tukapata vichwa vilivyopo nje ya mfumo wa Kiserikali, ambavyo vitaweza kusaidia jinsi gani hii Bodi inaweza kusimamia vizuri. Ndiyo maana katika hii *amendment* kama Mheshimwa Waziri ungelikubali, ungehakikisha kwamba, kuna watu watatu wanapatikana katika hiyo Bodi katika *competitive ways*. Kwamba, wafanyiwe *interview* watu ambao ni *qualified*, wakiingia pale wataweza ku-*challenge* vilevile, kuhakikisha Bodi inasimamiwa vizuri.

Ndugu zangu, jambo lingine tulilokuwa nalo zaidi ni la Mheshimiwa Waziri. Mara nyingi sana Wataalam wetu wengine wamekuwa wazembe katika kusimamia, wengine

wanasubiri hii Sheria ipite wapate ulaji kwa ajili ya kuweza kuishi. Hatutengenezi sheria kwa ajili ya watu kwenda kuishi hapa. Ninaomba sana, utaratibu wa kuchaguana kwa kujuana na undugu, Serikali haiwezi ikaenda hivyo. Nina imani Wizara yako haina hilo, lakini ninaomba lisimamiwe hili, tuwachague watu wenye uchungu na Taifa letu hili. Kuna wakati mwingine, baadhi ya watu wanasubiri tu wawe *CEO* wa Tume kama hii na kufanya sherehe kubwa.

Tunataka watu ambao wanapimika ndani ya miaka mitatu wamefanya nini katika suala zima la umwagiliaji na wakishindwa basi katika Kamati ya Kilimo, ikiwezekana hiyo Tume ifanye mabadiliko makubwa. Hatuwezi kuwaweka watu katika madawati wanatafuta mshahara tu. Bahati nzuri sana, Sheria hii inaelekeza tunataka watu ambao wanaweza kufanya *resource mobilization* kutafuta fedha.

Kwa hiyo, hata hawa ambao watakwenda kuchaguliwa ni lazima wawe na uwezo wa *resource mobilization*, siyo kuchukua watu ambao watakaa maofisini tu wanapoteza muda bure. Taifa hili linataka sehemu ya kwenda. Tunazungumza haya kwa uchungu kwa sababu Taifa letu linatakiwa liende tunakokusudia katika uchumi wa mbele.

Suala lingine ni upatikanaji wa vibali. Nimeona katika suala zima la upatikanaji wa vibali mlolongo utakuwa mkubwa sana. Ninaomba sana Sheria hii, ikiwezekana katika suala la utaratibu wa kanuni, tuangalie ni jinsi gani vile vibali visije vikatupeleka kwenye *bureaucracy* watu wakashindwa kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji; maana naona utaratibu wa kupata kibali cha umwagiliaji,



mlolongo wake ni mrefu sana. Ninaomba tuliangalie hilo kwa kina. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo ningelipenda kulizungumzia ni suala zima utwaaji wa ardhi. Kipengele Na.17 na 18 vimesema kwamba, Waziri kwa kupendekeza eneo fulani ambalo linaweza likafaa kwa umwagiliaji, eneo hilo linaweza likatwaliwa. Mimi sina shaka katika hilo, lakini nina shaka katika suala zima la matumizi ya ardhi.

Katika maeneo haya; kwa mfano, mimi ni mwathirika pale kwangu Kisarawe, tunayo maeneo ya ardhi nzuri, lakini kwa bahati mbaya kunaweza kukatokea Watendaji wabovu kiasi kwamba, wakaamua Wananchi fulani wakauzwa, eneo lile likanadiwa katika gazeti, watu wale wakapewa amri ya kuondoka. Tuwafikirie watu wale sasa hivi wanalima, hapo baadaye wakiondoelewa watalima wapi? *(Makofi)*

Hii ni changamoto kubwa, lazima tuliangalie vizuri. Haiwezekani wakati mwingine Waziri umekaa tu unatangaza katika gazeti kwamba agizo fulani kwa mfano kule kwangu Kimaramisale; Kimaramisale ninaitwaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, bila kusema kwamba, Wananchi wa pale utawawezesha vipi katika suala zima kwamba, wao ndiyo wawe *part and parcel* ya huo umwagiliaji. Mimi imani yangu kubwa ni kwamba, watu watakaokutwa katika maeneo hayo, wapewe kipaumbele wawe miongoni mwa *share holder* wa hicho kilimo cha umwagiliaji kinachofanyika katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimwia Mwenyekiti, tumechoka kuzungumzia migogoro ya ardhi na kama sheria hii haitasimamiwa vizuri, maana yake tutaenda kukuza migogoro mingine ya ardhi. Kitu kikubwa, kuwe na *commitment* ya wafanyakazi.

Mheshimwia Mwenyekiti, mimi nimefarijika sana, suala zima la umwagiliaji limekwenda mpaka katika Halmashauri za Wilaya. Sasa nina imani kwamba, hapa tutapata vijana wazuri.

Vilevile kuna jambo moja jana limenishitua kweli; kuna watu wanasema hapa sasa Tume hii itakwenda kuwaongeza watu kuajiriwa. Jamani, mmesema vijana wamesoma wako mitaaani hawana ajira, sasa kama kuna vijana waliomaliza *SUA* pale *engineering* mambo ya kilimo, wataajiriwa kuhakikisha wanasimamia umwagiliaji, hamtaki; ninyi mnazungumzia vijana gani ambao mnataka muwaajiri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema; "*Zilongwa mbali, zitendwa mbali.*" Tunao wasomi waliomaliza *SUA*, tunao wasomi waliomaliza kule Ilonga, wame-*qualify*, tunaweza tukawapeleka katika ngazi zetu za Wilaya, wakaajiriwa wakasimamia umwagiliaji; unasema utaongeza wafanyakazi! Tunachotakiwa ni kuongeza *capacity operation mobilization*, kuongeza uchumi katika hii Tume, kuhakikisha Tume inapata uwezo wa kutafuta fedha kwa mujibu wa sheria iliyopewa, kwa sababu tumesema inaweza ku-*raise* mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali. Tuna imani kwamba, wataochaguliwa wataweza kusimamia hilo, lakini kusema itaongeza idadi ya watu, maana yake ndiyo maana wamesoma lazima

waajiriwe katika Serikali, lazima waende kufanya hiyo kazi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kwa mfano, ninao vijana wangu wametoka pale Ilonga, wako mtaani wanatafuta kazi. Tuliwasomesha sisi wenyewe Kisarawe. Ninao vijana wangu wanaotafuta kazi, lakini wamesomea kilimo. Kama mtu amesomea umwagiliaji, anasikia kuna Tume imeanzishwa na yeye baadaye ataajiriwa atafanya kazi, wewe unasema kwamba tutaongeza wafanyakazi. Je, wale watu ambao unawasomesha unataka uwapeleke wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Tanzania, kwa mujibu wa Sheria hii, kitu kikubwa sana jinsi gani tutafanya kwenda kusimamia Sheria hii. Tujifunze, sisi Tanzania tuna nafasi kubwa sana ya kufanya mabadiliko mabubwa sana. Hata upande wa dini unakwambia kwamba, ndugu yetu Yusufu alipokuwa ametoswa katika kisima na alipochukuliwa na wale wafanyabiashara, alipokwenda katika nchi fulani, akawa yeye ndiye mmiliki mkubwa wa suala zima na watu wanaotafuta chakula walienda kumfuata pale. Maana yake ni nini? Tukizalisha kilimo, tukifanya kilimo cha umwagiliaji kiwe kikubwa ina maana watu wengi hata sasa hivi wanaojifanya hawatutaki, watakuja usiku na mchana kutubembeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa tukizungumza masilahi ya Taifa tuwe na jazba kwa ajili ya nchi yetu, siyo unazungumza ilimradi. Hapa hatupo katika *kitchen party*, tuko hapa kuzungumza masilahi ya Taifa. Tuzungumzie

masilahi ya Taifa, jinsi gani Taifa hili tutalikombooa kulipeleka mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, ayazingatie yale ambayo nimeyaainisha katika vifungu mbalimbali juu ya suala zima la ardhi, suala zima la uteuzi ikiwezekana watu watatu waingizwe katika Bodi ya Wakurugenzi, kwa ajili ya kuingiza watu wao watatafuta vyanzo mbalimbali, taasisi mbalimbali; kwa mfano, nimetaja ANSAP, ninajua ni *partner* mzuri sana wa kilimo Tanzania.

Kwa mfano, ukiangalia, mimi nilikuwa na rafiki yangu mmoja anaitwa Dkt. Khatibu wa pale SUA Morogoro, ni mtu ambaye ni kichwa kweli kweli, lakini unaangalia Taifa hili tunamtumia vipi; watu hawa tunawahitaji kwa ajili ya kuipeleka Tanzania yetu mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ahsante sana, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Said Jafo.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijampa nafasi ya kuchangia Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, ninaomba niwape taarifa ifuatayo; Mheshimiwa Waziri Mkuu, yuko safarini Tabora kikazi. Kwa hali hiyo, amemwarifu Mheshimiwa Spika kwamba, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni mpaka atakapokuwa amerejea tena ndani ya Ukumbi huu wa Bunge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mpokee taarifa hiyo. *(Makofi)*

Baada ya taarifa hiyo, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Shamsi, maana nyota njema huanza asubuhi, nimwite sasa Mheshimwia Asaa aweze kuchangia.

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nakushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuzungumzia machache juu ya Sheria hii ya Umwagiliaji ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo. Kwa mantiki hiyo basi, niwaambie Waheshimiwa Wabunge ya kwamba, Kamati imefanya kazi nzuri, kubwa na tumetumia muda mwingi kwa kadiri ya uwezo wa kibinadamu, tulihakikisha kwamba na wenzetu wataweza kuupokea Muswada huu, wataujadili, watauchambua, hatimaye wataukubali upite kusudi ile dhana ambayo Taifa hili linahitaji, iweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria imeletwa kwa sababu maalum. Sheria hii imekusudia kufuta ama kuondoa zile kasoro za yale yaliyotangulia na ikaonekana kwamba ni kikwazo kufikia malengo hasa tunayoyataka juu ya kilimo cha kisasa, kilimo bora, kilimo ambacho Mheshimiwa Rais, kakipa jina la Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni pembejeo adimu na yenye umuhimu wa pekee, siyo tu kwa kumwagilia. Kwa ruhusa yako, ninaomba niseme neno kwa kukariri, ambalo

Mwenyezi Mungu Mtukufu, aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo humo ndani, kwa msisitizo mkubwa juu ya maji amesema na anasema: *“Wajaanla mina-l-mai-haya, kula-shai-hai.”* Maana yake kwa ufupi, nimekuumbeni kutokana na maji ili kwayo iwe ni uhai ninyi viumbe. Sasa hapa tuone umuhimu wa matumizi wa maji kwa binadamu na mimea na viumbe vingine tunavyoviona na tusivyoviona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo basi, Mungu kaibariki nchi hii ya Tanzania kwa Mito, Maziwa na vyanzo vingi vingi vya maji. Vipi tutaweza kuyatumia maji hayo tupate uhai? Tunazungumzia kilimo, tunataka tulime ili tule, baada ya kula tushibe na tukishiba tusafirishe; hii ndiyo mantiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakula, tule, tushibe, tusafirishe na tunywe yale maji ambayo Mwenyezi Mungu katubariki. Kilichobaki kwetu sasa, rasilimali watu, tuna milioni arobaini na kitu, Mwenyezi Mungu katupa akili tuitumie sasa ili tufikie malengo tunayoyahitaji wenyewe. Sina wasiwasi na Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwanza, kwa Waheshimiwa Wabunge Wanawake, nakuombeni muiunge mkono kwa vishindo sheria hii. Katibu Mkuu wa Wizara hii ni mwanamama, mwanamama akikabidhiwa jambo, sote tunafahamu, uadilifu wao, uaminifu wao na umahili wao siku zote wanaona aibu kushindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utangulizi huu, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, waiunge mkono hoja iliyoko mbele yetu kwa masilahi ya Taifa hili. Tuna hekta milioni 29 na nukta kadhaa, wataalam wamezitenga kwamba zina ubora wa kilimo cha umwagiliaji. Kati ya hizo,

zimegawika tena maeneo matatu makubwa, ambayo yana ubora wa kumwagilia, kutoka hekta 44 milioni tulizonazo, 29 nukta tutaweza kuogelea vya kutosha kwa kutumia rasilimali iliyopo ya maji ili Tanzania hii tena tuachane na ile tabia ya kusikia mkoa upi una njaa, mkoa gani unahitaji msaada, hayo tena yaishe. *(Makofi)*

Sheria hii imeletwa kusudi sasa iweze kuziba mapengo yaliyotangulia na nadhani tuachane na kujenga dhana kwa kufikiria kwamba, labda tulikuwa na sera, tulikuwa na sheria ya umwagiliaji, labda imefeli kiasi gani na hivi na vile na hii nayo tukaichanganya; tusifanye hivyo, tuone kwamba, zilizotangulia imeonekana kuna mahali tumejikwaa ndiyo maana inaletwa sheria hii sasa kuleta ufanisi wa hayo ambayo tumekosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria imekwenda mbali zaidi, imetoka katika ngazi ya Taifa hadi kule Serikali ya Mtaa. Hili kuna Waheshimiwa wameliona ni mzigo kwa kiasi fulani, lakini pia tukumbuke kuwa, huwezi kupata bila kutoa; kwa hiyo, lazima tutumie kwa kupata mazuri na siku zote mtaka cha uvunguni wanasema shurti uiname. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tutumie, nakusudia kwenda huku na huku kujenga uelewa kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako. Maana yangu ni kwamba, tukubali mzigo huu tuupokee ili tujue hatima ni kuzaa matunda tunayokusudia.

Serikali pamoja na Sekta Binafsi, kwa ujumla wao wangeiendeleza Sera ya Umwagiliaji. Pia tutafika mahali ikawa bado kwa sababu wakulima wadogo na Sekta



Binafsi, kwa utaratibu tuliokuwa nao kabla ya Sheria hii, walifika mahali wakaona kana kwamba, siyo mali zao wala haziwahusu, hizi ni za Serikali na ndiyo maana ikawa inasubiriwa Serikali kwa kila jambo. Jambo ambalo limetufikisha mahali tukaona kwamba, ni vyema ipatikane sheria ambayo itaweza kuondoa hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria imejipanga kama nilivyotangulia kusema, kwenye *Regional Level* sheria imeweka *irrigation engineer*, mtu ambaye ni mahususi, siyo *officer* tu ambaye anajua kumwagilia, ni *Engineer* wa Umwagiliaji. Hivyo hivyo, kufika Wilayani kutakuwa na Ofisa Umwagiliaji mahususi, ambaye ile hofu tuliyonayo kwamba endapo atavurunda atueleze kwa nini kavurunda na yeye ni mtu mweledi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria imezingatia pia suala zima la Sheria ya Ardhi, Sheria ya Mazingira na Sheria za Vyanzo vya Maji. Jambo lingine kubwa, kuna chombo ambacho kinataka kianzishwe ndani ya Sheria hii, nacho ni Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Tume hii imejipanga na nasema imejipanga na imepangwa kwa wataalam mahili, imejipanga kuhakikisha kwamba, uendelezaji na uratibu na usimamizi wa shughuli nzima ya umwagiliaji maji imefanikiwa kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngazi ya Wilaya kushuka Serikali za Mitaa, huko ndiko tunakokusudia kuna hicho kilimo na kwa mujibu wa Sheria hii, imefuta mkulima mdogo wa Tanzania kufanywa manamba na wawekezaji wanaokuja. Hili nawatoa shaka Waheshimiwa Wabunge kwamba, yanayotokea sasa hivi ni kwa kutokuwepo Sheria hii ya sasa. Tuna Vyama vya Wamwagiliaji Serikali za Mitaa.



Serikali za Mitaa kupitia Wilayani kuna Wahandisi. Yote hii Tume inawakilishwa na hao kuhakikisha kwamba, maudhui, madhumuni na malengo yaliyokusudiwa, yanakwenda kwa ufanisi stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tumefika mahali tuiptishe Sheria, tumuunge mkono *engineer* na timu yake, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge, ndiyo walioko huko Majimboni, Mawilayani na kwenye Serikali za Mitaa. Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani. Kasoro zitakazojitokeza, wana nafasi nzuri ya kumkabili Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati wowote ule, wasije wakasubiri tuje tukutane kwenye mjengo kwa kusutana. *(Makofi)*

Dhamana ya suala hili tumempa *Engineer*, Mheshimiwa Waziri, lakini Waheshimiwa Wabunge yote ni dhamana, kukusudia kwamba tumefanikisha lengo. Mheshimiwa Rais amesema, Kilimo Kwanza, nina imani kwamba, katika uteuzi wa wale waliotajwa ndani ya Sheria hii, atatupatia watu mahiri, watu wenye weledi wa kutosha, watu waadilifu ili mwaka 2015, Mheshimiwa Waziri amwachie kijiti mtu ambaye atajua wapi aanze, aondoke Watanzania asilimia 80 ambao wanategemea kilimo kwamba ndiyo ajira, waweze kumkumbuka ndani ya maisha yao yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni uhai, kilimo ndiyo kitakachokupa vile viwanda tunavyovipigia kelele kwa Mheshimiwa Dkt. Kigoda.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili hiyo.

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kilimo ...

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nawapongeza waliotangulia kuchangia. Naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kengele ya pili.

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Nakushukuru, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumemsikiliza Mheshimiwa Asaa, sasa tunaendelea na wachangiaji wanaofuata. Katika orodha yangu anafuata Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, lakini simwoni katika Ukumbi huu, kwa hiyo basi, nitamwita Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Muhammad Chombo, ajiandae.

**FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. LUHAGA J. MPINA, MEMBER OF PARLIAMENT FOR KISESA CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE NATIONAL IRRIGATION ACT, 2013"**

---

*[Made under Standing Order 86(9) & (11)]*

---

A Bill entitled "The National Irrigation Act, 2013" is further amended as follows:-

**A:** In clause 17

- (a) by adding the words "the Commission or any person shall collaborate with" in sub-clause (5), between the words "rights" and "the";
- (b) by deleting the words "shall be entitled to Compensation in accordance with relevant and law" or as may be agreed upon" and replacing for it the words "in the investment in the irrigation development".

**B:** In clause 18, by deleting all words and replacing for them the following new words:-

"there shall not be any displacement of people or dispossession of land as a result of implementation of this Act".

Dodoma

30<sup>th</sup> August, 2013

HON. LUHAGA J. MPINA (MP.)

**KISESA CONSTITUENCY**

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. LUHAGA  
J. MPINA, MEMBER OF PARLIAMENT FOR KISESA  
CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF THE BILL  
ENTITLED "THE NATIONAL IRRIGATION ACT, 2013"**

**[*Made under Standing Order 86(9) & (11)*]**

---

A Bill entitled "The National Irrigation Act, 2013" is generally amended as follows:-

- A:** In Clause 1, by deleting the word "National" appearing in the short titled of the Bill.
- B:** In the interpretation Clause 2, by providing a proper interpretation of the phrase "Qualified irrigation engineer".
- C:** In Clause 11, by deleting sub-section (3) and replacing for it the following:-
- "(3) A person shall not be recommended for appointment as a Regional Irrigation Manager unless he possesses the necessary qualifications as an irrigation engineer."
- D:** In Clause 14, by deleting the words "or any other officer from regional offices or under the local government authorities" appearing in sub-section (1) between the words "engineers" and "to".
- E:** In Clause 16, by-

- (a) deleting the word "two" appearing between the words "then" and "million", and replacing for it the word "five";
  - (b) deleting the words "but not exceeding ten million shillings" appearing between the words "million" and "or"; and
  - (c) deleting the words "but not exceeding three years" appearing between the words "years" and "or".
- F:** In Clause 17, by deleting the words "or as may be agreed upon" appearing after the word "law".
- G:** In Clause 63 by-
- (a) inserting the words "develop and" in sub-section (1) (a), between the words "fail" and "maintain";
  - (b) inserting the words "and order for compensation of the damage caused" in sub-section (2), after the word "forfeited".

Dodoma

28<sup>h</sup> August, 2013

HON. LUHAGA J. MPINA (MP.)

**KISESA CONSTITUENCY**

**MHE. LUHANGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Namshukuru pia Mheshimiwa Waziri, pamoja na Kamati ya Kilimo, kwa kuwasilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unaweza ukaungwa mkono au ukakataliwa endapo Waziri hataweza kusikiliza vizuri hoja za Wabunge, kusikiliza vizuri marekebisho ya Wabunge, ambayo tunataka kuyafanya hapa. Kwa hiyo, lolote lile linaweza likatokea na mnajua kwamba, Waziri hajaleta hoja hii ili sisi Wabunge tupige makofi; ameleta hoja hii ili tuweze kuijadili na kuonesha maeneo yenye upungufu tuweze kuyarekebisha kwa faida ya Watanzania; ndiyo hoja ya msingi iliyopo. *(Makofi)*

Wako Mawaziri wazuri tu, ambao wanajua kusikiliza hoja za Wabunge; mfano mzuri ni Mheshimiwa Dkt. Mgimwa, huwa akisimama kujibu hoja za Wabunge anajibu kikamilifu na ndiyo maana safari hii nilikubali kuunga mkono Bajeti ya Serikali, kwa sababu karibu kila hoja niliyoihoji alinipatia majibu kwa ufasaha. Kwa hiyo, suala la Waziri kukubali hoja yake au kuikataa ni la kawaida na wala siyo geni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na kifungu cha kwanza; kama ambavyo Wabunge wenzangu wamejaribu kuzungumza, kwamba, ni kweli kabisa kama unanifuatilia ninavyochangia, Waheshimiwa Wabunge, mnaweza kuchukua ile *Schedule of Amendment* yangu, naenda kwa mtiririko huo huo wa *Schedule of Amendment*, ambayo nimeiwasilisha.

Muswada huu ni kweli kabisa hau-*qualify* kuitwa *The National Irrigation Act*, kwa sababu siyo Muswada wa Muungano. Kwa hiyo, suala la kilimo siyo la Muungano, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika siyo ya Muungano vilevile. Kwa hiyo, tukiangalia kwenye *Schedule of*

*Amendment* pale, neno “*National*” linatakiwa liondoke ili Muswada usomeke “*The Irrigation Act, 2013.*” Nadhani ndiyo linaweza likawa jawabu zuri.

Vilevile katika kifungu cha 14(1), neno “*qualified irrigation engineer*” linaweza likawa na maana nyingi sana. Sasa neno hili ni vizuri likatafsiriwa katika Sheria hii ili kuweza kuondoa utata wa tafsiri, kwa sababu lilivyotumika katika kifungu cha 14(1), limetumika kwa umuhimu mkubwa; kwa hiyo, ni vizuri likatafsiriwa katika Sheria hii neno “*qualified irrigation engineer*” ni mtu wa aina gani, ni mtu wa *qualification* gani, ni mtu wa sifa gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Kifungu cha 11(3), uteuzi wa *Regional Irrigation Manager*. Hii ni kazi ya kihandisi, isiwe kwa ajili ya Watumishi wa Umma pekee, kwa sababu sheria ilivyozungumza imebana tu kwamba, huu uteuzi utokane na Watumishi wa Umma pekee. Hii ni kazi ya kihandisi, watu wenyewe uwezo unaweza kuwapata sokoni, unaweza kuwapata kwenye Sekta Binafsi. Kwa hiyo, nafasi hii itangazwe na watu washindane kwa uwezo na kwa ujuzi. Kifungu hicho kinahitaji marekebisho ukiangalie. *Schedule of Amendment* niliyoifanya ndiyo hasa ambayo inaweza ikafaa kwa ajili ya sehemu hiyo.

Kifungu cha 14(1), uteuzi wa *Irrigation Inspector*, sheria imesema vizuri kwamba, *qualified irrigation engineer* anaweza kuteuliwa. Ilivyoendelea ndiyo ikaharibu iliposema; “*any person.*” Kazi hii ya ukaguzi unakagua Miradi ya Umwagiliaji, unakagua miundombinu ya umwagiliaji, lazima uwe mtaalam wa *field* ile, sasa ukiacha *any person*, hii inaweza ikatoa uchochoro wa kuteua watu

*incompetent* katika eneo hilo na matokeo yake tukakosa maana yoyote. Kwa hiyo, maneno yanayosema “*any person*” yanatakiwa yaondolewe pale kwa sababu yanaharibu, ibaki tu kwamba, huyu anayefaa kuteuliwa kuwa *irrigation inspector* lazima awe *qualified irrigation engineer*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 16 kinazungumzia suala la mtu anayezuia kufanya ukaguzi wa umwagiliaji wakati yeye hana *qualification* za eneo hilo. Adhabu iliyotajwa katika eneo lile ni ndogo mno na inaharibu maana yote, kwa sababu mtu anapoingilia suala la ukaguzi, yaani utapeli ule unaweza ukasababisha madhara makubwa ambayo yanaweza kulisababishia Taifa gharama kubwa, unaweza ukausababishia umma gharama kubwa. Sasa unapoweka kwamba alipe milioni mbili na zisizidi milioni kumi bila kuzingatia kwamba ule utapeli utakaofanywa utakuwa na *damage* kiasi gani katika umma, inakuwa siyo sawa. (Makofi)

Kwa hiyo, *at least* unaweza ukaniambia kwamba, asilipe chini ya milioni tano halafu ukanyamaza pale pale ili kama *damage* atakayoifanya itaenda mpaka milioni 50 mpaka kwenye milioni ngapi, huko sasa unaiachia Mahakama ambayo itajaji kuona *damage* iliyofanywa ni ya kiasi gani na ukiendelea zaidi anasema ni kifungo kisichozi miaka mitatu. Sasa kifungo kisichozi miaka mitatu; kwa nini kisizidi miaka mitatu wakati huna uhakika na huo utapeli utakaofanywa utakuwa na *damage* kiasi gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 17, *declaration of irrigation area*; ugumu wa Muswada huu na utata mkubwa



wa Muswada huu upo katika hili eneo. Ninapozungumza hapa ninayo Sera ya Umwagiliaji nchini ambayo inazungumza bayana kwamba, watu hawa, wawekezaji, kwa maana ya *private sector*, kwa muda mrefu wamekuwa na hofu kubwa kutokana na upatikanaji wa ardhi pamoja na maji. Kwa hiyo, hakuna mashaka kwamba, hii sheria iliyoletwa mbele yetu inajibu hiyo hoja kwamba, lazima uwepo uhakika wa upatikanaji wa ardhi na maji. Tatizo siyo hilo, tatizo ni kwamba, unazungumziaje sasa hao Wananchi ambao ardhi hiyo wanayo sasa. (*Makofi*)

Ukisoma kifungu cha 17(1) pamoja na kifungu cha 17(5), kifungu cha 18 pamoja kifungu cha 4(1), utaona kwamba, ardhi ya Wananchi inataifishwa sasa na Serikali na kuwa chini ya *Commission*. Sasa kutokana na vifungu hivyo, ukivisoma vyote kwa pamoja utagundua hilo. Utakapoligundua lile, tayari utatengeneza maswali mengi ambayo yanatakiwa yapate majibu kabla ya Bunge hili kuridhia Muswada huu. Unapata maswali mengi kwamba siyo mara ya kwanza Serikali kuwa na maeneo ya umwagiliaji, kuwa na mashamba makubwa ya ranchi, lakini mashamba hayo yalibinafsishwa, yaliuzwa na faida kwenye umma hatujaelezwa mpaka leo. Yapo Mashamba ya Kapunga, ya *NAFCO* na ranchi mbalimbali hapa nchini, hatujaelezwa faida hizo zimepatikana namna gani katika Taifa. (*Makofi*)

Sasa leo unaposema unaipa uwezo *Commission* wa *ku-own land*, wa kuichukua ardhi mpaka kwa Mwananchi na wao wanaanza kuwekeza na mwekezaji mwingine, maana yake unalirudisha Taifa kule kule ambako lilikuwa na ardhi hizo za umwagiliaji, lilikuwa na ranchi, ardhi zile zimeuzwa

kwa watu mpaka leo hawalimi, mpaka leo wanatumia ardhi zile kujipatia mikopo kwa faida yao, mashamba yale hayalimwi, wananchi hawanufaiki nayo. Sasa *caution* ya wewe unapoikabidhi leo *Commission*, uhalali na haki za Wananchi zimejengwa namna gani wanaomiliki ardhi hiyo sasa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikuombe sana katika kifungu hiki, Waziri asikilize kwa makini na bahati nzuri hata Wabunge ambao walisimama wakaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, bado wamekuwa na hofu kubwa na suala la ardhi. Suala la ardhi aliangalie vizuri kwenye sheria yake na kama maelezo ya hali ya suala la ardhi, kwa sababu sheria nilivyoisoma na nilivyoielewa, ukweli ni kwamba, imejibu hoja ya mwekezaji kwamba, atakuwa na uhakika na *land*, atakuwa na uhakika na maji; lakini je, haki ya hawa ambao wana ardhi leo, uhakika wa ardhi yao utakuwaje na masilahi yao yatakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia leo tunamruhusu sasa Waziri atangaze eneo la umwagiliaji, tumemruhusu akafanye hivyo, lakini tunamruhusu kazi ile akaifanye, hana *limit* yoyote, kwa sababu ardhi tunayoitaja leo, hekta milioni 29.4 ina watu ambao wanaishi mle, wanafanya shughuli za kiuchumi; unapozungumza kufanya *replacement* ya watu wanaoishi katika eneo la hekta milioni 29, maana yake unazungumzia kazi kubwa na ujue kwamba unazungumzia leo umwagiliaji, lakini shughuli za Wananchi wetu zimegawanyika.

Sasa kama huyo atakuwa na uwezo tu wa kutangaza, najua hawezi kutangaza *National Park*, anaenda

kutangaza maeneo ambayo yanamilikiwa na Wananchi. Kwenye *National Park* hata kama kunafaa kwa ajili ya umwagiliaji, hawezi kutangaza, lakini maeneo yanayofanyiwa kazi na Wananchi, yale ndiyo anayoenda kutangaza. Sasa leo yakitangazwa *irrigation* maeneo yote; je, suala la wafugaji litakuwa limezingatiwa kwa kiasi gani katika Sheria hii?

Kwa hiyo, ndiyo unakuja kwenye hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee, japo ni CHADEMA, lakini haki yake tunampa kwamba, lazima tukubaliane wote kwa pamoja kama ni ardhi yetu hii matumizi yake ni vipi; kama tunakubaliana hekta kadhaa ziende kwa ajili ya *irrigation*, basi hizo ziende kwa ajili ya *irrigation*. Leo tutatoa ardhi yote tutatangaza kwa sababu hii nayo ni sawa na *National Park* na watu ikishatangazwa kuwa ni eneo la umwagiliaji, hawaruhusiwi kufanya shughuli yoyote ile. Ukisoma kifungu cha 63, kinakataza kufanya shughuli nyingine yoyote tofauti na *irrigation*. Sasa, *suppose* haya maeneo yote, hekta milioni 29.4 yakatangazwa kwa ajili ya *irrigation*, mkasahau kwamba kuna wafugaji, mkasahau kwamba kuna watu wengine ambao wanafanya shughuli za uchumi ambao nao wanatakiwa wapate ile *ration* ya ardhi; itakuwaje katika hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atakapokuwa anajibu hoja hii, ajibu vizuri suala la ardhi ili kuondoa utata na kama atakuwa hajajiandaa vizuri kuhusu hili suala la ardhi, basi *a withdraw* Muswada wake ili tuelezwe vizuri, tuelewe uhalali wa Mwananchi baada ya *Commission* na baada ya Wawekezaji kuja watakuwa na uhalali gani katika ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 17(5) hiyo hiyo, kinazungumzia suala la fidia badala ya Tume kuwekeza pamoja na wamiliki wa ardhi. Sasa hapa inazungumza fidia tu, wewe ukikutwa na shamba lako imekuwa *declared* kwa ajili ya *irrigation*, unapata *compensation* unaondoka. Je, kama mimi mwenye ardhi hiyo nataka kuwekeza katika umwagiliaji kwa nini nisiingie ubia na huyo unayetaka kumleta wewe; aidha, wewe mwenyewe Tume au ulete hao wawekezaji unaotaka ili nipate *right* kwa ajili ya kuwekeza?

Kwanza, ile *ownership* ya ardhi yangu inaendelea kuwepo, lakini naendelea kufanya hizo shughuli za kilimo cha umwagiliaji. Sasa Sheria hii tukishapata ule uhalali wa ardhi, Sheria hii wanaweza wakaifanyia hata *amendment* wakaweka kipengele ambacho kitaruhusu Mwananchi kuwekeza pamoja na wale wanaokuja kuwekeza na siyo kulipwa fidia kwa ajili ya kutoa ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 17(5) hicho hicho, ukisoma pale mwisho wanasema *compensation* itafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi iliyopo, lakini wanasema kingine *as may be agreed upon*. Hiki kifungu ni kizuri kikitumika vizuri, lakini hatuna uadilifu namna ile. Unaposema *as may be agreed upon* katika *compensation* huwezi ukakutana na watu wengine wakalipwa fidia za ajabu, ikiwa ni uchochoro wa Taifa hili, ikawa ni uchochoro wa kufuja fedha za umma kwamba, Sheria inaturuhusu kwamba mtu yeyote anaweza akafanya hesabu zake na vilevile tukamlipa kulingana na tutakavyokubaliana.

Kwa hiyo, ukiweka Sheria ya namna hii, tayari umeweka uchochoro mkubwa wa ufujaji wa fedha za umma kwa Watendaji wa Serikali ambao siyo waaminifu. Vilevile ukiweka sheria ya namna hiyo lazima ujiulize; kwamba wakienda kwenye maelewano wakashindwa itakuwaje; nako lazima ufafanue kwamba, *as may be agreed upon*. Kama wataenda kwenye majadiliano yale wakashindana inakuwaje katika suala zima la uendelezaji wa *irrigation development*?

Kwa hiyo, hiki kifungu kimekaa hapa, lakini kinavyo-*hang* kinaweza kikatumika vibaya, kwa ufisadi mkubwa, Taifa likafilisika, kwa sababu ya watendaji ambao siyo waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hicho kifungu kirekebishwe na kiwekwe kifungu ambacho kitawa-*support* tu hawa Wananchi. Kama Sheria ya Ardhi iliyopo sasa hivi, Wananchi katika *compensation* hawapati haki yao sawasawa, basi kiwekwe kifungu ambacho kitawalinda kupata fidia iliyo halali ya mali zao zilizohamishwa au zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 63(1)(a) kiongezwe maneno ili kukipa nguvu zaidi kwa watu na kwa makampuni ambayo yameshajitwalia eneo la umwagiliaji, lakini bado wameshindwa kuendeleza miundombinu ili tusirudi kule kule. Watu watakimbilia kuyachukua maeneo haya, watachukua ardhi, watachukua hati na baadaye hawataenda kufanya zile shughuli za kilimo, wataenda kufanya shughuli zingine, lakini wanatumia zile hati kupata fedha kwa masilahi yao.

Sasa kifungu kile kinaweza kikarekebishwa, ikawekwa nguvu pale ya kisheria. Kwenye *Schedule of Amendment* pale, Kifungu cha 63(1) kinaonesha lile neno likiongezwa pale linaweza kuleta nguvu ya kuiwezesha Sheria hii kuwadhiti watu wa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 63(2) nacho kiongezwe nguvu ili kuweza kufidia hasara iliyosababishwa na mtu ambaye amehusika katika suala zima ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ni kengele ya pili.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Schedule of Amendment* ya Kifungu cha 63(2) inaonesha ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, ni kengele ya pili.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Mpina, nilisema nitamwita Mheshimiwa Chomboh, lakini simwoni ndani ya Ukumbi wa Bunge. Sasa nitamwita Mheshimiwa Kaika Telele na atafuatiwa na Mheshimiwa Moza Abedi.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada wa Sheria wa Taifa ya Umwagiliaji wa mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kufanya hivyo, naomba kwa rufusa yako, nimpongeze sana Naibu Waziri wa Maji, alipata nafasi ya kuutembelea Mkoa wa Arusha katika shughuli zake za kikazi. Ziara ambayo ilimpeleka katika Wilaya zote za Mkoa wa Arusha, ikiwemo Wilaya ya Ngorongoro ambako ni mbali sana na Mkoa na siyo Mawaziri wote wanaweza kufika huko. Nampongeza sana kwa kazi ambayo amefanya na kuona matatizo yetu ya maji, ila naomba kumkumbusha kwamba, zile milioni 700 ambazo tumewaomba kama Wizara, atukumbuke katika ufalme wake ili tuweze kutatua matatizo ya maji tuliyonayo.

Baada ya pongezi hizo, kwa niaba ya Wananchi wa Ngorongoro, naomba niipongeze pia Serikali kwa kuleta Muswada huu wa Umwagiliaji; kama walivyosema Wabunge wengi waliochangia, ni jambo ambalo litawasaidia Watanzania katika ujumla wao, lakini hasa maeneo ambayo wanakuwa na hizi skimu za umwagiliaji ambazo zimewekwa na Serikali au kuna zile ambazo ni *traditional irrigation schemes* za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limefika kwa kuchelewa kidogo, lakini tumewahi, tukichambua vizuri sana Muswada huu, bado inaweza kuleta neema kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Muswada huu ni kuanzisha Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, jambo ambalo pia litapelekea kuundwa kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Tume zimekuwa nyingi, lakini zikiwekewa mkakati na utaratibu mzuri, zinaweza zikafanya kazi nzuri.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako limepitisha sheria nyingi sana. Bunge hili na Mabunge mengine yaliyotangulia, ukiangalia sheria ambazo tumepitisha nyingi sana kusema kweli, lakini zingine zinakuwa mbovu na hivyo kupelekea kutazamwa upya na kufanyiwa marekebisho. Sheria zingine zinakuwa hazitekelezeki na kupitwa na wakati na hasa kwa sababu kanuni za utekelezaji wake zinachelewa kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zingine hazisimamiwi kikamilifu na hivyo kukosa meno ya uhalali wa kuwa Sheria. Wakati mwingine mimi naona kwamba, sheria za mila za makabila mbalimbali zinakuwa kali kuliko hata sheria tunazopitisha hapa Bungeni na hii ni kwa sababu taratibu hizo za mila na desturi zinasimamiwa na Wananchi wenyewe moja kwa moja wa jamii ile, zikiongozwa na wazee ambao wameteuliwa kuangalia mambo ya mila na desturi zinasimamiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niwape tu mfano; kwa jamii ya Kabila la Wamasai ambalo mimi ni mmojawapo, ukimuua ndugu yako kwa kukusudia au kwa bahati mbaya ni lazima ulipe ng'ombe 49 na wanataka ulipe pale pale moja kwa moja, inakuwa kama unapigwa faini Mahakamani na unatakiwa uitoe pale pale, ukikosa mtu wa kukudhamini unakwenda ndani, ndivyo ilivyo katika hii pia. Ndugu zetu Wabatemi ambao ni Wasonjo pia wanaitwa Wasonjo kwa jina maarufu, lakini kwa jina zuri wanaitwa Wabatemi; hawa Wabatemi, vijana wa umri kati ya miaka 15 na 30 hawaruhusiwi kufika kwenye vyanzo vya maji, wawe wa kiume au wa kike na wala msiniulize ni kwa nini, wanajua wenyewe.



Wakati Profesa Mwandosya akiwa Waziri wa Maji, nilimwomba aniletee wataalam wa kwenda kuangalia namna ya kutumia maji ya Mto Ngauka kule Digodigo kwa ajili ya umwagiliaji, akaniletea, lakini bahati mbaya sana wataalam wale waliongozwa na mwanamama. Kwa hiyo, kwa mujibu wa mila hizi na desturi hizi, hakuruhusiwa kufika kwenye chanzo cha maji.

Kwa hiyo, nikapata tabu sana ya namna sasa ya kujenga hoja kwa wale wazee, huyu mtaalam aliyetoka kote huko Dar es Salaam akafika Digodigo Ngorongoro, aweze kukubalika kufika huko. Ilinichukua saa nzima kuwashawishi, lakini wameniambia chanzo atakwenda lakini chanzo cha maji ni pale na hawezi kwenda zaidi ya pale. Basi, bahati nzuri ikawa kwamba, walikuwepo wataalam wengine wawili zaidi, akawakabidhi hiyo kazi wakafika kwenye chanzo cha maji. Naeleza haya kwa sababu Sheria tunazotunga mara nyingi zinakuwa hazina meno, hatuzisimamii ziweze kutekelezwa vizuri zisaidie jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niliseme ni kwamba, baadaye wazee wale walikubali kwa masharti hayo, lakini yule mtaalam tulimwomba msamaha sana kwa sababu naye alijsikia vibaya, lakini nikamwambia wala asijisikie vibaya kwa sababu hawa watu wa huku bado wanashikilia mila na desturi zao, kama ninyi mmeshaachia za kwenu, siyo huku sasa inaleta matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, masuala ya umwagiliaji ni muhimu sana katika kupata uhakika wa chakula na usalama wa chakula. Katika Jimbo langu la Uchaguzi, yapo maeneo ambayo kuna hizi *traditional irrigation schemes* ambazo nitaomba Serikali baadaye ziboreshwe ziweze kunufaisha zaidi kuliko ilivyo sasa.

Maeneo ya Wabatemi au Wasonjo kule, eneo la Muholo, Olonyosambu, Chema, Kisangiro, Digodigo, Samunge, Sale, yana hizi *irrigation schemes* za kienyeji tu, lakini zimewasaidia kwa miaka mingi iliyopita. Katika maeneo mengine ya Pinyinyi, Engaresero, Monikisero na kule Harashi, tungeweza kuweka *irrigation schemes* ambazo zitasaidia sana Wananchi katika masuala ya umwagiliaji.

Kwa hiyo, kwa ujumla tuna hekta 500, 600 hivi, ambazo zikiboreshwa maeneo yale yanaweza yakalisha Wilaya nzima ya Ngorongoro. Niwaambie tu kwamba, Wilaya ya Ngorongoro ina kilomita za mraba 14,036, ni eneo kubwa sana kijiografia, lakini asilimia 59 ya eneo lile ni Hifadhi ya Ngorongoro, ambako kule kilimo cha kujikimu au kilimo kikubwa hakiruhusiwi kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo, tuangalie eneo hili la asilimia 41 tu ndiyo ambalo linatumika kwa mambo mengine ya Wananchi. Kwa mfano, kwa kilimo ndiyo kule *Game Control Area*, ni *RAMSAR side*, ni maeneo ya misitu, ni maeneo ya madini, ni maeneo ya uwekezaji na maeneo ya malisho ya mifugo. Kwa hiyo, ni asilimia hii 41 ndiyo inatumika kwa kazi yote hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutwaa maeneo ya Wananchi kwa ajili ya umwagiliaji kama Sheria inavyosema kwamba, Tume inaweza kufanya hivyo, ni jambo la

kuangalia sana. Kwa sababu kama wanavyosema Wabunge wenzangu, migogoro ya ardhi imekuwa mingi sana katika nchi hii na tusiongeze mingine. Kama inatakiwa eneo lichukuliwe kwa ajili ya umwagiliaji ni lazima Tume iafikiane na Wananchi wa maeneo yale kupitia Halmashauri zetu za Wilaya. Vinginevyo, tutakaribisha migogoro na hali itaendelea kuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wa kilimo cha umwagiliaji lazima kwa mujibu wa Sheria hii waende vijijini zillipo hizi *traditional irrigation schemes* ili kutoa elimu, ushauri na maelekezo ya kilimo cha umwagiliaji kwa Wananchi kwa mujibu wa Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ole-Telele, kwa mchango wako na hasa kwa kutukumbusha hizo Mila za Kimasai. Sasa sijui kwenye *fifty fifty* itakuwaje huko, lakini utasonga mbele tu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, naomba nimwite Mheshimiwa Moza Abedi, atafutiwa na Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kupata nafasi niweze kuchangia suala la hili la upitishaji wa Sheria ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nampongeza Waziri pamoja na Kamati yake, walioweza kukaa kwa

pamoja wakajadili suala hili likapitishwa. Suala hili linanitia wasiwasi mkubwa, kwanza, nimelipokea na ninaliunga mkono, kwa sababu limekaa katika *section* ambayo ni nzuri kabisa na utekelezaji wake unaonekana utakuwa mzuri. Sasa kama Taifa limekumbuka kwamba, kuna Wananchi ambao wanapata shida ya njaa, wanahangaika na leo hii wameamua kupitisha Sheria hii, mimi ninaiunga mkono asilimia mia kwa mia. Wasiwasi unakuja, utekelezaji huu ambako tena umekuja wakati siyo mwafaka, umechelewa, angalau ungekuja hata kuanzia mwaka 2011, 2012, leo 2013, tungekuwa tunaona utekelezaji wake.

Hofu yangu isije ikawa ni sera ya kutufikisha 2015 na kama ni kweli ni dhamira ya kumkomboa Mwananchi kwa kuweza kumtoa katika hali ngumu ya kimaisha, hasa yule mkulima anayelima kule kilimo cha chini kabisa, leo hii unampanulia wazo kama hili anapata zana za umwagiliaji, anaingia katika mfuko huu ambao anaweza kupata pensheni yake kwa kila mwezi inamnufaisha. Mimi ninaomba uwekwe mkazo mkubwa kwenye Sheria hii kwa wale wote ambao wataipotosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi mwingine nilionao ni kwamba, kuna migogoro mikubwa sana ya ardhi. Tanzania ina ardhi pana, ina mapori makubwa na ina maeneo makubwa, lakini tunaposema tunaita wawekezaji, wawekezaji hawa hawa ndiyo wanaofanya Wananchi wetu kuwa manamba wao, halafu hawatapata manufaa, wawe wanapitia kwenye migongo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majuzi tu hapa kati kwenye migogoro hii hii ya ardhi, Mheshimiwa Waziri, alisimama

ndani ya Bunge hili Tukufu akasema, alipita kwenye Wilaya ya Kondoa akakuta kulikuwa na migogoro ya ardhi akasema angepita kule akahakikisha anamchukua Mheshimiwa Zabein Mhita na Mheshimiwa Nkamia ili waende wakatatue mgogoro ulioko kule wa ardhi.

Mpaka leo hii Mheshimiwa Waziri hajafika na mpaka leo hii Wananchi wanaendelea kunyanyasika kidogo kidogo bila ya kupata utatuzi wowote na wala bila ya kupewa maelekezo. Sasa leo sheria kama hii inakuja na tayari katika Wilaya ya Kondoa kuna mabwawa yaliyoanza kutengenezwa na fedha zimeshatengwa kwa ajili ya kutengenezwa kilimo cha umwagiliaji. Je, kilimo hiki cha umwagiliaji si kitakwenda kuwa cha kina fulani na fulani?

Mimi ningeona katika mpangilio mzima huu, basi ungetoa ufafanuzi zaidi, unawalenga Wananchi wa maeneo gani na katika maeneo yao wana hadhi ya kuweza kusimama pale pale walipo ili wapate haki zao au wataambiwa waondoke ili waweze kulipwa kiasi fulani wapishe maeneo kama hayo? Sasa vitu kama hivi, Muswada huu haukuweka uwazi; kuna maeneo yako sahihi, kuna maeneo mengine ya kuwafafanulia Wananchi ili wajue kiuhalali, jinsi ulivyo unatia mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna maeneo mengi na kuna mabonde mengi, ninayatolea mfano mabonde mengine ambayo yako katika Wilaya ya Kondoa hasa kule kwa Madebe, wanalima na mifano mnaiona; mikungu ya ndizi inaoneshwa mpaka kwenye maeneo ya mifano. Mnenia kule kuna mabonde makubwa, watu wanalima vitunguu. Mheshimiwa Waziri pia nilimwambia,

tunahitaji kilimo cha umwagiliaji katika Bonde lile na akasema angepeleka watu.

Mimi nimefurahi suala hili limekuja hapa, sasa nafikiri hili eneo litakuwa mwafaka na Wananchi wa Wilaya ya Kondoa wasipate wasiwasi, wahakikishe wanatenga tu maeneo, maana kuna Mto Bubu pale mpunga na kila kitu tutaupata. Sasa je, mbegu bora mbona hamkutuainishia ziko wapi? Tutapata wapi hizo mbegu, maana mbegu zinazouzwa huko kwenye wakala zingine ni za miaka iliyopita ukipanda hazioti. Tumelalamika na mpaka leo tunaendelea kulalamika, bado hazifuatiliwi na mawakala wanaobeba hizi mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimefurahia sana suala hili limekuja na suala la maji, akina mama naona sasa watapata burudani kubwa ya kupata maji katika maeneo ambayo yanakabiliwa na shida ya maji. Maji ni chanzo kikubwa na ni kero kubwa kwa akina mama; akina mama wengine wanafia kwenye mashimo ya maji hasa huku katika Wilaya ya Kondoa. Akina mama wanakunywa maji machafu kama hizi sofa tunazokalia nyekundu. Akina mama wana kilio kikubwa cha maji, maji yamekaa kama maziwa, maji siyo salama.

Huko Mrijo watu kila siku wanapata vichocho. Leo Mradi huu umekuja, najua utakuwa ni salama na utakuwa mzuri, lakini wasiwasi wangu isiwe ni sera ya kuingia mwaka 2015, iwe ni sera endelevu ya kuhakikisha Wananchi wananufaika, wanapata maji salama na wanapata kilimo hicho kwa usahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Moza, Mbunge kutoka Kondo, Mkoa wa Dodoma, Chama cha Wananchi (*CUF*), kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, nilisema sasa nitamwita Mheshimiwa Murtaza Mangungu na baada ya hapo atafuatiwa na Mheshimiwa Keissy.

**A SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON.  
MURTAZA ALLY MANGUNGU, MEMBER OF PARLIAMENT FOR  
KILWA CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF THE BILL  
ENTITLED "THE NATIONAL IRRIGATION ACT, 2013"**

---

*[Made under Standing Order 86(9) & (11)]*

---

A Bill entitled "The National Irrigation Act, 2013" is amended in Clause 34 as renumbered, by deleting the words "Village Council" appearing in sub-clause (1), between the words "the" and "authenticate" and substituting for them the following new words "General Village Assembly."

**Dodoma**

30<sup>th</sup> August, 2013

**HON. MURTAZA ALLY MANGUNGU, MP.**

**KILWA CONSTITUENCY**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada ambao uko mbele yetu leo. Ukichangia mwishoni, ipo shida kwamba, utaweza



kuchangia mengi ambayo tayari yalikuwisha kuzungumzwa. Kwa kuwa yapo ambayo nakubaliana nayo, nataka nianze na ndugu yangu Mheshimiwa Jafo, alisema methali moja ya Kizaramo kuwa: *"Zilongwa mbali, zitendwa mbali"*. Wazaramo wanasema *"Zilongwa mbali, zitendwa mbali"*, maana *Kisokela Kulonga Mbuli Muhala,* maana yake kwamba, tumechoka kusema maneno matupu.

Maneno matupu yanakuja kuletwa sasa na Muswada huu. Wachangiaji waliotangulia asubuhi wametustaajabisha kwa maana kwamba, tumekuwa tukiishinikiza Serikali ilete sheria, sheria imekuja na wengine bado wanasema hakuna jambo ambalo limefanyika, bado hatujafika kokote; ajabu kubwa sana! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirudi kwenye Muswada huu, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, kwa mtu yeyote yule ambaye ana fikra timamu, hawezi kuwasha taa halafu akaifunika; haiwezekani. Unawasha taa ili iweze kumulika. Umeleta Muswada, Wabunge wanaunga mkono, wanaupitisha, tunataka sheria hii haraka ifanye kazi tuweze kuokoa kilimo, tuweze kuboresha kilimo.

Mwezi Julai, nilikuwa miongoni mwa Wabunge ambao tulikuwa kwenye ziara ambayo iliandaliwa na wenzetu wa *USAID*, tulitembelea maeneo mbalimbali; tulikwenda Arusha, Arumeru, Mgeta, Dakawa na maeneo tofauti. Matatizo ambayo yameainishwa mengi yatakata suluhu kufuatana na Muswada huu ambao umeletwa. Naomba baada ya Sheria hii kupitishwa na kusainiwa na Mheshimiwa Rais, kanuni zisije tena zikatumia miaka kumi kuanza kutumika kwa Muswada huu. Tunaomba mharakishe,



kanuni zitengenezwe haraka ili Muswada uweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri; wakati dhana ya Kilimo Kwanza inakuja na kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais, ilikubalika kabisa lazima kianzishwe chombo ambacho kitakuwa kinafanya *coordination* na Wizara nyingine zote. Chombo hiki ilikuwa kinatarajiwa kiitwe *Agricultural Transformation Council*. Hatukufanya hivyo na mpaka sasa bado hatujafanya hivyo; matokeo yake Wizara ya Ardhi wana yao, Wizara ya Kilimo wana yao, Wizara ya Mifugo wana yao, Serikali za Mitaa wana yao, Wizara ya Maji wana yao, nchi moja na Serikali moja kwa nini hakuna *coordination*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ethiopia walikuja kwetu ku-*adapt* Mpango wa KILIMO KWANZA. Wamekuja kuchukua Mpango ule na waliporudi kwao wakaenda kufanya kila kitu ambacho tulikifanya sisi na wao walianzisha *agency* kufanya *coordination* ya kilimo. Huwezi kulima kama huna maji, huwezi kulima kama huna ardhi.

Sasa Wizara hizi zinakinzana, Wananchi wanaweza wakasema eneo hili ni bora sana kwa ajili ya kilimo, Wizara ya Maliasili inasema hapana eneo hili sisi tumeliweka kwa ajili ya hifadhi kwa ajili ya kuweka wanyama. Serikali za Mitaa kupitia Halmashauri wanasema hapana, eneo hilo tumetenga kwa ajili ya uwekezaji wa kuchimba gesi au kitu kingine chochote. Sasa nani ambaye atakuwa anafanya *coordination* ya hizi taasisi nyingine ambazo zinaunganika? Nitafurahi sana kama Mheshimiwa Waziri, ataweza kunijibu hili na hili litaweza kufanyiwa kazi inavyotakikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo lingine, licha ya umwagiliaji kuwekewa sheria hii; hebu tujaribu kuangalia Wizara ya Nishati na Madini nayo vilevile inatakiwa itoe mchango wake. Pale Dakawa lipo tatizo, mradi ule uwe una-*run* kwa kipindi cha miezi minane, lakini bili ya umeme ambayo wanatozwa kwenye Mradi ule wa Skimu ya Umwagiliaji wa Mpunga wanatozwa *throughout the year*, miezi yote 12.

Sasa lazima kuwe kuna *coordination* pia, huwezi kuboresha kilimo bila ya kuwa na nishati ya kubadilisha hayo mazao ya kilimo kufikia kwenye soko. Vinginevyo, kila siku tutakuwa tunaandaa chakula lakini hakiwezi kufikia thamani, kwa sababu hatuna nyenzo za kukiongezea thamani chakula kile kuingia kwenye soko.

Lingine ambalo nilitaka niseme ni *coordination* ya masoko. Ni jambo la kustaajabisha sana, ukienda maeneo ya Mgeta, kuna Wamarekani ambao wamewekeza pale katika kilimo cha umwagiliaji, wanalima mpunga na kuna mchele ambao haujulikani hata idadi yake. Kwa kipindi cha miaka minne, mchele ule wameshindwa kuuingiza kwenye soko kwa sababu chakula kinatoka nje; kinatoka Thailand, China, Taiwan na Vietnam. Mchele sisi tunao ndani, sasa tunafanya *coordination* gani ya masoko yetu?

Leo hii utakuta Kyela na Tunduru wana mchele wa ziada ambao haujaingia kwenye soko, lakini maeneo ya Shinyanga, Mwanza na Lindi wana upungufu wa chakula. Haya ni mambo ya ajabu, hata kama tutatunga sheria ambayo itakuwa ni nzuri kwa kuiramba, kama hatuitekelezi

na kufanya *coordination* ni sawasawa na kuchota maji kwa uma tunatia kwenye tenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nikubaliane na pendekezo moja ambalo limetolewa pamoja na mapendekezo mengine yote, nataka nisimamie kwenye moja. Kamati ya Kilimo katika mapendekezo yake, kipengele cha (4), imesema: “Pamoja na ushirikishwaji wake sekta binafsi katika kilimo, utekelezaji wa Sheria hii, Serikali iweke utaratibu mzuri ili wakulima wadogo wasiathirike.

Kama tunatenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji, wawekezaji waende katika maeneo ambayo yanahitaji kuwekeza miundombinu na maeneo ambayo ni magumu kuweza kufikika. Wakulima wetu waendeleo kuwepo katika maeneo yao ya asili, waweze kunufaika na maeneo hayo. Siyo leo hii anakuja mwekezaji anaonekana yeye ni Nabii mpya kuweza kupewa eneo bora na mkulima anaambiwa atoke aende kwenye eneo lingine. Hii itakuwa ni sheria mbaya kabisa ambayo haikustahili kuwepo kabla ya kuwepo kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Muswada huu, kipengele cha 35, nitaanzia katikati kinasema hivi: “...*Village Council, authenticate ownership of plots or allocate plots on an irrigation scheme as the case may be ...*” Mimi nasema, Mamlaka ya Vijiji maeneo mengine ndiyo yamekuwa matatizo. Serikali ya Kijiji wanakaa wao wenyewe watu wanane, Mwenyekiti na Wajumbe wake, wanampa eneo mwekezaji, Wananchi hawana habari. Sasa hapa lazima tufanye marekebisho tuseme kwamba, Mkutano Mkuu wa Kijiji kile uhusike na Halmashauri ibariki

uwekezaji huo ili uwe na ushirikishwaji mpana, kuondoa vita ambayo inakuwepo baina ya Wanavijiji na Viongozi wa Vijiji. Mara nyingine Wananchi wanachukuliwa tu wanaingizwa kwenye chombo ambacho hawajawahi kushirikishwa na hawajakubaliana. Hili unaweza ukaliona maeneo mengi hata mihitasari wanakuwa wanai-*forge* ili kuweza kumpitisha tu mwekezaji kwa kuwa mwekezaji yule ametanguliza kitu fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha 37 cha Muswada huu kimesema kwamba, Mamlaka iwe na uwezo. Yenyewe imetoa Sheria ya *Land Act* na *Village Act* ndiyo ambayo itakuwa inasimamiwa. Hizi sheria ndizo ambazo zinatumiya mlolongo mrefu kuweza kutoa nafasi kurudishwa ardhi ambayo imetwaliwa na kumilikishwa bila kuendelezwa. Sasa mamlaka iwepo kwamba, pale ambapo tunaweza kufanya *assessment*, mwekezaji huyu tumempa kwa misimu miwili hajaweza kuendeleza, palepale tuna-*nullify* mkataba wake na tunampa mtu mwingine aweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie katika Muswada huu, mengi ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge hapa ni ya msingi. Nataka nikubaliane na mapendekezo ambayo Serikali imeyaleta kwamba, sasa tuweze kusimamia, tuwe na kilimo na tupate mazao yenye tija. Kipengele cha mwisho ambacho nilitaka nikizungumzie ni Ibara ya 54(d) cha Muswada ambayo inaelezea namna ambavyo Wananchi au Wakulima wataweza kupata mikopo. Lazima tuangalie mfumo mzuri wa kuwasaidia wakulima kuweza kuboresha kilimo hiki.

Kwa kipindi kirefu sana wakulima wamekuwa hawana mahali pa kukimbilia, hakuna sehemu ambayo wanaweza wakapumulia, tunataka tuweke mfumo mzuri ili kila mkulima ambaye ana uwezo wa kulima akopeshwe alime ili tuweze kupata chakula cha kutosha na tuachane na hii adha ya kuagiza chakula kutoka nje. Ni jambo la kustaajabisha sana, kwa kiasi kikubwa cha ardhi tulichonacho leo hii Tanzania na mvua tunazozipata, tumekuwa tukitegemea chakula kutoka nje! Tunaagiza mahindi, sukari, mchele na itafikia hata mtama utaagizwa kutoka nje kwa ajili ya ku-*feed* viwanda vya vyakula hapa nchini.

Tunayo ardhi ya kutosha na mabadiliko haya yote hayawezi kupatikana kama hatukwenda kwenye *mechanised agriculture*. *Engineer* Chiza ni mtu ambaye tunamwamini na ametumia muda mrefu sana kuitumikia Serikali kwa uadilifu, sasa tunataka ule uadilifu wako usiwe wa maneno, tunataka vitendo. Una Mchumi ambaye amebobea na tumempitisha yuko hapo na wewe ni *Engineer* mtaalamu, hatutaki maneno, tunataka tuone kwamba sasa kilimo kinainuka na kupata mwelekeo unaotakikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Murtaza Mangungu. Waheshimiwa Wabunge, nilisema sasa nitampa nafasi Mheshimiwa Keissy, baada ya Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Agripina Buyogera naye ajiandae.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi jioni ya leo. Kwanza kabisa, namwunga mkono Mheshimiwa Mpina, mia kwa mia. Marekebisho ya Mheshimiwa Mpina, yafuatwe ndiyo nitaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mimi sikatai Muswada huu, Muswada moja kwa moja ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wabunge wanaochangia hawana ujuzi wa kulima na hawajashika hata jembe; anakuja hapa anachangia anasema haufai mradi wa kumwagilia kwa sababu hajui lolote, hajawahi kulima. Mimi nimewahi kulima mpaka eka 250 ziliungua zote kwa kukosa maji mara mbili na mpaka nikauza trekta.

Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya umwagiliaji lakini natahadharisha, hatukubali Mkoa wa Rukwa kumleta mwekezaji. Wananchi wetu wawezeshwe maji watalima wenyewe. Hatuna ardhi ya kumwezesha mwekezaji, tuna matatizo, Malonje wanauawa watu kwa ajili ya uwekezaji mpaka Rais ameingilia mzozo lakini mpaka leo Wananchi hawajapewa shamba lao, hatukubali uwekezaji watatuletea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ibadilishwe wote waliopora mashamba kwanza wafuatiliwe wanyang'anywe yale mashamba waliyopora kwa njia za haramu. Wamejiuzia mashamba kwa bei ya chini, bei ya kutupa, wamekwenda kuweka *deposit* benki, wamechukua mabilioni ya fedha na mpaka mabenki yamefilisika. Tuanze

upya, tutaunga mkono hoja hii, hatuna ardhi Tanzania ya kuchezeachezea.

Wamechukua mashamba vibaya ya Wananchi, Rukwa hatuna mashamba na hivi leo nazungumza hapa kuna ugomvi Kata ya Kipili kati ya wafugaji na wakulima, wanataka kuuwana. Maandamano, zaidi ya watu 200 au 500 wako Polisi Kirando wanataka kuuwana kwa ajili ya ardhi, leo mnataka kutuletea wawekezaji itakuwa Zimbabwe nchi hii. Hatuwezi kuwa kama Zimbabwe, Wananchi wetu tulipata uhuru tukiwa milioni saba, leo tuko milioni 45 ardhi iko pale pale haijaongezeka.

Tufanye mipango ya umwagiliaji, tunakubali mia kwa mia lakini Wananchi wetu wakopeshwe hayo maji hata kwa gharama ndogo, walipie maji, hatutaki wawekezaji watoke kule kwao ardhi wameshaimaliza wanakuja kutumalizia ardhi yetu hapa; hiyo haiwezekani. Ardhi ya Watanzania na inatoka Tanzania. Tunazidi kuzaana, mimi nimeshazeeke sizai lakini wako vijana wanazaa wanaongezeka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa na naunga mkono hoja hii ya umwagiliaji, kitu tunachokataa ni hii hadithi ya uwekezaji, hawa wawekezaji wa nini? Wamechukua mashamba ya katani kule, hatujaona faida yoyote, wamechukua fedha benki na wengine wamekimbia, wamechukua mashamba ya Nkundi hamna kitu mpaka leo, Malonje hakuna kitu, sasa hawa wawekezaji mnawataka wa nini? Kapunga hakuna kitu. Leo wananchi wetu wamelima mpunga wamejaza



magodauni, hakuna pa kuuza kwa huu huu ulimaji mdogo mdogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwawezeshe hiyo *Irrigation* na naunga mkono hiyo Tume mia kwa mia, lakini ni wananchi wetu wenyewe. Hatukubali mgeni kuingia kwenye ardhi, nyie mnasema 80% ni wakulima, mtawapeleka wapi, wawe vibarua katika nchi hii? Mtaleta mzozo kama wa Zimbabwe hapa. Namuunga mkono Mugabe mia kwa mia. Nasi hatutaunga mkono mwekezaji. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy, rudia tena hapo hatujasikia vizuri.

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono Mugabe mia kwa mia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashangaa wanasema 80% ni wakulima, nani kafanya sense kuona 80% ni wakulima? Siyo kweli labda 35% au 40%, wote wako Dar es Salaam, Arusha, Mbeya kule wanauza vinguo nguo tu, wanalima wale? Mnataka na wananchi wa Rukwa msipofanya *irrigation* nao waje kuuza vichupi chupi Dar es Salaam? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, fanyeni *irrigation*, tuna mabonde mazuri kule Lwanfi, Korongwe, bonde la Rukwa, mtawezesha watu watakuwa hawana shida ya kuja kuuza vichupi chupi. Kwanza hawalipi hata kodi, nchi inarudi nyuma.



Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimeambiwa Kundi kaweka geti pale ushuru gunia sh. 10,000/=, wanataka kumpiga, gunia moja la alizeti, nchi gani hii jamani? Waoneeni huruma wakulima, wapeni maji walime wenyewe hao wawekezaji wa nini? Mnawaletea nini wawekezaji? Mmetuletea matrekta, ma-*powertiller*, sijui nini vyote ni vibovu, leo *powertiller* ziko ngapi zinalima? Mnatuletea pembejeo ya mbolea ya ruzuku haiendi kwa wakulima, toeni hela ya ruzuku ya mbolea iende kwenye maji, utampa mtu mbolea, utampa mbegu, lakini hakuna maji mazao yatakauka, unatia kibiriti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza ni maji, maji kila kitu kitastawisha, mbolea baadaye, nyie mnakazania mbolea ya ruzuku na mbolea yenyewe inachakachuliwa, nani atachakachua maji hapa? Atachukua maji akauze Zambia? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Muswada lakini hatukubali kumleta mwekezaji, wawekezaji ni wananchi wetu wenyewe watakwenda wapi? Leo mnasema hamna ajira, hata ajira ya kulima mnawanyang'anya, wawe vibarua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwamini sana Mheshimiwa Injini Chiza na Mheshimiwa Kighoma Malima, lakini hilo la kuleta wawekezaji, hapana! Rukwa hatukubali, labda Mikoa mingine Wazee, lakini Rukwa sikubali!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mizozo na magomvi ya kila siku na wafugaji, Mkoa wa Rukwa siyo Mkoa wa wafugaji, ni Mkoa wa wakulima, wametuvamia wafugaji tu.

Nimewaeleza wananchi wangu, mwananchi yeyote pale haruhusiwi kuuza shamba lake kwa vyovyote vile mpaka ashirikishe familia yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaambia akinamama pia kuwa, mwanaume kama anataka kuuza shamba mfukuze, ubakie na shamba, yeye akatafute shamba kwingine na akatafute mke kwingine, shamba ndiyo rasilimali ya wananchi wetu, hawana kazi, mmesema 80% mtawapeleka wapi na wanazaana kila siku. Kwa hiyo, hii *irrigation* naiunga mkono, lakini wawekezaji wawe ni wananchi wetu wenyewe, mnasemaje ndugu zangu?

**WABUNGE FULANI:** Sawa.

**MHE. ALLY K. MOHAMMED:** Niungeni mkono, ya mwekezaji ondoeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka wawekezaji tena acha Wazungu wawekezaji rangi nyeusi wamo humu nchini, ndiyo wabaya zaidi, wamechukua mashamba hawalimi maheka na maheka wamo humu. Wamemaliza mapori yote Rukwa, hata ardhi hawalipii, ile ardhi waliyochukua hawalipii Serikalini, mnakaa mnawa-charge kodi hawa wapiga debe, mtu kachukua heka elfu sita, heka elfu kumi na sita halipii hata kodi. Leo mnataka kuwaleta na wengine kwa mtindo huu kwamba, hatuna uwezo wa maji mnaleta na wengine tena watumalize, wananchi watabaki vibarua mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali hoja hii, lakini narudia tena kuwa, wawekezaji ni wananchi wetu

wenyewe, ni kweli *scheme* zilikuwa zinakawia kama kule Lwanfi, miaka mitatu wataalam mpaka watoke Morogoro, ndiyo wakafanye *study* kule, unawabembeleza, gharama kubwa, lakini wakiwa Sumbawanga au Namanyere inakuwa ni rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mabonde mengi na tunaunga mkono hoja, lakini kuleta mwekezaji Rukwa haiwezekani, wawekezaji wa Rukwa ni wana Rukwa wenyewe na hao wenye mashamba makubwa hatuwakubali, tutagawana kidogo kidogo ndiyo ajira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimpore mtu ardhi yake, ya Zimbabwe yanatosha na ndiyo maana Afrika ya Kusini inaogopa kumsema Mugabe, inajua na kwake kutatokea moto. Hawana ardhi, ardhi yote ni ya Wazungu mashamba mazuri wanachukua Wazungu na hapa itakuwa ni yale yale, mwekezaji anachukua pori kubwa na halihudumii, mwananchi akienda kule walenzi wake wanampiga mshale, lakini linakuwa pori miaka na miaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali mtengeneze Muswada hapa, tubadilishe, wenye mashamba makubwa wote waporwe ni mali ya Serikali, wapewe wanakijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli ni Ubunge tu, lakini bila Ubunge nakwambia ningehamasisha wananchi kuwaporwa watu waliochukua mashamba kinyume cha Sheria. *((Kicheko/Makofi))*

**MBUNGE FULANI:** Ni Ubunge tu!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Ubunge unanizuia tu, lakini sitakubali wananchi wanahangaika na mashamba, wewe umechukua heka elfu tano, elfu sita wanakutazama, ajira iko wapi? Mtu ana watoto hana ardhi, wewe umekumbatia ardhi. Waheshimiwa tunakubaliana, Muswada upite lakini cha wawekezaji *no*, wawekezaji wawe ni wananchi wenyewe na Rukwa hatutaki mwekezaji wa aina yeyote, akiwa mweupe, akiwa mweusi, akiwa mwekundu hatutaki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy akiwa mweupe kama wewe, akiwa mwekundu hapana.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uliza Namanyere, mimi sina hata heka mbili za shamba.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, huyo ndiye Mheshimiwa Keissy na tumemsikiliza mchango wake na akaamua kugeuza jukwaa hili la siasa akaanza kuhamasisha Bunge kumuunga mkono.

Sasa naomba nimwite mchangiaji wetu anayefuata ambaye ni Mheshimiwa Agripina Buyogera atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kidogo katika Muswada huu muhimu sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nikiri kuungana kabisa na Wabunge wale wanaokubaliana na kuundwa kwa Tume hii. Nakubaliana kuundwa kwa Tume hii, tatizo ni usimamizi wa chombo hiki tunachokiunda. Hili naomba kabisa Waziri wa Kilimo ni kaka yangu, ili kulitendea haki Taifa la Tanzania na kutujengea heshima wana Kigoma kwa elimu uliyonayo, asimamie Muswada huu, Sheria hii ili ahakikishe inazaa matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitisha Sheria nyingi sana katika nchi hii. Ukiona tunabadilisha Sheria kila siku, tatizo siyo Sheria, tatizo ni wasimamizi na watekelezaji wa Sheria hii. Leo tuna malalamiko mengi sana katika nchi yetu kuhusiana na ardhi, siyo kwamba Serikali yetu haina Sheria za Ardhi. Tuna Sheria za Ardhi nzuri sana ambazo zinatekelezwa kuanzia vijijini, lakini viongozi tuliowaweka madarakani ndiyo hao hao wanakwenda kuvunja Sheria hizo kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeunga mkono kuanzishwa kwa Tume hii kwa makusudi. Kule Jimboni kwangu nina miradi mikubwa sana ya umwagiliaji na nimekuwa nikiongea humu Bungeni, nikiishukuru Serikali kwamba, inapeleka pesa katika utekelezaji wa miradi ile ya umwagiliaji. Leo ukisema tuunde chombo cha kusimamia, kuhakikisha tunapata usimamizi thabiti ili wananchi wale waweze kunufaika na uzalishaji unaofanyika katika miradi ile, ni sahihi lakini yuko wapi msimamizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Wabunge walioonesha mashaka kuwa chombo hiki ambacho

tunataka kiundwe (Tume) kimepewa mamlaka makubwa ambayo inaonesha kabisa kutia wasiwasi kuwa, itakwenda kunyang'anya madaraka ya wananchi vijijini. Kama leo hii unaweza ukaipa Tume mamlaka ya kuchukua ardhi wakati wowote na ikatangaza tu kwenye gazeti ikiwa Dar es Salaam, hii ni hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kama Wabunge ni lazima tuishauri Serikali, irudi ikae chini na ipitie Muswada huu vizuri, iweze kurekebisha hivyo vipengele kwa maslahi ya Taifa letu. Mimi ni muhanga katika changamoto Jimboni, nina migogoro mikubwa sana ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikilalamika hapa, lakini bado haijafanyiwa kazi na ninatoa angalizo, Mheshimiwa Waziri hili analijua, nimekuwa nikilalamika humu Bungeni, tunapopitisha Tume hii isiende kuongeza migogoro badala ya kwenda kupunguza migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa nina wabembeleza sana wapiga kura wangu, nawaambia Jimbo lile linaongozwa na Mama, kwa hiyo, mpaka nitakapofikia hatua ya kusema sasa tumekata tama, Serikali haitaki kutusaidia, yaliyotokea sehemu nyingine yatatokea ndugu zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuwe makini katika kuandaa Sheria hii. Nayasema haya kwa nini? Leo hii Kigoma tuna shamba la mradi wa Kilimo Kwanza ambayo ni Sera ya Taifa. Katika Mkoa inayozalisha chakula, ni pamoja na Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile shamba la mradi wa Kilimo Kwanza limo Jimboni kwangu Kata ya Helimushingo, Kijiji cha Kigadi, lakini leo hii Mkuu wa Wilaya amekaribisha wageni wenye mifugo, amekwenda kuwakabidhi shamba lile na kuwafukuza wale watu waliokuwa wanalima wakisaidiwa na Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vitu vya kushangaza, Serikali ipo, shamba lile ni la Serikali, Halmashauri kwa kutumia fedha za wananchi, tumetoa pesa kulilinda shamba lile kwa ajili ya nguvu kazi ya Taifa, leo mtu anachukua watu wachache anawakabidhi shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoongea, Halmashauri imeunda Kamati kwenda kufuatilia mgogoro huu, wamekwenda na wamekuta watu kwenye mradi huo na wamechukua maelezo, matokeo yake wameleta taarifa katika Halmashauri kumwambia *DC* ashughulikie hilo. *DC* anasema kuwa Kamati ya Ulinzi na Usalama italifanyia kazi tulieni. Kwa hiyo, tunapozungumza, Serikali ni lazima msikie ndugu zangu, mkiona Wabunge tunapiga kelele, haya ndiyo yanayosababisha matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kwa kuwa kilimo ndiyo nguvu kazi ya Taifa na ndiyo tegemeo la Watanzania walio wengi, hii Tume watendaji Mikoani waondolewe, hatimaye tuanzie uwakilishi kwenye Halmashauri kwa maana ya Wilaya, ambapo tutakuwa na chombo cha Taifa ambapo tutakuwa tunawasiliana pale, ikitoka pale inawasiliana na Halmashauri moja kwa moja ili kuweka mawasiliano mazuri, kuondoa ukiritimba hapa katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea machache, naomba nisisitize, miradi ya Rungwe Mpya, miradi ya Titye, Mheshimiwa Waziri watakapokuwa wanajumuisha ni vizuri watueleze kuwa hii Sheria itawanufaisha vipi kwa sababu ni watu ambao ni waanzilishi wa muda mrefu. Pia kwa kuwa, Jimboni kwangu nina maporomoko mengi ya maji na kule Kigadi tunategemea kwenye bonde lile kuanzisha kilimo cha miwa kwa ajili ya kujenga Kiwanda cha Sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama walivyokuwa wakizungumza Wabunge wenzangu kwamba yapo maeneo ambayo tumeshatangulia kuanza uzalishaji huu, Sheria inatukuta tuko kazini, ni pamoja na Kasulu Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nataka nichangie hayo, bila kupoteza muda nikushukuru sana na kwa kuwa mambo mengi yameshachangiwa ninaomba niwashukuru kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Agripina Buyogera. Waheshimiwa Wabunge baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Agripina Buyogera, sasa nitamleta kwenu Mheshimiwa Riziki Lulida na atafuatiwa na Mheshimiwa Yussufu Hussein.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuwa mmojawapo wa wachangiaji wa hoja ambayo iko mezani.



Mheshimiwa Mwenyekiti, napata kigugumizi, hoja ni nzuri, yenye mashiko, lakini inanitia wasiwasi, je, Mkoa wa Lindi maana nazungumzia Mkoa wa Lindi maana ndiyo Mkoa wa mwisho kwa maendeleo, Mkoa wa Lindi itatusaidia kwa haya nitakayoyazungumza na namwomba Mheshimiwa Waziri na Mawaziri husika wengine wanisikilize kwa makini na wakishanijibu hii hoja nitaiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutembea ni kuona mengi Kamati ya Nishati na Madini ilituchukua, ikatupeleka Malaysia, tukaona maendeleo ya Malaysia, kuanzia kilimo, madini, utalii, kwa kweli wale watu wameamua kupiga hatua na tulipewa elimu ya wiki moja, kutuonesha kuwa kwa nini walipiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu waliheshimu ardhi yao, waliheshimu utu wao, sisi hapa tunaheshimu wageni, hatuwaheshimu Watanzania. Tena Mtanzania yuko tayari kumtoa Mtanzania mwenzie ambaye angeweza kufaidika na kuhakikisha mgeni anakuja kufaidika kwa maslahi yake binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku najiuliza Mkoa wa Lindi ni eneo zuri kwa kilimo; tuna mabonde makubwa ya Mbekenyela, Ruangwa, Kiyope, Milola, Matandu na Mbwemkuru, sasa hivi ile mito tuliyokuwa tunaitegemea imekauka. Ni kwa nini imekauka? Usimamizi Wizara ya Mazingira haupo, usimamizi Wizara ya Mifugo haupo na sasa hivi maji hakuna na vyanzo vyote vimekatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Telele amenifundisha vitu kuhusu Wamasai wanavyoheshimu

vyanzo vya maji Umasaini. Mmechukua mifugo mmepeleka Lindi, tunakubali tunataka tushirikiane katika mifugo lakini hakuna malambo, hakuna majosho wamekimbilia katika vyanzo vya maji na maji yamekauka je, umwagiliaji huu Lindi utasaidia nini? Watamwagilia nini Lindi, wakati mito yote imekauka, vyanzo vya maji vimekauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingia katika *Google Earth* unakuta kuna *Lake Mkoa*, lakini leo *Lake Mkoa* ni historia, hakuna maji. Wafugaji wamekwenda katika *Lake Mkoa* wameweka mifugo, ni pakavu hakuna maji, Kijiweni hakuna maji, Mvuleni hakuna maji, Kilolambwani hakuna maji, Mwang'ole hakuna maji, sasa tutaishije kama hatuna maji? Watu wanahitaji usafi, lakini maji hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea wafugaji hakuna majosho wala malambo mifugo yao inakunywa nini? Sasa utasema watu wa Kusini hawataki ng'ombe, siyo hivyo! Utaratibu na usimamizi ni mbovu. Naomba Waziri mwenye dhamana ya Mifugo, Waziri wa Mazingira, Waziri wa Kilimo na Waziri wa Ardhi wakaliangalie hili suala ili lilete tija na ili umwagiliaji uweze kufanya kazi katika Mkoa wa Lindi, la sivyo tunatwanga maji katika kinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna suala la *early burning*, wanaanza kuchoma moto mapema ili nyasi ziote, wafugaji wapate nyasi nzuri kwa mifugo, ile miti ambayo tulikuwa tunaitegemea imekwisha, sasa kama miti inakwisha, tunategemea tutapata wapi mvua, kilimo endelevu kitapatikana wapi? Sasa je, hizi sera mbona zinakinzana, watalaam wanaliona hili au hawalioni?

Mmewatoa ng'ombe lhefu, sasa hivi ikifika usiku wanaletwa ng'ombe kwa ajili ya kuwapeleka Lindi kwenda kunenepesha ili wasafirishwe kwenda Dar es Salaam, utaratibu haufuatwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sielewi mpaka inafika mahali najiuliza, ni nini? Nasema tena, nitaunga mkono kama usimamizi wa maeneo ambayo tunahitaji yapate maji, utakuwa ni wa ushirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tuna Wamachinga Dar es Salaam, wananyanyaswa kuliko hesabu, wakitembea na nguo wanafukuzwa, lakini maeneo yale kule watakwenda kufanya nini? Pesa nzito, *fund* za *SAGCOT* Lindi haipo wala Mtwara haipo. Leo watalima nini hata kama ukileta maji ya umwagiliaji, hela hazipo, *SAGCOT* imepelekwa maeneo tofauti. Tulikuwa na Mtwara *corridor* hata haijulikani imepotelea wapi, wakati Mtwara *corridor* ilishirikisha mikoa hiyo yote, lakini sasa hivi *SAGCOT* Lindi na Mtwara haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale Wamachinga waende wapi, nataka Bunge lako Tukufu liniambie wale Wamachinga niwapeleke wapi, wakikaa Dar es Salaam wanafukuzwa, wanapigwa, wananyanyaswa, Lindi hakuna kitu cha kukimbilia, hakuna shule, hakuna hospitali, *fund* tunazopelekewa ni ndogo. Tufikie mahali ushirikishwaji wa ardhi, mifugo, mazingira waliangalie. Tusije hapa tunaleta sera ambazo hazina mashiko katika utekelezaji. Usimamizi bado haujawa mzuri, tungekuwa na usimamizi maendeleo yangepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejifunza jambo la pili Malyasia, wao hawakuwapa Wawekezaji ardhi kukaa nayo miaka 90 ya huku, mwekezaji yule hamtaki Mtanzania kuwa mshiriki mwenzake, anakuja na mwenzie, kama akija Mchina, basi watakuja Wachina 500 katika uwekezaji. Kenya wenzetu tumekwenda kuona *geothermal*, kuna wataalam watano wanasimamia mradi mkubwa wa mabilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeeomba katika kijiji, wataalam ambao wanataka kufanya uwekezaji wawalete wataalam, wakae na wananchi, wakiondoka pale wananchi wapate utalam wao tuendelee, masuala ya kutunyang'anya ardhi hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnahitaja ardhi ya ukubwa wa 80.4, lakini kuna maeneo mengine ni ya wanyama, mapito ya wanyama mmeyachukua mnataka kuyaingiza kwenye ardhi, haipo! Haiwezekani hata mnyama nae ana haki ya kuishi katika pori lake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuja wawekezaji wanachukua ardhi kama madalali. Nataka nitoe mfano wa Mavuji, amepewa mwekezaji heka 34,000 amefanya fujo, amekata magogo, hakulima hata kidogo, Mavuji katika lile bonde, amefanya uchimbaji, amemaliza wanyama waliokuwa wanapita katika mapito yale na amekimbia kwa kuona aibu. Leo lile eneo linauzwa na madalali kwa dola bilioni saba *point something*. Unataka kusema nini hapa, utakuwa una haki ya kujisikia una raha katika nchi yako?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wawekezaji wanachukua maeneo kwa ajili ya udalali, anachukua eneo kijijini bure saa nyingine anawapa watu S. 25,000/=, anapewa heka 20,000. Akitoka pale mwekezaji ameshakuwa na kila kitu anaingia kwenye udalali, akitoka pale kwenye udalali anayekwenda kumwuuzia yule wa pili anakuja mbogo, toka wewe huna haki, mwananchi wa pale anabakia kuwa mpweke, hana thamani katika nchi yake, hana uwezo mwingine wowote, ni kumtoa tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kila kijiji, kila Kata hasa katika Mkoa wa Lindi, uingie ubia na uwekezaji, lakini katika kuendeleza kwa muda mfupi wa miaka mitano, wananchi wangu wakishajua, wawekezaji waondoke, hatuwezi kufika mahali ambapo kila eneo linachukuliwa, sisi tunabakia na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mmoja sasa hivi anakimbilia Lindi kwa ajili ya kukamata ardhi, si kwa sababu anaitaka ardhi ya Lindi, anakamata madini, anakamata maeneo oevu, baadaye anakwenda kuyauza nje, haiwezekani! Tufike mahali tujiulize tumeifanyia *research* hii kazi, utafiti wa kutosha tumeufanya, ili angalau tusije hapa tukawa kama Zimbabwe, likailitea aibu nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea naonekana kama ni mropokaji, lakini naomba usimamizi mbovu, hatupo *committed*, tumefikia mahali ambapo tunajitia mashaka hata sisi wenyewe hatuaminiani. Ukiona mradi unaanza kuukataa kwa kujua kama ule uliharibika je, huu utaweza. Kama huu hauwezekani, basi tufike mahali kwanza tusimame, tujirekebishe ili tuweze kwenda. Lakini kama kazi

enyewe itakuwa tunaiuza ardhi, watu wanakwenda kufanya udalali Ulaya, nchi itakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaingia ndani ya ndege unaona watu walivyojazana kuja kukamata fursa Tanzania, lakini mwenye fursa yupo chini amekuwa kama boga, boga anasuka mkeka, lakini mwenyewe amelala chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni ngumu na inahitaji kusimamiwa na watu wenye mshiko, tunasema CCM ndiyo wenye makosa, lakini ndani ya Serikali kuna watendaji wanaangalia maslahi, hawajali Chama, si CCM, wala si CHADEMA, wala siyo NCCR, ni Watanzania ambao hawaitakii mema Tanzania, msikiseme Chama kimoja. Msinyooshe mkono kule, kwanza jiulize na wewe msafi?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tufikie mahali nyumba ni moja Tanzania ambayo inataka ijengwe na kila Mtanzania, nawaomba Watendaji, Wabunge, Wanasiasa na wengine wote tuwe kitu kimoja ili tuweze kulisukuma hili gurudumu tuweze kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupeleka hizo hoja za *SAGCOT*, je, Lindi tutapata *SAGCOT*, maendeleo ya kilimo Lindi yatakwenda? Je, mifugo mnayoipeleka Lindi mnaisimamia au imekuwa kama kichaka? Kama si hivyo naiogopa hii hoja, kwangu inakuwa nzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Riziki Lulida. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Chomboh.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha jioni hii kusimama hapa. Pili, nikushukuru Mwenyekiti kwa kuweza kunitoa nje leo kwa mara ya kwanza katika Bunge hili.

Tatu, uniwie radhi niwashukuru wapiga kura wangu kwa kunichagua na kwamba niwawakilishe ndani ya Jimbo hili. Nawashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano walionipa na kwa muda mfupi ambao nipo Bungeni nimekuwa na marafiki wengi wa vyama vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo sasa nichangie Muswada huu ambao upo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati unachangia asubuhi ulisema kwamba tuna hofu na kwa nini tuna hofu? Niseme tu kwamba, ni kweli tuna hofu kwa sababu kila mchangiaji hapa ameonesha hofu yake aliyonayo. Mimi nina miaka hamsini sasa...

**MWENYEKITI:** Miaka 50 kiumri?

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Aaa. (*Kicheko*)

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tokea nchi hii inapata uhuru zinazungumzwa hapa, nyimbo nyingi kuhusu kilimo, tuliambiwa nchi hii ni ya wakulima na wafanyakazi, kilimo ni uti wa mgongo, siasa ni kilimo, kilimo cha kufa na kupona, kilimo ni uhai, lakini hadi leo kilimo bado kinakuwa ni tatizo ndani ya nchi hii. Inabidi sasa tujiulize, tatizo ni nini? Kabla ya kupitisha Muswada huu tunatakiwa tujiulize tatizo ni nini kilimo chetu kikawa hakimnufaishi Mtanzania na tunaambiwa nchi hii itakuwa ni ya wakulima na wafanyakazi? Pia kilimo hakimnufaishi Mtanzania kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunapaswa tuwe wakweli na ile hofu inakuja kwa sababu Wabunge wengi hapa walikuwa wanachangia na kusema huu Muswada ni mzuri, masuala haya ya kilimo ni mazuri. Hakuna Mtanzania leo ukimwambia atakataa kwamba suala la kilimo cha umwagiliaji kitamkomboa Mtanzania, hakuna ambaye atakataa. Lakini Wabunge wengi wanachangia wanakwambia, wawekezaji wasije kwenye Jimbo langu, wasije kwenye Wilaya yangu, wasije kwenye Mkoa wangu, ina maana hapa kuna *kifukumkunya*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wasingeweka hofu kwamba, wawekezaji wasiende kwenye maeneo yao, ila kuna suala hapa kwamba, inawezekana pengine Muswada au sheria hii inaletwa kwa sababu kuna



wawekezaji wanataka kuja kuwekeza, sasa hatuna sheria, kwa hiyo, tulete sheria ili wawekezaji waje wawekeze, tuna hofu hapa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi hapa wanatoa mfano hata wa Zimbabwe. Zimbabwe inapata uhuru tayari nimeanza kuwa na fahamu, inasaidiwa hapa ili ipate uhuru, lakini leo tunaambiwa kwamba imeendelea kwa kilimo lakini sisi Tanzania wanatuacha hapa! Sasa tutaendelea kuzisifu nchi nyingine, kuzitaja nchi nyingine zinaendelea sisi tunabakia hapa mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tabia tuliyonayo ya kukaa ndani ya Bunge hili, tunapanga mipango mizuri, tunapitisha sheria nzuri, wenzetu wanatusikiliza na wanakuja wanazichukua sheria hizi au mipango yetu wanakwenda kuifanyia kazi kwao wanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hapa Ethiopia wamekuja kuchukua mpango mzima wa kilimo kwanza, wameanza kazi, baada ya muda mfupi tu wao watakuwa wapo mbele sisi wanatuacha hapa! Tutaacha lini hii tabia ya mpiga ngoma mjinga? Maana tumekuwa na tabia ya mpiga ngoma mjinga mwerevu *akobeaye!* *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Watanzania sasa tubadilike na tuone kwamba nchi yetu inakwenda mbele kwani hii nchi ni ya nani? Kuna mgeni humu? Kama kuna tatizo kwa nini halielezwi waziwazi likatafutiwa ufumbuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana watu tunapozungumzia suala hili, lakini hatuliangalii, kilimo hiki kitatukomboa kweli, lakini tupo tayari? Ni Wabunge hawa wamesema hapa, maana yake kilimo cha *irrigation* ni sawasawa na unapofuga vifaranga vya kuku, vinahitaji uwe na umeme, uwe na maji, uwe na chakula kwa wakati na usafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kilimo cha *Irrigation* ambacho tunasema tunakianzisha, Wabunge hapa wanasema kwamba inafika muda wanataka kupanda, mbolea ya kupandia haijafika huko, inafika wakati sasa wanapalilia, ndiyo mbolea ile ya kupandia inafika huko, inafika wakati wa kuvuna ndiyo madawa ya kupalilia yanafika huko. Tunakwenda kwenye *irrigation* kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tujipange na tunapojipanga tunafanya kwa maslahi ya nchi yetu. Leo miaka hamsini umri wangu nchi hii tayari imepata uhuru bado sisi tuna tatizo la chakula, tunaomba chakula. Asilimia 60 ya ardhi yetu na mamilioni ya hekta ya ardhi yaliyotajwa hapa, sisi hatunufaiki nayo, tunakwenda kuomba chakula! Inazungumzwa hapa na inasikitisha unaambiwa sehemu chakula kipo, lakini tunaagiza mchele kutoka nje, ina maana hata hizi taarifa hapa hatupeani vizuri, sasa tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu inakuja hapa, isije kuwa kuna wajanja wachache wanataka kuja kuwekeza kwenye hiki kilimo, lakini hamna sheria, basi hebu wekeni sheria ili tuje tuwekeze, ndiyo hii ikaja. Tuwe makini sana katika hili. Sasa tunahitaji kubadilika na ni lazima tubadilike! (*Makofi*)

Mhehsimiwa Mwenyekiti, kuna suala la fedha, nilikuwa najiuliza kama bajeti ya Wizara ya Kilimo kila mchangiaji anasema ni dogo, bajeti ya Wizara iongezwe na *Irrigation* ni kilimo ambacho kinakula fedha kweli kweli, hii fedha itatoka wapi? Hili napata wasiwasi labda Waziri atakapokuja atatuambia hivi vyanzo vya fedha vitatoka wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine imezungumzwa hapa suala la Tume ambayo ndiyo itasimamia kilimo hiki na inakwenda kufanya kazi huko na Halmashauri, sasa tumejipanga vipi ili kuondoa hizi *contradictions* baina ya Tume na Halmashauri, baina ya Tume na Wizara nyingine kama Wizara ya Maji na kadhalika ingawa Wizara ambayo mimi niko kwenye Kamati, Wizara ya Nishati na Madini ndiyo imesahauliwa kabisa hapa. Lakini sawa haya ni matatizo ya kibinadamu yatarekebishwa je, tumejipanga vipi kuyaondoa haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atupe mfano wa wapi tumefanikiwa katika masuala haya ya kilimo ili tushawishike, tusiogope na ile hofu yetu iondoke ya kwamba, kuna wajanja wanataka kuja kuchukua hili eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 3(6), zimetajwa Wizara au Taasisi ambazo zitakuwa zinahusika, Wizara ya Nishati na Madini imeachwa, hadi leo bado tuna tatizo la upungufu wa umeme. Tumeondoka Dar es Salaam juzi kuna hilo tatizo baada ya ile *shot* iliyotokea pale Ubungo na tunapokwenda hapa kwenye suala la *irrigation*

ambapo maji yatatumika na hawa watu hawajashirikishwa, hatuongezi tatizo lingine hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake itakuwa tunatatua tatizo la chakula, tunatatua tatizo la *irrigation*, tunaongeza matatizo mengine je, hapa tumejipanga vipi? wahusika hawa hawajashirikishwa labda wangetupa majibu kwamba labda ndugu zetu wa Kusini kule wataturuhusu ile gesi yao iingie hapa. Nadhani hapa panahitaji kuangaliwa vizuri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Mheshimiwa Mnyaa aliieleza vizuri Ibara ya Tatu sehemu ya pili kuhusu yale marekebicho, lile neno mpango wa Kitaifa, kwa hiyo, itabadilishwa, sijui kama itabadilishwa lakini nadhani ingekuwa vema ibadilishwe ili kuondoa haya maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naiomba Serikali kwamba, sasa ni lazima tubadilike na tuwe wawazi. Kama kuna tatizo basi tuelezane ukweli ili tulichangie kwa uwazi kabisa na lisiwe linaleta manung'uniko. Manung'uniko haya ambayo yanazungumzwa yatasababisha matatizo huko mbele tunakokwenda. Kwa hiyo, tushirikiane, tuwe wawazi, haya masuala yawekwe bayana ili tuweze kufikia yale malengo tuliyoyakusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kizazi hiki ambacho sisi tumezaliwa katika uhuru, hatutakubali tena kuona nchi za wenzetu tuliopata uhuru pamoja kama Kenya wanatuacha kwa hatua kumi na nane zaidi sasa hivi, wapo mbele na sisi tupo hapa hatutakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizi hadithi za nyimbo nyingi, usanii huu wa maneno mengi ambapo Watanzania ni wazuri sana katika kujenga hoja na kuzungumza, lakini utendaji wetu unakuwa mbovu, nadhani sasa umefika wakati tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nakushukuru kwa kunitoa nje siku ya leo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, ingawa leo hiyo misamiati ya Kizanzibari imetuacha hoi kweli. Maana yake tupo ndani ya ukumbi wa Bunge, wewe unanishukuru kwa kukutoa nje, sasa kazi kweli. Lakini tutaendelea kuelewa taratibu. Nilifikiri unanishukuru kwa kukupa nafasi ndani, wewe unanishukuru kwa kukutoa nje ya ukumbi wa Bunge. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea hiyo ni misamiati ya Kizanzibari, nilimwita Mheshimiwa Chomboh lakini simwoni kwenye kiti chake, basi naomba nimwite Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ambayo imebeba hatima ya Watanzania, lakini pia imebeba hatima ya ajira kwa vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na bila kutafuna maneno nasema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa kuthubutu na kuona umuhimu wa kuwa na Sheria hii ya Umwagiliaji badala ya kuendelea kuishi kwa kuongozwa na Sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme wazi na siku zote nimekuwa mkweli, inanisikitisha sana humu ndani anaposimama Mbunge anasema hakuna umuhimu wa kuwa na Sheria katika nchi hii, inanisikitisha sana na nitatoa mfano kwa sababu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge wenzangu wote humu ndani wote ni mashahidi. Tumeona kwenye baadhi ya sekta mambo mengi yakishindwa kwenda kwa sababu ya kukosa Sheria ya kusimamia sekta husika. Kwa mfano, tumekuwa tukipiga kelele kwamba Sera ya Afya inayosema matibabu kwa mwanamke mjamzito, mtoto wa miaka mitano na wazee yawe bure, imeshindikana kutekelezeka kwa sababu hakuna sheria ya kumbana mpeleka huduma na mtoa huduma kuhakikisha Sera hii inatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo hii Mbunge ambaye kazi yako ni kutunga Sheria, lakini pia unatoka katika maeneo yenye mito na mabonde ambao mpango huu utakwenda kufanya kazi, unakuja kutwambia eti hakuna haja ya kuwa na Sheria katika sehemu muhimu inayosimamia suala zima la kilimo cha umwagiliaji. Inanishangaza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inaonekana ni jinsi gani tusivyojua wajibu wetu, tunakwepa majukumu yetu. Kazi ya

Mbunge ni kutunga Sheria, kama kuna matatizo, fanya marekebisho ili nchi i-move. Haiwezekani Bunge likawa sehemu ya kukwamisha Sheria, kazi ambayo imekuleta Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimeshangaa, Mbunge anasema Serikali tuahirishe Muswada tuache kutimiza wajibu Kikatiba wa kutunga Sheria kwamba imeleta *amendment* nyingi na yenyewe pia inanishangaza sana. Kazi yetu sisi ni kupitia yale marekebisho yaliyoletwa na Serikali kuona tunatakiwa turekebishe wapi. Kuona marekebisho gani yanafaa na kuona marekebisho gani hayafai kama Mbunge. Hiyo ndiyo kazi ya Mbunge, lakini si kukimbia kazi uliyopewa kwa mujibu wa Sheria na wala si kukataa kutimiza wajibu wako, ndiyo kazi yetu. Serikali imeleta marekebisho tuyafanyie kazi *that is why we are here*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesema naunga mkono na naamini pia Mheshimiwa Chiza utanijibu haya ambayo vijana wenzangu wamenitumia *message* kutoka Karukekere, kutoka Mgeta kule Bunda, kutoka Igunga, kutoka Kilombero na maeneo mengine. Wanasema, wameshindwa kunufaika katika sekta ya madini, wameshindwa kunufaika na maeneo mengine. Akili yao yote mbali na changamoto ya ajira waliokuwanayo wanaamini watanufaika na ardhi yao na watanufaika na ardhi yao kwa ajili ya ku-*invest* kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajua wana hekta milioni 29 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na wanaamini

watanufaika kupitia kilimo cha umwagiliaji na namshukuru Mungu leo umeleta Sheria. Swali lao wanasema je, Sheria hii itawanufaisha wazawa? Itawanufaisha vijana ambao wameamua ku-*invest* kwenye kilimo au Sheria hii itaendelea kuwalinda wawekezaji na wao kuwa manamba katika nchi yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwamini sana Mheshimiwa Chiza, naamini ukakasi huu wa vijana wa Taifa hili ambao ni zaidi ya asilimia 60, leo hii atatoa majibu na wataona uhalali na haki ya Bunge hili Tukufu kutunga Sheria hii ambayo itakwenda kuwasaidia Watanzania wanyonge, itakwenda kuwasaidia vijana ambao wameamua kujiajiri wenyewe kupitia sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa Mheshimiwa Chiza na katika hizi hekta milioni 29 na wenyewe watapata zile *prime area* ambazo wamezoea kwenye kilimo kuona wanapewa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kuwapa kipaumbele vijana na isije ikageuka wao wakawa vibarua tu kwa wawekezaji ambao watakuja ku-*invest* kwenye sekta ya kilimo na mmesema mlikubaliana kwenye *SADC*, lakini mjue saa hizi wako *aware*, wanajua kabisa Tanzania wana ardhi nzuri, Tanzania wana mito na mabonde na wenyewe ujue wana uchu na ardhi yetu. Pia si wengi ambao wanatakiwa mema Taifa letu. Naomba Mheshimiwa Waziri suala hili aliangalie kwa umuhimu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia sina tatizo la kuundwa Tume. Unapoanzisha *project* kubwa kama hii, ni



lazima kuwe na chombo ambacho kitasimamia. Sasa swali kile chombo kinafanya nini? Hilo na lenyewe pia ni jambo la msingi. Kwa sababu tumekuwa na Tume nyingi sana na wewe pia Mheshimiwa Mwenyekiti umeonesha wasiwasi wako wakati unachangia kwamba tunaweza tukawa na dhamira, lakini usimamizi ukawa mbovu, lengo likashindwa kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana kwa Mheshimiwa Chiza, hii Tume ifanye kazi ya kuleta mabadiliko kwenye Sekta ya Kilimo kitachoweza kuwanufaisha Watanzania, kitakachowafanya Watanzania wawe na imani na viongozi wao. Tusipokuwa makini Tume hizi hazitakuwa na tofauti na Tume zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu hivi karibuni tulipitisha hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla, mpango maalum wa kusaidia vijana mbali ya kwamba kulikuwa na mipango mingi tu na tukasema kuna uhalali wa kuwa na hicho chombo na ndivyo hivyo hivyo kuna Idara, kuna nini, lakini si mbaya kama kutakuwa na chombo maalum kitakacholeta ufanisi na kazi ionekane na Wabunge tusijute kwa nini tulikubali kuundwa kwa Tume hii. Kwa hiyo, hayo pia ni mambo ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Muswada huu kuna vipengele vingi sana vya uteuzi. Nadhani mambo ya uteuzi, uteuzi, uteuzi yamepitwa na wakati. Acha watu washindane kwa *professions* zao. Tuna Watanzania wengi wana uwezo, tusipende kujifungia kwenye kachumba kadogo. Hebu tutanue wigo tuweke ushirikishwaji, watu waombe kazi waajiriwe kwa vigezo vyao. Haya mambo ya

uteuzi haya ndiyo mambo ya kuanza kuuziwa mbuzi kwenye gunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona kuna haja ya msingi ya kuwepo na uwazi, mwenye sifa aombe na apate kazi kutokana na *profession* yake. Pia naamini katika mpango huu vijana wengi sana watapata ajira, tunaamini *SUA* kuna wataalam wengi pale wa kilimo na siamini kwamba kutakuwa na ujanja ujanja katika kuhakikisha vijana wanapata ajira. Hilo pia ni jambo lingine la msingi ambalo nimeliona kwa sababu naamini kutakuwa na Maafisa Umwagiliaji huko kwenye ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kipengele kile cha adhabu, Wabunge wengi wamekilalamikia humu ndani. Kweli adhabu ile ni ndogo sana kwa mtu ambaye anataka kuhujumu mradi mkubwa wa namna hii ambao una thamani kubwa katika nchi yetu na tumeona adhabu za namna hizi ambazo zina *option*, watu ambao watakuja ku-*invest* hapa ni watu wenye hela, hawawezi kushindwa kulipa milioni mbili. Kwa hiyo, watu watakuwa wanafanya makusudi, anajua ana uwezo wa kulipa milioni mbili na mwisho wa siku mambo yasiende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo la msingi sana na nimeona hata kaka yangu Mheshimiwa Mpina pale amelizungumzia kwa mapana yake, nisingependa kwenda *in deep*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kitu kingine Wabunge wengi wameonesha wasiwasi wao katika kifungu cha 17 na 18. Mheshimiwa Waziri na hapa pia anatakiwa

apaangalie kwa umuhimu wake. Suala la ardhi unazungumzia uchumi wa Mtanzania, unazungumzia rasilimali pekee ambayo Mtanzania anajivunia nayo kwa sasa hivi. Hapa ninaona kuna uwingiliano mkubwa wa madaraka na utaleta mgogoro mkubwa na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa ni vyema Mheshimiwa Waziri akaangalia kwa kina hiki kipengele, ni hatari, Watanzania watanyang'anywa ardhi yao, bila kuwa makini mtawapa wawekezaji na wengine watashindwa ku-*invest* watakaa na mapori ambapo Watanzania wadogo wadogo wangeweza kupewa na wenyewe waka-*invest* na wakaondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kipaumbele wapewe Watanzania wazawa katika ku-*invest* kwenye kilimo. Watanzania wamechoka kuona wimbo wa wawekezaji, wawekezaji, wawekezaji uchwala ambao wanakuja, wanahodhi maeneo na wanashindwa kuwekeza. Hilo hata mimi sitakubaliana nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vijana wengi, tumepitisha bilioni 16. Nadhani mkikaa na Wizara ya Vijana mkaona ni vijana wangapi ambao wameweza kukopeshwa ku-*invest* kwenye kilimo na mkawasaidia, naamini hakutakuwa na haja ya mwekezaji kuja ku-*invest* hapa na wazawa watawekeza na watanufaika na ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo mambo ya msingi ambayo nilikuwa nataka kuyasisitiza. Tunaomba, tunaomba Mheshimiwa Waziri, Watanzania kitu pekee ambacho wana

imani nacho, kitu pekee ambacho wanaamini kitawatoa katika wimbi la umaskini ni ardhi. Wapewe *priority* ya kuhakikisha wanawekeza na kuhakikisha wananufaika na huu mradi wa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naona na muda umekwisha, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Ester Bulaya. Mheshimiwa Chomboh!

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu jioni hii. Lakini pia kunipa nafasi ingawa mara mbili tatu umenita nilikuwa na dharura kidogo. Sasa hivi niko tayari kutoa mawazo yangu katika Muswada ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Naungana na wenzangu ambao wameunga mkono. Pia naamini na wale ambao waesema hawaungi mkono si kwa nia kwamba kweli hawaungi mkono, isipokuwa ni katika kuboresha tu na katika kuonesha ule upungufu ambao wanaona labda upo na kuwezesha Serikali ichukue hatua ya kuboresha Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuliko yote nasisitiza usimamizi na utekelezaji wa hii Sheria na yale ambayo yote ambayo tunakubaliana au yaliyokusudiwa katika Muswada huu. Katika watu waliobahatika ulimwengu huu, dunia hii kuwa na ardhi nzuri Tanzania ni mojawapo. Tuna ardhi nzuri,

tuna maji, tuna mabonde, kiasi ambacho ni nchi chache sana duniani zenye bahati kama hii. Lakini kwa bahati mbaya sana kwenye miti hakuna wajenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejaliwa na Mwenyezi Mungu, lakini kwa kipindi kirefu sana hatukuiona tunu hii tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, ni namna gani tunaweza tukaitumia kwa vizuri kwa maslahi ya watu wetu na nchi yetu kwa jumla. Leo bahati nzuri sana au kwa sasa tumeanza kushtuka. Hiyo ni kheri, tushukuru Mwenyezi Mungu kwamba tumeanza kugutuka, maana yake kitu kibaya ni kule kwamba hata kushtuka mtu hashtuki, anajiendea tu lakini Mungu kaleta kheri yake, tumeshtuka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumeshastuka basi tushikamane, tushirikiane na tufanyeni kweli kwa kuyatekeleza na kusimamia kwa uhakika kabisa yale ambayo tunakubaliana. Narudia kusema, jambo zuri lote lile linahitaji kujipinda na kujitahidi na kuhangaika na ndiyo baada ya matokeo yake tutakuja kupata raha na hakuna anayekataa raha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujitahidini ndugu zangu, tunatunga Sheria, lakini usimamizi ndiyo tatizo letu na utekelezaji ndiyo tatizo letu. Kuna hii dhana iliyopo sasa hivi kwamba, matokeo makubwa sasa. Tumeanza kuona baadhi ya Mawaziri wanajitahidi kuonesha kwamba kweli wanataka matokeo sasa. Basi na katika kilimo tujitahidini kusimamia ili tuone matokeo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kitu cha kushangaa kabisa kwamba Watanzania katika baadhi ya mikoa wanalia njaa au wana matatizo ya njaa, ni aibu. Lakini si tatizo la mtu mwingine, ni tatizo letu wenyewe, adui wetu ni nafsi zetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi nashauri tunapokuwa tunapanga mipango mizuri ya kilimo tutegemee kwamba tutavuna vizuri. Tujiandae basi na masoko lakini pia tujiandae na maghala ya kuweza kuhifadhi mazao hayo. Tujiandae na miundombinu ya kuweza kufikisha bidhaa zetu katika masoko. Isije kuwa tumeshalima mazao yanaozea shambani. Hiyo itakuwa sasa siyo akili ya kibinadamu sijui ni ya nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeshajaliwa na tukajitahidi na tukafanya, bidhaa zimerundikana. Hakuna pa kuhifadhi, hakuna soko la kuuza, matokeo yake ni kwamba itakuwa ni kazi bure. Tujitahidini sasa, tumeanza kutunga Sheria hii na Sheria itatekelezwa na itekelezwe kweli kwa usimamizi thabiti tutafika. Lakini cha muhimu kuliko yote tutauza wapi, tutapelekaje chakula hicho kwenye masoko, masoko yako wapi, tujiandae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwetu kule Visiwani kwa asilimia kubwa sana tunategemea sana chakula kutoka huku. Hatuna ardhi kubwa. Sasa ndugu zetu huku mkianza tena kuwa hamlimi tutakufa wote, sisi angalau ukisikia kule kuna njaa, basi ni kwamba hakuna mchele tu, hata kukiwa na muhogo, lakini mradi hakuna mchele, basi Zanzibar kuna njaa. Kwa hiyo, tulimeni, tusaidiane kulima, lakini pia

tuhangaikeni na masoko, tujue wapi tutakwenda kuuza vitu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo sina zaidi ya hayo, isipokuwa ni kusisitiza tu utekelezaji wa Sheria tunazozipanga. Tunafeli kwa sababu ya kutotekeleza na si ya kilimo tu, sehemu nyingi sana tunaposikia kuna matatizo, ni kwa sababu ya utekelezaji na usimamizi wa Sheria zetu tunazozitunga haupo. Sasa itakuwa tunarundika Sheria tu au mipango tu, utekelezaji haupo, itakuwa kazi gani! Ni afadhali tuamue sasa na kama kweli tulishaamua basi tutekeleze kwa maslahi ya nchi yetu na watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninao wachangiaji wachache ambao hawako ndani ya Ukumbi huu. Nilipokuwa nakuja kuketi kwenye Kiti cha Spika kipindi hiki cha jioni maelekezo ya Muswada huu niliyoyapokea ni kwamba, tutaumaliza kesho.

Sasa naacha kazi kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Spika kwa maana ya Makatibu wa Bunge kuona kama hawa wachangiaji waliobakia wanaweza kupata nafasi kesho na wao wakatupa mawazo yao. Halafu tutapeana muda ili Wizara ijiandae kujibu hoja ili tuweze kuhitimisha.

Kwa maneno mafupi ya kikanuni ni kwamba, ratiba ya shughuli za Bunge, Ofisi ya Mheshimiwa Spika itaipanga kwa mujibu wa Kanuni tutaipata asubuhi na tutajua tunaendeleaje na hivyo tutahitimisha hoja hii kwa ratiba hiyo kwa namna itakavyokuwa imepangwa.

Kwa hiyo, baada ya kusema maneno haya, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu na naahirisha shughuli hizi za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi ndani ya Ukumbi huu.

*(Saa 1.15 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 30 Agosti, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*